**ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR**

| | | |
|---|---|---|
| **MHE. ZUBEIR ALI MAULID** | **-** | **SPIKA** |
| 1. Mhe. Mgeni Hassan Juma | - | Naibu Spika/ Nafasi za Wanawake |
| 2. Mhe. Mwanaasha Khamis Juma | - | Mwenyekiti wa Baraza/ Jimbo la Chukwani |
| 3. Mhe. Shehe Hamad Mattar | - | Mwenyekiti wa Baraza/ Jimbo la Mgogoni |
| 4. Mhe. Balozi Seif Ali Iddi | - | MBM/Makamu wa Pili wa Rais /Kiongozi wa Shughuli za Serikali/ Jimbo la Mahonda |
| 5. Mhe. Issa Haji Ussi (Gavu) | - | MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Jimbo la Chwaka |
| 6.Mhe. Haji Omar Kheri | - | MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ/ Jimbo la Tumbatu |
| 7. Mhe. Haroun Ali Suleiman | - | MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma |

| | | |
|---|---|---|
| | | na Utawala Bora /Jimbo la Makunduchi |
| 8. Mhe. Mohammed Aboud Mohammed | - | MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar/ Uteuzi wa Rais |
| 9. Mhe. Dkt. Khalid Salum Mohamed | - | MBM/Waziri wa Fedha na Mipango /Jimbo la Donge |
| 10. Mhe.Mahmoud Thabit Kombo | - | MBM/Waziri wa Afya/ Jimbo la Kiembesamaki |
| 11. Mhe. Riziki Pembe Juma | - | MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali / Nafasi za Wanawake |
| 12. Mhe. Balozi Amina Salum Ali | - | MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko Zanzibar/ Uteuzi wa Rais |
| 13. Mhe. Balozi Ali Abeid Karume | - | MBM/Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji/ Uteuzi wa Rais |
| 14. Mhe. Rashid Ali Juma | - | MBM/Waziri wa Habari, Utalii na Michezo/Jimbo la Amani |
| 15. Mhe. Hamad Rashid Mohamed | - | MBM/Waziri wa Kilimo, |

| | | |
|---|---|---|
| | | Maliasili, Mifugo na Uvuvi/ Uteuzi wa Rais |
| 16. Mhe. Maudline Cyrus Castico | - | MBM/Waziri wa Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto/ Uteuzi wa Rais |
| 17. Mhe. Salama Aboud Talib | - | MBM/Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira/ Nafasi za Wanawake |
| 18. Mhe. Juma Ali Khatib | - | MBM/ Waziri Asiekuwa naWizara Maalum/Uteuzi wa Rais |
| 19. Mhe. Said Soud Said | - | MBM/Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/ Uteuzi wa Rais |
| 20. Mhe. Khamis Juma Mwalim | - | Naibu Waziri, Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora/ Jimbo la Pangawe |
| 21. Mhe. Mihayo Juma N'hunga | - | Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa pili wa Rais wa Zanzibar/ Jimbo la Mwera |

| | | |
|---|---|---|
| 22. Mhe. Shamata Shaame Khamis | - | Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ / Jimbo la Micheweni |
| 23. Mhe. Harusi Said Suleiman | - | Naibu Waziri wa Afya/ Jimbo la Wete |
| 24. Mhe. Mmanga Mjengo Mjawiri | - | Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali /Jimbo la Mkoani |
| 25. Mhe. Mohamed Ahmada Salum | - | Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji / Jimbo la Malindi |
| 26. Mhe. Chum Kombo Khamis | - | Naibu Waziri wa Habari, Utalii na Michezo/Nafasi za Wanawake |
| 27. Mhe. Shadya Mohamed Suleiman | - | Naibu Waziri wa Uwezeshaji,Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto/ Nafasi za Wanawake |
| 28. Mhe. Lulu Msham Abdalla | - | Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi/ Nafasi za Wanawake |

| | | |
|---|---|---|
| 29. Mhe. Juma Makungu Juma | - | Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira/ Jimbo la Kijini |
| 30. Mhe. Abdalla Ali Kombo | - | Jimbo la Mwanakwerekwe |
| 31. Mhe. Abdalla Maulid Diwani | - | Jimbo la Jang'ombe |
| 32. Mhe. Ahmada Yahya Abdulwakil | - | Uteuzi wa Rais |
| 33. Mhe. Ali Khamis Bakar | - | Jimbo la Tumbe |
| 34. Mhe. Ali Salum Haji | - | Jimbo la Kwahani |
| 35. Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata) | - | Jimbo la Kijitoupele |
| 36. Mhe. Ame Haji Ali | - | Jimbo la Nungwi |
| 37. Mhe. Amina Iddi Mabrouk | - | Nafasi za Wanawake |
| 38. Mhe. Asha Abdalla Mussa | - | Jimbo la Kiwengwa |
| 39. Mhe. Bahati Khamis Kombo | - | Jimbo la Chambani |
| 40. Mhe. Bihindi Hamad Khamis | - | Nafasi za Wanawake |
| 41. Mhe. Hamad Abdalla Rashid | - | Jimbo la Wawi |
| 42. Mhe. Hamida Abdalla Issa | - | Nafasi za Wanawake |
| 43. Mhe. Hamza Hassan Juma | - | Jimbo la Shaurimoyo |
| 44. Mhe. Hassan Khamis Hafidh | - | Jimbo la Welezo |
| 45. Mhe. Hidaya Ali Makame | - | Nafasi za Wanawake |

46. Mhe. Hussein Ibrahim Makungu (Bhaa) - Jimbo la Mtoni

47. Mhe. Jaku Hashim Ayoub - Jimbo la Paje

48. Mhe. Khadija Omar Kibano - Jimbo la Mtambwe

49. Mhe. Machano Othman Said - Jimbo la Mfenesini

50. Mhe. Dkt. Makame Ali Ussi Makoti - Jimbo la Mtopepo

51. Mhe. Makame Said Juma - Jimbo la Kojani

52. Mhe. Maryam Thani Juma - Jimbo la Gando

53. Mhe. Masoud Abrahman Masoud - Jimbo la Bububu

54. Mhe. Miraji Khamis Mussa - Jimbo la Chumbuni

55. Mhe. Moh'd Mgaza Jecha - Jimbo la Mtambile

56. Mhe. Mohamed Said Mohamed - Jimbo la Mpendae

57. Mhe. Mohammedraza Hassanaali Mohamedali- Jimbo la Uzini

58. Mhe. Mtumwa Peya Yussuf - Jimbo la Bumbwini

59. Mhe. Mtumwa Suleiman Makame - Nafasi za Wanawake

60. Mhe. Mussa Ali Mussa - Jimbo la Ole

61. Mhe. Mussa Foum Mussa - Jimbo la Kiwani

62. Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa - Nafasi za Wanawake

63. Mhe. Mwantatu Mbaraka Khamis - Nafasi za Wanawake

64. Mhe. Dkt Mwinyihaji Makame Mwadini - Jimbo la Dimani

65. Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy- Jimbo la Chaani

| | | |
|---|---|---|
| 66. Mhe. Nassor Salim Ali | - | Jimbo la Kikwajuni |
| 67. Mhe. Omar Seif Abeid | - | Jimbo la Konde |
| 68. Mhe. Panya Ali Abdalla | - | Nafasi za Wanawake |
| 69. Mhe. Rashid Makame Shamsi | - | Jimbo la Magomeni |
| 70. Mhe. Saada Ramadhan Mwendwa | - | Nafasi za Wanawake |
| 71. Mhe. Said Omar Said | - | Jimbo la Wingwi |
| 72. Mhe. Said Hassan Said | - | Mwanasheria Mkuu |
| 73. Mhe. Salha Mohamed Mwinjuma | - | Nafasi za Wanawake |
| 74. Mhe. Salma Mussa Bilal | - | Nafasi za Wanawake |
| 75. Mhe. Shaib Said Ali | - | Jimbo la Chonga |
| 76. Mhe. Simai Mohammed Said | - | Jimbo la Tunguu |
| 77. Mhe. Sira Ubwa Mamboya | - | Uteuzi wa Rais |
| 78. Mhe. Suleiman Makame Ali | - | Jimbo la Ziwani |
| 79. Mhe. Suleiman Sarahan Said | - | Jimbo la Chakechake |
| 80. Mhe. Tatu Mohamed Ussi | - | Nafasi za Wanawake |
| 81. Mhe. Ussi Yahya Haji | - | Jimbo la Mkwajuni |
| 82. Mhe. Viwe Khamis Abdalla | - | Nafasi za Wanawake |
| 83. Mhe. Wanu Hafidh Ameir | - | Nafasi za Wanawake |
| 84. Mhe. Yussuf Hassan Iddi | - | Jimbo la Fuoni |
| 85. Mhe. Zaina Abdalla Salum | - | Nafasi za Wanawake |

86. Mhe. Zulfa Mmaka Omar - Nafasi za Wanawake

Ndugu Raya Issa Msellem - Katibu wa Baraza la Wawakilishi

**Kikao cha Ishirini na Nne – Tarehe 08 Juni, 2017**

*(Kikao kilianza saa 3:00 asubuhi)*

**DUA**

*Mhe. Mwenyekiti (Mwanaasha Khamis Juma) alisoma Dua*

**MASWALI NA MAJIBU**

**Nam. 145**

**Ukiukwaji wa Utaratibu wa *One Way* Kwa Barabara za Kwa Hajitumbo – Mchangani**

**Mhe. Dkt. Mwinyihaji Makame Mwadini** - Aliuliza:

Kuanzia siku za nyuma hadi hivi sasa barabara za Kwahajitumbo, Mlandege na Mchangani (mjini) ni za kupita kwa njia moja tu *(one way).*

(a) Wizara haijagundua tatizo liliopo siku hizi kwa madereva hasa wenye vyombo vya moto *(motor cycles)* na baiskeli kuvunja utaratibu wa *one-way*.

(b) Je, wahalifu wangapi walikamatwa kwa kipindi cha miezi 6 iliyopita.

(c) Je, ni lini Wizara itashirikiana na askari wa barabarani kukomesha hali hiyo.

**Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais –** Alijibu:

Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Dkt. Mwinyihaji Makame Mwakilishi swali lake Nam. 145 lenye vifungu (a) (b) na (c). Naomba kutanguliza maelezo mafupi kama yafuatayo:-

Mhe. Mwenyekiti, ni kweli kuanzia siku za nyuma hadi hii leo barabara za Kwahajitumbo, Mlandege na Mchangani ni za kupita kwa njia moja tu *(one way traffic).*

Mhe. Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo mafupi sasa naomba kumjibu Mhe. Mjumbe swali lake kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Mwenyekiti, Wizara imegundua tatizo la Madereva hususan wenye vyombo vya moto *(motor cycles)* na baiskeli kuvunja utaratibu wa *one way* ila kwa sasa utaratibu wa zamani wa kuwapanga askari kupiga doria katika maeneo hayo na mengineyo kumepungua, kwa sababu ya kuongezeka kwa shughuli za kusimamia barabara katika njia kuu kutokana na upungufu wa Askari wa Usalama Barabarani uliopo. Hata hivyo, operesheni ya kuzuia makosa katika njia hizo hufanywa kwa kushitukiza badala ya kuwa ni utaratibu wa kazi za kawaida.

(b) Mhe. Mwenyekiti, katika kipindi cha miezi sita iliyopita hakujakamatwa kesi katika maeneo ya njia hizo.

(c) Mhe. Mwenyekiti, Wizara yangu ipo karibu sana na Jeshi la Polisi na tumekuwa tukishirikiana katika mambo mengi pamoja na hili la kusimamia sheria za nchi ikiwemo hili la uvunjifu wa Sheria za Usalama Barabarani.

**Mhe. Dkt. Mwinyihaji Makame Mwadini:** Mhe. Mwenyekiti, namshukuru sana Mhe. Naibu Waziri wa Ofisi ya Makamu wa Pili ya Rais kwa majibu yake. Naomba nimuulize swali moja la nyongeza lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mhe. Mwenyekiti, sheria za nchi lazima zifuatwe na tunapozungumzia suala la demokrasia nchini basi suala zima la usimamizi wa sheria nchi, sasa tukiwaachia watu kwa makusudi wanavyunja sheria kwa kweli suala la utawala bora halipo.

Naomba sasa, kwa nini wizara yake haisimami askari polisi kama tunavyowaona wengine, kama leo wako *round about* matofalini wanakamata gari zisizokuwa na leseni na pikipiki. Hivyo, kwa nini na wao hawaendi kwenye barabara za Kwahajitumbo, Mlandege, Mchangani kuzuia wimbi la watu wanaofanya makusudi kupita *one way* wao wanakwenda vyengine. (*Makofi*)

**Mhe. Naibu Waziri wa Ofisi ya Rais Makamu wa Pili wa Rais:** Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Dkt. Mwinyihaji Makame Mwadini swali lake la nyongeza kama ifuatavyo.

Mhe. Mwenyekiti, kama ambavyo nimejibu katika jibu langu la msingi si dhamira ya serikali wala Jeshi la Polisi kutokuwacha kusimamia sheria za nchi, dhamira kubwa na wajibu mkubwa wa kuhakikisha kuwa sheria zote zinazotungwa katika nchi hii zinasimamiwa ipasavyo katika maeneo yetu. Lakini tumekuwa na upungufu kidogo wa askari wa *traffic* katika maeneo yetu, ndio

maana tumeweka kipaumbele zaidi katika zile *main road* kama ambavyo ulivyotoa mfano. Lakini pia Jeshi la Polisi halikusita kwenda kufanya doria za kushtukiza katika eneo lile kadri ambavyo wamekuwa wakijitahidi kufanya, ili kuweza kupunguza ule msongamano. Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru.

**Mhe. Ali Salum Haji:** Ahsante Mhe. Mwenyekiti pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri naomba kumuuliza swali la nyongeza lenye vifungu (a) na (b).

(a) Mhe. Naibu Waziri, wakati anatujibu hapa swali la msingi amesema kwamba wameweka umuhimu katika njia ya *main road*, anataka kutwambia hizi njia ambazo zimezungumzwa hapa za Kwahajitumbo na Mchangani hazina umuhimu wa kupelekwa hao polisi. Katika jibu lako Mheshimiwa kwamba umepeleka umuhimu katika njia za *main road* maana unataka kutwambia hizi njia zilizozungumzwa hazina umuhimu.

(b) Mhe. Mwenyekiti, pamoja na suala lililozungumzwa la watu kuvunja sheria na utawala bora kutokupatikana katika njia hizi. Lakini pia kuna watu wanaovunja sheria ya kuuza biashara kwenye barabara hizi. Je, hili nalo analiangalia vipi.

**Mhe. Naibu Waziri wa Ofisi ya Rais Makamu wa Pili wa Rais:** Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Ali Salum Haji swali lake la nyongeza lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo.

Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyojibu katika jibu langu la msingi nilivyosema njia hizi hazikuwa na umuhimu haikumaanisha kwamba umuhimu wake unalingana na zile njia *main road*, kuna *main road* na *internal road* katika barabara zetu. Kwa maana hiyo, katika zile njia za *main road* kuna wajibu wa kuhakikisha

muda wote zinakuwa katika hali ya usalama na ulinzi unakuwa umeimarishwa vizuri. Lakini katika hizi njia za ndani kidogo ambazo na zenyewe zina umuhimu wake kutokana na mahitaji ya watu wanaokwenda katika maeneo hayo ya Kwahajitumbo na maeneo mengine, ndio maana tukawa tunaweka ulinzi wa kushtukiza kadri ambavyo mahitaji yamekuwa yakitokea.

(a) Lakini dhamira yetu ni kuhakikisha kwamba pale tunapopata nguvu ya kutosha barabara zetu zote hizi tutaziwekea ulinzi mzuri na kutosha.

(b) Mhe. Mwenyekiti, suala la njia za ndani kuvamiwa na baadhi ya wafanyabiashara kweli hata sisi serikali tumekuwa tukiliona hilo linatukera. Lakini tumhakikishie Mhe. Mjumbe tu kwamba tutalichukua jambo hili tutalizingatia tutakaa na wenzetu wafanyabiashara, ili kuweza kuwawekea mazingira yaliyo mazuri zaidi kwa kushirikiana na taasisi zinazohusika za Manispaa na Baraza la Mji katika maeneo yetu mbali mbali. Nakushukuru Mhe. Mwenyekiti.

**Mhe. Ali Suleiman Ali:** Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais kwa ruhusa yako naomba kuuliza swali la nyongeza.

Mhe. Mwenyekiti, katika mazingira tuliyokuwa nayo katika nchi yetu sheria za barabarani nyingi zinavunjwa na hasa vyombo vidogo vidogo baskeli na pikipiki au vespa. Kwa kuzingatia hilo utakuta baadhi ya barabara vyombo vinakwenda mwendo wa kasi kupindukia kiwango, *exhausts* zimepasuliwa na kusababisha kero kwa wananchi.

Lakini pamoja na hayo kwa kuwa barabara hizo zilizoguswa wananchi wengi wanapata ajali ambazo hawazitarajii kwa kupitwa upande ambao hawahusiki na vyombo hivyo. Wizara pamoja na juhudi za kukamata vyombo vya magari na pikipiki barabara kuu hawawezi kuwaweka askari maalum kuanzia upande wa Kwahajitumbo na hao Kwabiziredi au kutoka Mlandege mpaka Darajani kukamata vyombo hivi ambavyo vinaleta adha kwa wananchi ambao ni kero katika mzunguko wa wananchi wetu kusababisha ajali zisizokuwa na msingi.

**Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais:** Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Ali Suleiman Ali swali lake moja la nyongeza kama ifuatavyo.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza kabisa naomba kutumia fursa hii kuwaomba na kuwanasihi sana vijana na baadhi ya watu wengine ambao wamekuwa wakitumia vyombo vya maringi mawili, pikipiki pamoja na baiskeli, hasa wale wanaotumia pikipiki vyombo vya maringi mawili na wanaokwenda kwa kasi katika mazingira hatari. Jeshi letu la Polisi limekuwa likifanya kazi kubwa ya kuwazuia watu hawa, lakini bado limekuwa likifanya jitihada kubwa za kuhakikisha kadhia hii inapungua. Lakini tuendelee kuwanasihi sana, ni vyema taratibu, sheria na kanuni za usalama wa barabarani zikafuatwa kuanzia kwa hawa wanaotumia vyombo vya maringi mawili kwa kufuata sheria zetu na pia kuwatazama afya zao pale ambapo wamekuwa wakipata matatizo ya ajali.

**Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais:** Mhe. Mwenyekiti, baada ya majibu mazuri sana ya Mhe. Naibu Waziri naomba pia niongezee majibu ya nyongeza kama ifuatavyo.

Lakini kabla ya kufanya hivyo ningependa sana nimpongeze sasa muuliza swali la msingi na masuala yote ya nyongeza yenye dhamira ya dhati kabisa katika kuhakikisha usalama katika barabara zetu. Imeonesha wazi Waheshimiwa Wawakilishi katika Baraza lako Tukufu dhamira yao ya kuwahurumia wananchi wetu na pale wanapoyaona makosa wanataka hatua za dharura zichukuliwe ili kuondoa makosa hayo.

Nataka niwahakikishie Baraza lako Tukufu kwamba tutawasiliana na Jeshi la Polisi ili tuwe na mpango maalum wa kusimamia maeneo waliyoyataja kwa ajili ya kuondoa kadhia na yale maeneo vile vile. Kuna baadhi ya vijana wanazitumia vibaya barabara hizi ama kwa kuendesha mbio pikipiki zao au vyombo vyengine pamoja na kutoboa makusudi *exhausts* zao, ili wafanye kelele barabarani kwa furaha zao. Tutahakikisha kwamba tunaweka utaratibu maalum kwa hao kuwashughulikia mara moja. Naomba nitoe wito kwa wenye mitindo ya namna hiyo hususan vijana kuacha mara moja, pamoja na wale wanaotumia barabara za nje ya mji kwa kurusha mapikipiki juu na kwenda mwendo wa kasi wote hawa tutawashughulikia ipasavyo. Kwa hivyo, naomba sana waache mara moja. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.

## UTARATIBU

**Mhe. Ali Suleiman Ali:** Baada ya swali la kwanza kuna swali la Mhe. Suleiman Sarahan Said, kwa bahati mbaya hakulisema labda kalifuta tu hatukujua Mhe. Mwenyekiti.

**Mhe. Mwenyekiti:** Mhe. Mjumbe, hiyo ni kuhusu taarifa, utaratibu sijui umezungumza kanuni gani. Lakini Mheshimiwa nisikilize na mimi, umeomba muongozo kwa hiyo naomba unisikilize.

**Mhe. Ali Suleiman Ali:** Muongozo Mhe. Mwenyekiti.

**Mhe. Mwenyekiti:** Ndio nakujibu nimekufahamu hamna tatizo, kiti kina maamuzi kuna suala limejitokeza tumeombwa, kwa hiyo tumeanza la swali la Mhe. Jaku Hashim Ayoub na baadae litafuatia hilo swali la Mhe. Suleiman Sarahan Said na wala hakuna tatizo. Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira.

**Nam. 77**

**Ahadi ya Kutatuliwa Shida Kubwa ya Maji kwa Wananchi wa Michamvi**

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub**– Aliuliza:

Mnamo tarehe 13/10/2015 wakati Mhe. Rais wa Zanzibar akiwa Chwaka kufanya kampeni za Uchaguzi Mkuu, alimnadi mgombea uwakilishi wa jimbo hilo na moja kati ya ahadi zake aliahidi kuwa atahakikisha maji yanapatikana kwa asilimia 100. Kwa kuwa Michamvi ni sehemu ambayo mgombea aliyenadiwa na Dkt. Ali Mohamed Shein anatokea, na kwa kuwa tangu dahari dunia iumbwe maji hayajapatikana.

Je, serikali kupitia wizara ipo tayari kutafuta njia ya haraka kutekeleza ahadi ya Mhe. Dkt. Ali Mohamed Shein siku ile ya kampeni kwa wananchi wa Michamvi kupatiwa maji ya uhakika.

**Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira** – Alijibu:

Mhe. Mwenyekiti, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Jaku Hashim Ayoub swali lake Nam. 77 kama ifuatavyo:-

Mhe. Mwenyekiti, serikali kupitia Wizara ya Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira imekuwa ikifanya jitihada mbali mbali za kuwapatia wananchi wa Michamvi huduma ya maji safi na salama, baada ya kisima kilichokuwa kinahudumia hapo awali kupoteza uwezo wake. Miongoni mwa juhudi hizo ni pamoja na ufungaji wa mitambo ya kuchuja maji ya chumvi na kuwa ya kunywa *(Reverse Osmosis Desalination System)* kwa kushirikiana na Kampuni ya *UST* ya Ujerumani kwa ajili ya wakaazi wa viijiji vya Michamvi Pingwe na Michamvi Kae.

Aidha, katika kutafuta njia ya haraka na ya uhakika serikali kupitia mradi wa *Ras al Khaimah* imechimba visima na kujenga tangi katika eneo la Bwejuu. Vile vile, wizara yangu imeandaa makisio ya gharama za kukamilisha kazi zilizobakia ambapo jumla ya shilingi 1.8 bilioni zinahitajika. Mara tu fedha hizo zitakapopatikana wizara yangu itakamilisha kazi hiyo katika kipindi kifupi kadri iwezekanavyo.

Hivyo, namuomba Mhe. Mwakilishi na wananchi wa eneo hilo kuwa wastahamilivu wakati jitihada za kutafuta njia ya haraka na ya uhakika kwa tatizo hili zinaendelea.

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub:** Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri kutokuwa na afya. Naomba kumuuliza maswali madogo ya nyongeza.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri alipokuwa akijibu swali la msingi alisema kuwa wanafanya jitihada mbali mbali kuwapatia wananchi wa Michamvi huduma ya maji safi na salama. Hebu atwambie hatua gani alizochukua kwa wananchi wa Michamvi mpaka muda huu na siku zote huwa nasimama kupiga kelele kwamba toka dunia kuanza maji kule hayajatoka. Huu mradi alioutaja leo miaka mitatu na mimi mchango wangu ni mkubwa

sana sio milioni moja, sio milioni mbili katika mradi wa maji ya *dissection* ikiwemo kutandika msingi kutoka karibu sijui mita ngapi. Mhe. Naibu Waziri alipokuwa akijibu swali Nam. 8 tarehe 23/5/2016 la Mhe. Bahati Khamis Kombo alijibu vipi.

"Mhe. Spika, serikali haiogopi hasara kwa kunufaisha wananchi wake. Tutafanya hivyo hata mara kumi kuhakikisha tu maji safi na salama yanawafika wananchi."

Sasa hapa tukamate lipi. Kama kweli serikali haiogopi hasara, haoni kama Baraza hili amelidanganya na tokea kuanza dunia Michamvi hakujawahi kutoka maji, haya ni maneno yake sio maneno yangu. Narudia tena Mhe. Mwenyekiti *hansard* hii:

"Mhe. Spika, serikali haiogopi hasara kwa kunufaisha wananchi wake. Tutafanya hivyo hata mara kumi kuhakikisha tu maji safi na salama yanawafika wananchi. Tulifanya hivyo Chambani."

Hivyo hapa tukamate kipi. Si suala la juzi na sasa tokea dunia kuanza na hivi juzi alijibu swali hili haoni majukumu yake yamemshinda sasa hivi na analidanganya Baraza. *(Makofi)*

**Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira:** Mhe. Mwenyekiti, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Jaku Hashim Ayoub swali lake la nyongeza kama ifuatavyo.

Lakini kabla ya kumjibu nikiri kuwa nilisema kwamba serikali haiwezi kukwepa gharama kwa kuwahudumia wananchi. Lakini afahamu kwamba serikali hiyo imefanya jitihada nyingi za kuhakikisha wananchi wa Paje wanapata maji.

(a) Kama nilivyokuwa nimesema kuna ule mradi ambao unabadilisha maji chumvi kwenye maji ya kunywa na ilikuwa inafika mpaka kule ambapo anasema sasa hayafiki, lakini lililotokezea ni kwamba baadhi ya wananchi waliokuwa si waaminifu wamekata mipira na yeye mwenyewe ni shahidi. Lakini jengine *ZAWA* kama *ZAWA* imekuwa ikifanya namna ya kuhakikisha wanapata maji.

(b) Nichukue nafasi hii kumpongeza kwa dhati Ndg. Haji Makame Simai ambaye alikuwa ni mfanyakazi wa *ZAWA* anasaidia kuhakikisha wananchi wa pale wanapata maji ya kunywa. Hata pale ambapo *ZAWA* tunajaribu kumpa mafuta wakati mwengine anasema hapana, wakati maji yapo basi tuhakikishe yanafika.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza tuna uhakika kwamba wananchi wa Michamvi maji hayatoshi lakini maji ya kunywa wanayapata. Hivyo, nimuombe tu Mhe. Mwakilishi aungane na jitihada hizi ambazo tunazifanya za kuhakikisha wananchi wa Michamvi wanapata maji. Lakini tuna mazungumzo na wafadhili kuhakikisha kwamba tunafanya mradi mwengine maalum wa kupeleka maji kule. Hata hivyo, panahitajika mashirikiano ya dhati kuhakikisha tunafanikisha hilo pamoja na mipira ambayo itatandikwa haitaharibiwa. Ahsante sana.

**Nam. 162**

**Ulipaji wa Mishahara Kinyume na Taratibu za Sheria**

**Mhe. Suleiman Sarahan Said -** Aliuliza:

Mhe. Mwenyekiti, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa nia safi ya kutaka kuleta maendeleo imejitahidi kuziba mianya ya uvujaji wa mapato na matumizi holela. Hata hivyo, kuna suala la wafanyakazi au wateule wa Mhe. Rais huteuliwa ambao hufanya

kazi na kulipwa mishahara yao, lakini pindi uteuzi unapokwisha kwa kutenguliwa, mtu yule huendelea kupokea mishahara ule ule.

(a) Je, hili serikali inalijua na ndio utaratibu au mazoea.

(b) Kama hivyo ndivyo, hatuoni tunamlipa mtu asiyefanya kazi.

(c) Kwani katika kuteuliwa hakuna mikataba yake ya kumaliza kazi na kumpa kiinua mgongo chake ili kumalizana kwa hilo, kuliko kumlipa mshahara kinyume na utaratibu.

**Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi (Kny. Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora) -** Alijibu:-

Mhe. Mwenyekiti, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 162 lenye kifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

Mhe. Mwenyekiti, kwanza naomba kutoa maelezo mafupi kama ifuatavyo:-

Mhe. Mwenyekiti, kwa mujibu wa taratibu za utumishi wa umma, hakuna mfanyakazi au mtumishi yeyote katika utumishi wa umma ambaye analipwa stahiki zile zile kwa mujibu wa wadhifa au cheo chake baada ya kutenguliwa wadhifa wake. Kwa mujibu wa utaratibu uliopo katika utumishi wa mma, stahiki za wateuliwa wote wa Mhe. Rais hulipwa kwa utaratibu maalum ikiwa ni pamoja na mshahara jumuishi, posho la mafuta na posho maalum kwa baadhi ya wateuliwa.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo sasa naomba kumjibu kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Mwenyekiti, kwa mujibu wa utaratibu huo, pindi mtumishi anapokosa uteuzi au kutenguliwa uteuzi wake hubakiwa na mshahara jumuishi tu na kuondolewa malipo ya posho zilizobakia. Hakuna utaratibu wa kuendelea kumlipa stahiki nyingine mtumishi ambaye uteuzi wake umetenguliwa au haukufanyika tena.

Mhe. Mwenyekiti, aidha kwa mujibu wa Kanuni za Utumishi wa Umma, Kanuni Nam. 23(1) inaeleza kwamba naomba kunukuu:

"Mtumishi yeyote anaweza kustaafu kwa hiari atakapofika umri wa miaka 55 baada ya kukubaliwa na Tume ya Utumishi husika. Aidha, kwa mteuliwa wa Mhe. Rais anaweza kustaafu kwa hiari baada ya kuwasilisha ombi lake kwa Mhe. Rais kupitia kwa Katibu Mkuu Kiongozi."

(b) Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa hakuna utaratibu wa kumlipa stahiki za mteuliwa mtumishi aliyekosa uteuzi, hivyo haiwezekani kumlipa mtu asiyefanya kazi mshahara huo kama mhusika.

(c) Mhe. Mwenyekiti, mteuliwa yeyote anapokosa uteuzi, basi hutakiwa arudi katika kazi yake kwa mujibu wa taaluma yake na kulipwa mshahara unaostahiki bila ya marupurupu ya wateuliwa.

**Mhe. Suleiman Sarahan Said:** Mhe. Mwenyekiti, nimshukuru sana Mhe. Waziri kwa majibu yake mazuri. Naomba kumuuliza Mhe. Waziri.

(a) Baada ya kumaliza kazi katika kuteuliwa kwake, ni muda gani anaweza kupokea mshahara ule ule wa uteuzi ambao atadumu nao kwa muda gani katika uteuzi ule baada ya kuwa hana kazi tena.

(b) Kutokana na muda ambao wanaofanyia kazi na mtu yule ameteuliwa katika kada fulani. Je, katika malipo yake ya kiinua mgongo inajumuishwa kutoka kule katika kiwango kile kile au anabaguliwa mishahara yake.

**Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi (Kny. Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora):** Mhe. Mwenyekiti, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza lenye vifungu (a) na (b) kama hivi ifuatavyo.

(a) Mhe. Mwenyekiti, inapoundwa serikali, unapofanyika uteuzi, maana yake ni kama ile hesabu ya wale wateuliwa ndio wanaolipwa mshahara, kama yule hayumo katika wale wateuliwa hawezi kupata mshahara huo kwa nafasi ya mteuliwa. Hivyo, mara tu baada ya kukosa uteuzi analipwa mshahara wake jumuishi bila ya marupurupu ya nafasi ya uteuzi wa Mhe. Rais.

(b) Kiingua mgongo cha mtumishi wa serikali kinalipwa kutokana na mshahara wake na sio marupurupu yake. *(Makofi)*

**Nam. 87**

**Hatua za Kuwasaidia Udhibiti wa Maji ya Mvua Katika Mabonde ya Mpunga Pemba**

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub -** Aliuliza:

Mhe. Mwenyekiti, kumekuwa na malalamiko kwa wakulima wa mpunga Pemba kuhusu uvamizi wa maji ya chumvi kwenye mabonde ya mpunga, hali inayoathiri maendeleo ya kilimo hicho kwa wakulima hao.

Je, hatua gani za muda mfupi na muda mrefu serikali imepanga kuzichukua, ili kudhibiti mabadiliko ya tabia ya nchi kwa maji ya chumvi kuvamia mabonde ya mpunga.

**Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi -** Alijibu:

Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 87 kama ifuatavyo:-

Mhe. Mwenyekiti, kazi ya uratibu wa uvamizi wa maji ya chumvi katika maeneo ya visiwa vyetu yakiwemo mabonde ya mpunga ni suala mtambuka. Hivyo, serikali kupitia taasisi zilizo chini ya Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ, Wizara ya Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira na Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi zinashirikiana katika kukabiliana na changamoto ya uvamizi wa maji ya chumvi katika maeneo ya visiwa vyetu yakiwemo mabonde ya mpunga.

Mhe. Mwenyekiti, serikali tayari imeyaainisha maeneo 161 (Unguja 36 na Pemba 125) ambayo yameathirika na uingiaji wa maji ya chumvi ambayo mengi ya maeneo hayo ni maeneo muhimu kwa kilimo hasa cha mpunga. Aidha, mmong'onyoko wa

fukwe na maeneo ya makaazi ya watu pia ni miongoni mwa athari zinazoongezeka siku hadi siku.

Mhe. Mwenyekiti, tafiti zilizofanyika zimeonesha kwamba athari ya uvamizi wa maji ya chumvi zimesababishwa na mabadiliko ya hali ya hewa na mwenendo wa mifumo ya hewa ya kidunia pamoja uharibifu wa mazingira unaotokana na kuongezeka kwa gesijoto, kuongezeka kwa kina cha maji ya bahari na ukataji wa misitu hasa mikandaa ambayo inasaidia sana katika kuzuia mmong'onyoko wa sehemu za fukwe katika maeneo husika.

Mhe. Mwenyekiti, tafiti zimeonesha athari kama hizi ambazo husababishwa na mabadiliko ya hali ya hewa na mwenendo wa mifumo ya hewa zinapotokea ni vigumu kuzizuia ila jambo la muhimu ni kusaidia waathirika kuweza kuhimili athari hizo. Pia gharama za kukabiliana na athari hizo ni kubwa.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo sasa naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, katika kukabiliana na athari za uvamizi wa maji ya chumvi katika mabonde ya mpunga, serikali imeandaa mipango na mikakati ya kuhimili athari za mabadiliko ya hali ya mwenendo wa mifumo ya hewa Zanzibar ambayo ndani yake zimeainishwa hatua za muda mfupi na za muda mrefu.

Mhe. Mwenyekiti, hatua za muda mfupi ni pamoja na upandaji wa mikoko, mikandaa ambayo husaidia kuzuia mmong'onyoko wa ardhi na kutoa elimu kwa wanajamii kuhusiana na madhara ya uharibifu wa mazingira na hatua mahsusi zinazopaswa kuchukuliwa katika kuyatunza. Ujenzi wa matuta na kuta ili kuzuia uvamizi wa maji ya chumvi katika maeneo husika na kuendeleza matumizi ya nishati mbadala katika ngazi zote, ili

kupunguza uharibifu wa misitu na uzalishaji wa gesijoto kwa ujumla ni miongoni mwa hatua za muda mfupi.

Mhe. Mwenyekiti, hatua za muda mrefu ni pamoja na kufanya tafiti zitakazosaidia kukusanya taarifa za kisayansi, ili kusaidia kufanikisha shughuli za kupunguza athari za mabadiliko ya hali ya mwenendo wa mifumo ya hewa Zanzibar na kuimarisha mipango miji na vijiji katika hali endelevu.

Aidha, Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kupitia Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imesaini na kuridhia mkataba wa kimataifa *(Kyoto Protocol)* unaohusiana na makabiliano ya mabadiliko ya hali ya hewa duniani na mwenendo wa mifumo ya hewa, ambao unaelekeza pamoja na mambo mengine fidia kwa hasara na madhara yatokanayo na mabadiliko hayo, ambayo husababishwa na matendo ya binaadamu na pia zaidi na nchi zilizoendelea zenye viwanda vyenye kutoa gesijoto kwa wingi.

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub:** Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu marefu sana ya Mhe. Waziri naomba kumuuliza swali dogo la nyongeza.

(a) Mhe. Mwenyekiti, kama yeye Mhe. Waziri ni mwenye dhamana amechukua hatua gani kukutana na wananchi hawa walioathirika na mabonde haya na kwa mujibu wa takwimu. Hata jana Mhe. Mkuu wa Wilaya ya Micheweni Bwana Abeid alifanya ziara hiyo kutembelea maeneo ya kule Micheweni. Kama ni waziri mwenye dhamana amechukua hatua gani kwa wananchi hawa na ukizingatia wanatoka asili ya upande wa pili ndio walioathirika. Kwa maana hiyo, kama hajachukua hatua hizo ni lini atachukua hatua hizo kukutana nao na kuwapa maneno mazuri.

b) Walitegemea kupata kipato lakini kwa bahati mbaya Mwenyezi Mungu hakujaalia kutokana na athari hiyo. Hivyo, serikali ina jukumu kwa wananchi wake imewasaidia nini kwa kupitia wizara husika.

**Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi:** Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyoeleza katika majibu ya msingi kwanza tunafanya utafiti wa kutosha kujua kina cha athari kilichotokea na kazi hii haifanywi tu na waziri kutembelea inafanywa kitaalam. Hivyo, ni lazima wataalam waende wakafanye *proper assessment* halafu ndio wana *determine* athari iliyotokea na kwa kiasi gani athari hiyo inaweza ikadhibitiwa.

Lakini nasema zipo zile athari za kibinaadam kwa yale mambo yanayofanywa na binaadam kuathiri mazingira. Haya nafikiri tunaweza tukakabiliana nayo kwa pamoja, kwa mfano ukataji wa mikoko ovyo, maeneo ambayo yanachimbwa mchanga hayaruhusiki, maeneo yanayochimbwa vifusi na kadhalika.

Mimi nafikiri kwanza ni kudhibiti wenyewe inakuwa rahisi na serikali vile vile kuchukua hatua. Sasa katika hatua ambazo serikali inachukua mara nyingi, kwanza tumejenga maeneo mbali mbali makuta makubwa ya kuzuia maji ya bahari yasiingie. Kwa bahati mbaya, katika mvua hizi maeneo hayo mengine yameathirika tena tunaanza kurudia pale pale. Jambo ambalo ni endelevuu hasa kutokana na mambo mawili. Moja, ni sisi wenyewe binaadam. Pili, vile vile na suala zima la hali ya tabia ya nchi ilivyotokea.

Lakini la tatu, anauliza kwamba tunasaidia kiasi gani. Mhe. Mwenyekiti, tunasaidia kwa mambo mawili, kwanza kama unaifahamu Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ni serikali pekee inayotoa asilimia 75 kwa wakulima hasa wa mpunga ruzuku wao

wanachangia asilimia 25 tu. Huo ni msaada mkubwa sana hakuna serikali yoyote duniani inayofanya hivyo. Hivyo hivyo kwenye mbolea na kadhalika. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, hii ni baadhi ya misaada ambayo tunayoitoa na pale ambapo tunaona kwamba serikali lazima isaidie angalau mbegu tunafanya. Kwa mfano, ndugu zetu wa Tumbatu karibuni waliathirika tukawapelekea mbegu na kadhalika. Kwa hivyo, tunapita na kuangalia uhalisia wenyewe.

Mhe. Mwenyekiti, lakini nasema jukumu kubwa bado tunalo sisi kama wananchi kuhakikisha na sisi tunatunza mazingira yetu vizuri, ili hizi athari zinazotokea ambazo zipo nje ya uwezo wetu tuweze kuzikabili kwa pamoja.

## UTARATIBU

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub:** Utaratibu Mhe. Mwenyekiti.

**Mhe. Mwenyekiti:** Nimekuona Mhe. Jaku Hashim Ayoub kuhusu utaratibu, lakini naomba ukae tuendelee. Mhe. Suleiman Makame Ali kwa swali la nyongeza.

**Mhe. Suleiman Makame Ali:** Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, nashukuru kwa kuweza kunipa nafasi hii ya kuweza kuuliza swali dogo la nyongeza.

Kwanza, nikubaliane na majibu ya Mhe. Waziri kwamba wanatoa mbegu kwa asilimia kidogo ya pesa, ni kweli. Lakini katika majibu yake alisema kwamba wanawasaidia gharama wakulima. Mimi katika kipindi kile nilimuuliza Mhe. Naibu Waziri wake kwamba kuna wakulima wangu katika Jimbo la Ziwani maeneo ya Ndagoni, Wesha na sehemu nyengine za Michungwani

waliingiliwa na chumvi. Je, atawasaidiaje. Jibu alinijibu kwamba wakanunue hiyo mbegu.

Sasa nataka kujua hapa ni wakulima wangapi waliopata msaada kwa sababu walisema kwamba wanawasaidia gharama. Ni wakulima wangapi waliowasaidia Unguja na Pemba angalau kupata mbegu kwa mwaka wa uliopita.

**Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi:** Mhe. Mwenyekiti, wakulima wote wa mpunga ambao sasa hivi tunayo mbegu ya kutosha tunawapa kwa asilimia 75 inatoa serikali, asilimia 25 wanatoa wao. Vile vile, wanalimiwa hivyo hivyo matrekta kwa shilingi 65,000 lakini wao wanalipa shilingi 10,000.

Kwa hivyo, nasema serikali inawasaidia watu wote kwa jumla, pale inapotokezea tatizo maalum ndio pale serikali inaingilia, ili kwenda kuangalia ni kiwango gani serikali inaweza kusaidia. Lakini sio *commitment* ya serikali kwamba kila anayepata maafa serikali itaweza kusaidia. Inasaidia pale inapoona kwa kweli kuna haja ya kusaidia.

Tumefanya maeneo mengi moja tumekwenda Tumbatu tukaona hali yao mbaya sana kila kitu chao walichopanda kimeharibika, tukawasaidia mbegu ya mpunga, mtama, muhogo, inategemea mazingira na mazingira, siwezi nikasema ni jambo la jumla hapana. Kwanza na sisi wenyewe kutimiza wajibu wetu ingawa serikali inatoa msaada mkubwa sana asilimia 75 ya ruzuku ni msaada mkubwa sana haujapata kutokea katika nchi yoyote.

**Mhe. Suleiman Sarahan Said:** Nakushukuru Mhe. Mwenyekiti kwa kuniona. Mhe. Mwenyekiti, nimsifu Mhe. Waziri kwa majibu yake mazuri. Pia tupeane pole Mhe. Waziri kwa msiba wa mzee wake Mwenyezi Mungu amlaze mahali pema peponi. Amin.

Mhe. Mwenyekiti, naomba nimuulize swali moja la nyongeza lenye vifungu (a) na (b). Katika watu waliopata athari ya mabonde haya ni Tibirinzi, inawezekana Mhe. Waziri ameshafika kukagua na kuwatambua watu wale na athari zenyewe zilizotokea sifikirii tena maeneo yale kama yanaweza yakafanyika kilimo cha mpunga ambacho ndicho kilichokuwepo pale.

(a) Mhe. Waziri katika tathmini aliyoifanya je, watu wale atawalipa gharama au atawafidia kama pesa, ili kuondokana na kadhia ile au atawapa fidia ya maeneo mengine ili kwenda kulima.

(b) Ni lini fidia hii itapatikana.

**Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi:** Mhe. Mwenyekiti, kwanza nataka nikubaliane na Mhe. Suleiman Sarahan Said kwamba ni kweli bonde la Tibirinzi limevamiwa na maji chumvi. Lakini kama nilivyotoa takwimu zangu hapa ni maeneo 162, kwa hivyo sio peke yake Tibirinzi.

Mhe. Mwenyekiti, tunachofanya sasa hivi tumetuma wataalam kuangalia. Je, katika maeneo haya tunaweza tukafanya kitu chengine kwa mfano kufuga samaki na kadhalika. Kwa hivyo, huo ndio msaada tunaweza kuutoa wa kuweka aina nyengine ya ufugaji wa samaki, kaa na kadhalika.

Kutokana na hali hiyo, ndio maana nikasema kwamba tunawatuma wataalam wakafanye utafiti, wakaangalie maeneo haya tunafanya nini mbadala, ili kuwasaidia wananchi. Hata leo ukenda ukiwapa pesa kesho asubuhi watalala na njaa pale pale, lazima uwape kazi ambayo ni endelevu kwao kuweza kuwapatia kipato. Kwa maana hiyo, tunapanga huu mpango na wataalam

kwenda kuangalia maeneo halafu *then* tuone tunafanya kitu gani. Lakini *idea* ya kwanza ni kuona njia peke yake basi angalau ni kufuga samaki katika maeneo yale ili wapate mapato endelevu.

**Nam. 12**

**Kuanzishwa kwa Mashindano ya *FA***

**Mhe. Abdalla Maulid Diwani -** Aliuliza:

Mhe. Mwenyekiti, pamoja na dhamira nzuri ya mapenzi ya kupenda michezo hapa Zanzibar kwa Rais wetu wa Zanzibar Mhe. Dkt. Ali Mohamed Shein, lakini kumekuwa na malalamiko ya muda mrefu ya kusimama kwa mashindano mbali mbali ambayo ilikuwa kichocheo cha kuimarika kwa michezo hiyo.

Je, ni lini Chama cha Mpira wa Miguu Zanzibar kitaanzisha mashindano ya *FA* kama zilivyo nchi nyengine.

**Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo** - Alijibu:

Mhe. Mwenyekiti, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 12 kama ifuatavyo:-

Mhe. Mwenyekiti, nakubaliana na Mhe. Mwakilishi kuwa Mhe. Rais wetu wa Zanzibar ana dhamira nzuri na mapenzi ya kupenda michezo hapa Zanzibar. Lakini nakiri kuwa kumekuwa na malalamiko ya muda mrefu ya kusimama kwa mashindano mbali mbali ya mpira wa miguu ambayo ni kichocheo cha kuimarika kwa mchezo huo.

Mhe. Mwenyekiti, ni muda mrefu Chama cha Mpira wa Miguu Zanzibar (*ZFA*) hakijafanya mashindano ya *FA Cup*, lakini kutokana na kukubalika kuwa mwanachama kamili wa *CAF* wamelazimika kuyarejesha tena mashindano hayo. Kwani, taratibu za Shirikisho la Mpira wa Miguu Barani Afrika, mshindi wa *FA Cup* ndie atakayewakilisha nchi katika Mashindano ya Kombe la Washindi Barani Afrika. Hivyo basi, *ZFA* kwa mnasaba huo wamo katika hatua za mwisho za maandalizi ya kufanyika mashindano hayo. Ahsante Mhe. Mwenyekiti.

**Mhe. Abdalla Maulid Diwani:** Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu ya Mhe. Waziri tuyachukue hivyo hivyo tu yalivyo naomba kuuliza swali la nyongeza lenye vifungu (a) na (b).

(a) Kwa kuwa sio kigezo cha mshindi wa mashindano ya *FA* kushiriki katika mashindano ya Kombe la Washindi. Je, haoni kutochezwa mashindano hayo kwa muda mrefu kumepoteza lengo na dhamira nzima la kukua vipaji vya soka katika nchi hii.

(b) Ni lini au ni sababu gani zilizopelekea mashindano yale kutochezwa kwa muda mrefu.

**Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo:** Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti. kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Abdalla Maulid Diwani swali lake la nyongeza kama ifuatavyo.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa amesema sio kigezo kwa kutokushirikishwa timu hizi za *FA* kwamba kushiriki katika Kombe la Afrika, lakini hili katika swali mama nimemjibu kwamba hii *FA Cup* na katika masharti ya *CAF* kwamba ndio

timu ambazo zitawakilisha katika Kombe *(Cup)*. Lakini kama nilivyojibu kwamba tumo katika matayarisho ya mwisho ya kufika hatua hii ili hizi mechi au ligi zianze. Ahsante Mhe. Mwenyekiti.

**Mhe. Mwenyekiti:** Mhe. Waziri wa Afya kwa majibu ya nyongeza.

**Mhe. Waziri wa Afya:** Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru pamoja na majibu mazuri sana ya Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo na kwa bahati na mimi nimeshawahi kuwepo nafasi hiyo hiyo aliyokuwa yeye hapo kabla na tulikwenda mbio sana kwa ajili ya *CAF* pamoja na *FIFA,* tulifanikiwa kwa kiasi fulani kuleta kombe la *FIFA* hapa Zanzibar ambapo wengi miongoni mwa wananchi walipata nafasi ya kupiga picha na kombe hilo.

Mhe. Mwenyekiti, kuja kwenye swali la Mhe. Abdalla Maulid Diwani naomba kuongezea majibu ya Mhe. Naibu Waziri. Katika Katiba ya *Confederation of African Football (CAF)* linatamka kwamba *Member State should have their own internal leagues,* yaani katika nchi wanachama zote lazima ziwe na ligi zao za ndani ndio hizo alizokusudia Mhe. Diwani.

Katika zile ligi za ndani *CAF* inaruhusiwa kuwa kama *observer* kuangalia, ili waweze kufuata zile taratibu na sheria zote kupatikana mshindi ambaye atakwenda kucheza kombe la *Confederation African Nation Cup* ambapo ndio hapo mshindi wa Afrika nzima. Kwa hiyo, katika yale aliyouliza ni moja wapo jambo ambalo linataka kusimamiwa na *ZFA* hii ligi ianze haraka sana ili kutimiza haraka sana masharti ya *CAF*. Ahsante Mhe. Mwenyekiti.

**Mhe. Mwenyekiti:** Ahsante Mhe. Waziri. Nimekuona Mhe. Hidaya Ali Makame kwa swali la nyongeza.

**Mhe. Hidaya Ali Makame:** Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa na mimi nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Kwanza nimpongeze sana Mhe. Waziri kwa majibu yake mazuri, lakini pia napenda nimuulize swali dogo la nyongeza.

Kwa vile Mhe. Rais wetu wa Zanzibar anapenda sana suala la michezo na anasisitiza sana vijana kuhusu suala la michezo lakini sio tu mchezo wa mpira wa miguu. Tunafahamu kwamba michezo ya aina nyingi ikiwemo *netball*, *volleyball* na mingineyo ya kurusha mikuki na tufe na rede pia. Je, wizara ina mpango wa kuimarisha michezo hii ili nayo iweze kushindaniwa hapa kwetu Zanzibar kwa mashindano makubwa na vijana wetu waweze kunufanika na michezo hii hususan wanawake. Ahsante Mhe. Mwenyekiti. (*Makofi*)

**Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo:** Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza kama ifuatavyo.

Kwanza kabisa, naomba nimpongeze Mhe. Hidaya Ali Makame kwa kuona kwamba nao wanawake pia wanatakiwa washiriki katika michezo mbali mbali ya kitaifa na kimataifa.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli naomba nitambue na yeye pia atambue kwamba kuna vyama vya mpira, yaani kuna *ZFA*, lakini pia kuna vilabu mbali mbali ikiwemo CHANEZA. Kwa hiyo, tutashirikiana nao na tutawaita tuone kwamba mechi hizi zinaendelea kufanyika kama inavyofanyika michezo mingine ya *football*. Ahsante Mhe. Mwenyekiti.

**Mhe. Ali Khamis Bakar:** Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kunipa nafasi ya kuweza kuuliza swali la nyongeza. Vile vile nichukue fursa hii kumpongeza Mhe. Naibu Waziri kwa majibu mazuri ambayo ametupatia. Lakini pia katika swali mama alitaja neno maandalizi kwa hiyo naomba nimuulize swali kama ifuatavyo. Je, ni maandalizi gani hayo yanofanyika kufanikisha mashindano hayo.

**Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo:** Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, naomba kumjibu Mhe. Ali Khamis Bakar swali la nyongeza kama ifuatavyo.

Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyojibu kwamba tumo katika kukamilisha taratibu ili ligi hizi ziendelee kuchezwa. Taratibu ambazo tumo katika matayarisho kati ya hizo kutayarisha katiba kama ambavyo *CAF* wanataka na pia ni kupunguza utitiri wa vilabu na kufuata utaratibu ambao *CAF* wanataka. Ahsante Mhe. Mwenyekiti.

**Mhe. Mwenyekiti:** Mhe. Waziri Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa jawabu la nyongeza.

**Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenytekiti wa Baraza la Mapinduzi:** Mhe. Mwenyekiti, niendelee kumpongeza sana Mhe. Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri na mwanana naomba niongezee padogo sana. Swali la msingi lilikuwa linazungumzia suala zima la Zanzibar namna ya kuweza kuendeleza masuala haya ya *FA* yaani *Football Association*. Mashindano haya kikawaida huwa yanajumuisha timu za madaraja tofauti na yanakuwa ya nchi nzima, na ili uendeleze mashindano haya kama vile ambavyo Mhe. Naibu Waziri

amesema lazima muwe na msingi wa awali ambao ni kanuni au sheria.

Kwa hiyo, kanuni yetu itarudi baada ya kupata uanachama wa *CAF*, maana yake ni wajibu sasa kwa *ZFA* kuweza kukaa na kuandaa kanuni itakayoanzisha mashindano haya, baada ya kupatikana kanuni ambayo ndio msingi wa awali maana la pili litakalofuata itakuwa ni gharama ama mdhamini wa kuweza kuyadhamini mashindano haya. *(Makofi)*

La tatu kama vile ambayo imeweza kusemwa na Mhe. Naibu Waziri kwamba mara nyingi tunapopata uanachama wa *CAF* mnaandaa mashindano haya, ili kumuwezesha kikanuni sasa kwamba mshindi wenu atakayepatikana katika mashindano haya ya *FA* kuwa miongoni mwa washiriki watakaoshindana mashindano ya *CAF*. Kwa mfano, upande wa Tanzania Bara mwaka huu mshindi wa *FA* ni *Simba Sports Club* ambapo kwa kipindi takriban miaka mitano ataweza kupanda ndege kama inavyopanda *Dar es Salaam Young Africans*. *(Makofi)*

Lakini jambo la msingi sababu za *FA* kuchelewa ni kwamba kanuni hazipo na hatuwezi kuwa na kanuni wakati hatujapata uanachama wa shirika ambalo linakuwa linasimamia mashindano haya. Kwa hiyo, baada ya kuwa wanachama kuandaa kanuni tutatafuta mdhamini, tukipata mdhamini mashindano haya yatakuwepo. Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru.

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub:** Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, naomba na mimi kabla ya kujibiwa swali Nam. 78 niwapongeze Mawaziri leo kutuonesha mfano kuinuka wakiisaidia serikali na huu ndio wajibu wao kuisaidia serikali. Kwa kweli muda mfupi tu wameinuka mawaziri kusaidia serikali na muendelee na moyo huo huo anapopata mtu kigugumizi jibuni swali.

Baada ya maelezo hayo Mhe. Mwenyekiti, naomba serikali ijibu swali Nam. 78 ambalo mimi ni muajiri wao wananchi walionileta hapa kuja kuyasema matatizo yao.

**Nam. 78**

**Gharama za Umeme kwa Vituo vya Afya vya Vijijini**

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub –** Aliuliza:

Kwa muda mrefu sasa Vituo vya Afya vya Bwejuu, Kitogani, Jambiani na maeneo mengi mengine vimekuwa vikitumia gharama kubwa kununua umeme kwa ajili ya kuendesha shughuli zao za kuwahudumia wananchi. Mara nyingi fedha hizo wanazipata kupitia michango midogo wanayopata kutoka na baadhi ya huduma wanazotoa au kupitia fedha za mifuko za Wawakilishi wao.

Je, ni lini Wizara ya Afya itapeleka fedha za umeme kwa Vituo vya Afya vya Bwejuu, Kitogani, Jambiani na maeneo mengine ili kuvipunguzia mzigo wa kuomba fedha hizo.

**Mhe. Naibu Waziri wa Afya -** Alijibu:

Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Jaku Hashim Ayoub swali lake Nam. 78 kama hivi ifuatavyo:-

Mhe. Mwenyekiti, ni kweli kwamba tatizo hili lilijitokeza kwa muda mfupi katika kipindi kilichopita.

Mhe. Mwenyekiti, kwa sasa wizara yangu inaendelea kulipia umeme wa vituo vyake vyote vya afya kila mwezi kupitia mfuko

wake wa *Basket Fund* pamoja na fedha nyengine za kuhudumia vituo zinazopelekwa wilayani.

Mhe. Mwenyekiti, kutokana na kuongezeka kwa huduma na matumizi ya vifaa vya kisasa katika vituo vyetu vingi, baadhi ya wakati mahitaji ya umeme katika vituo hivi yamekuwa yakiongezeka sana, hivyo pesa zinazopelekwa humalizika mapema zaidi kabla ya muda uliopangwa. Hali hii ikitokea wafanyakazi wa kituo hutakiwa kuwasiliana mapema na Afisa wa Afya Wilaya husika kwa kupatiwa fedha za ziada.

Aidha, kupitia mkakati wa ushirikishaji jamii katika huduma za afya, baadhi ya shehia na ngazi nyengine za uongozi katika maeneo hayo zimekuwa na utaratibu maalum wa kuchangia huduma kama umeme, ulinzi na huduma nyenginezo katika vituo vyao pale inapohitajika. Moyo huu hauna budi kupongezwa na kushajihishwa sana ili maeneo yote yawe na utaratibu huu. Hii itasaidia sana kuhakikisha ulinzi na upatikanaji wa uhakika wa huduma nyengine kama umeme zinapatikana. Ahsante Mhe. Mwenyekiti.

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub:** Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu ya Mhe. Naibu Waziri, Jimbo la Wete Mhe. Naibu Waziri ameanza kulijua yeye kabla ya mimi, na Jimbo la Paje nitaweza kulijua mimi mwanzo kabla ya yeye.

Mhe. Mwenyekiti, hii kadhia si ya muda mfupi labda kipindi hichi tu, miezi minne au mitano limetulia. Sasa kama wanapeleka pesa hakuna uaminifu sijui, hili limetokea kama miezi mitatu, minne. Kutokana na hali hiyo, ningemuomba Mhe. Waziri au Naibu Waziri wa Afya kabla ya kujibu swali hili kwanza wangefanya utafiti hasa kwa hivi vituo nilivyovitaja kwa ajili ya kupata ukweli

na uhalisia uliopo na baadae ndio kuja kujibu swali kwa usahihi na uhakika kwa sababu hivi vituo sikuchangia juzi wala jana...

**Mhe. Mwenyekiti:** Mhe. Jaku Hashim Ayoub naomba uulize swali.

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub:** Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, ni sababu gani za msingi hivi vitu vinaonekana kama mvua za masika zinakuja kwa miongo, maana yake mwaka hata mwaka. Ni sababu gani za msingi baadhi ya vituo hivi kukosa. Hata hivyo, hivi sasa jambo la kushukuru dawa zinapatikana lakini hapo nyuma nimebeba mzigo mkubwa sana wa madawa kwenye vituo hivi.

**Mhe. Naibu Waziri wa Afya:** Ahsante Mhe. Mwenyekiti. Mhe. Mwenyekiti kwanza napenda nimhakikishie Mhe. Jaku Hashim Ayoub kwamba wizara inaumwa sana na huduma za afya ambazo zinatolewa kwa wananchi wetu. Kwa hiyo, huduma hii ya umeme huwa tupo makini kweli kweli katika kipindi hiki chote na ninamuomba aondoshe kipindi cha nyuma, sasa katika kipindi hiki chote Mhe. Mwenyekiti, huduma ya umeme tunapeleka kama ipasavyo.

Katika taarifa zilizopo ni kwamba katika vituo vya Bwejuu, Kitogani na Jambiani zinaonesha kuwa katika kipindi chote cha hivi karibuni vimekuwa vikipata umeme bila ya matatizo kupitia fedha za *Basket Fund* na inapotokea kukosekana na sababu mbali mbali zilizotajwa hapo juu, basi wafanyakazi wa vituo vile wanawasiliana na Afisa wa Afya wa Wilaya, ili kupatiwa huduma hiyo haraka iwezekanavyo. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, nina wasiwasi wa kitu kimoja katika vituo hivyo naomba avifuatilie na angalie sana isijekuwa kuna

udanganyifu baina ya wafanyakazi na yeye kwa kutaka pengine asaidie katika kile kituo, inawezekana hilo jambo linajitokeza kwasababu wafanyakazi wetu ni binaadam na ubinaadam unajua una kasoro mbali mbali. Kwa hiyo, namuomba afuatilie kwa undani akigundua kama lipo tatizo ambapo kuna kituo katika vituo alivyovitaja au vyengine vyovyote hatupeleki pesa za umeme naomba awasiliane na sisi, ili tuweze kufuatilia tujue kuna tatizo gani. Lakini nataka nimhakikishie kwamba vituo vyote tunapeleka umeme ipasavyo. *(Makofi)*

**Mhe. Mohamed Said Mohamed:** Mhe. Mwenyekiti, nikushukuru sana kwa kuniona. Pamoja na majibu ya serikali yasiyokuwa na uhakika naomba kuuliza swali dogo sana la nyongeza. Kwa kuwa wizara inapitishiwa bajeti tena bajeti nzuri tu ya *OC* na wanapata kikamilifu asilimia 100, sasa vituo vingi vimeanza kujitokeza huduma ya umeme kukosekana kikiwemo kituo cha Mpendae. Je, ni mpango gani mkakati kibajeti unaweza kuwekwa ili huduma hiyo isikosekane katika hospitali hizo.

**Mhe. Naibu Waziri wa Afya:** Mhe. Mwenyekiti, naomba kumjibu Mhe. Mohamed Said Mohamed swali lake la nyongeza kama ifuatavyo.

Mhe. Mwenyekiti, wizara ina mpango maalum ambao umewekwa wa kufikisha huduma ya umeme katika vituo hivi kama nilivyosema awali. Katika kila kituo au vituo vyote vinaingiziwa shilingi 120,000 kwa vile vituo ambavyo vina huduma kubwa na vifaa vingi vya umeme, lakini vile vituo vidogo ambavyo havitoi huduma ya uzazi na mambo mengine vinaingiziwa kila mwezi shilingi 50,000. Mpango huu ni endelevu na tunaendea kuudumisha, ili kuhakikisha vituo vyetu vya afya havikosi huduma muhimu ya umeme kwa manufaa ya wananchi wa Zanzibar.

Ahsante Mhe. Mwenyekiti.

**Mhe. Hidaya Ali Makame:** Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipatia na mimi nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza lenye vifungu (a) na (b).

Mhe. Mwenyekiti, kwanza nimpongeze sana Mhe. Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri na ufasaha na ya kujiamini. Kwa kweli nampongeza sana Mhe. Naibu Waziri wa Afya maana yake anatuonesha moyo hasa wa kuona kweli wanawake tunaweza.

(a) Je, ni muda gani zimeanza kutolewa hizo fedha za vituo alizoziita ni shilingi 120,000 kutokana na kwamba taarifa zilizopo vituo hivi vinapewa shilingi 50,000 kwa kila mwezi.

(b) Kama Wizara ya Afya ina mpango gani kushirikiana na *ZECO* kuhusu hili suala la umeme kwenye vituo, kuhakikisha kwamba vituo hivi havikatiwi umeme isipokuwa kwa dharura zinazotokana na ukarabati wao wenyewe wa kuzima umeme huu kwa ghafla tu au kwa mara moja. Hivyo, ni taratibu gani ambazo wataziandaa kushirikiana na kujua kwamba vituo hivi muda wote vina umeme na unafanya kazi. Ahsante Mhe. Mwenyekiti.

**Mhe. Naibu Waziri wa Afya:** Ahsante Mhe. Mwenyekiti, naomba nimjibu Mhe. Hidaya Ali Makame swali lake la nyongeza kama ifuatavyo.

Mhe. Mwenyekiti, hii huduma ilikuwa ikisuasua kidogo kama nivyotaja mwanzo katika kipindi cha nyuma, lakini baada ya kuingiziwa bajeti ya mwaka uliopita na huduma nyengine zikaanza kwenda kama kawaida, basi na huduma tayari ilianza kwenda kama kawaida haikusita na mpaka leo. Kwa hiyo, natoa

tena wito maana inaonekana kama kwamba baadhi ya vituo vina tatizo hili kwa mujibu wa maelezo ya Waheshimiwa Wawakilishi nahisi kama kuna wasi wasi. Kutokana na hali hiyo, naomba wafuatilie kwa kina vituo vyenu vilivyomo katika majimbo na kama kuna kasoro yoyote ya upatikanaji wa umeme naomba watujulishe, ili tuweze kufuatilia wapi kuna tatizo.

Mhe. Mwenyekiti, hizi pesa zinazotolewa, hizi ni pesa na pesa zina bilisi na huduma ni muhimu kupatikana kwa wananchi wote. Naomba wafuatilie kama watakuta tatizo lolote basi watujulishe ili tuweze kufuatilia, inawezekana kutakuwa kuna tatizo baina ya wanaopokea hizi pesa na huduma zinavyotolewa.

Lakini tuna mpango gani kushauriana na *ZECO*. Mhe. Mwenyekiti, *ZECO* ni shirika ambalo lipo kwenye wizara tofauti na Wizara ya Afya. Hili naomba nilichukue kama shauri tuangalie kama kuna haja ya kuona kwamba sisi tunashindwa kulipia, basi tushauriane na wao ili watusaidie. Lakini naona huduma hii inakwenda vizuri na kwa jinsi bajeti yetu walivyoipitisha juzi sifikirii kama itakwama popote.

**Mhe. Mwenyekiti:** Mhe. Waziri wa Afya kwa majibu ya ziada.

**Mhe. Waziri wa Afya:** Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii, pamoja na majibu mazuri sana ya Mhe. Naibu Waziri ambaye amekuwa akifuatilia vituo hivi na kadhia hii na mimi nikishirikiana nae kwa karibu sana.

Hivi karibuni kama tutakumbuka katika *hansard* Mhe. Jaku Hashim Ayoub alikuja na orodha ya kusema wizara zinazodaiwa na Shirika la Umeme moja wapo ilikuwa ni Wizara ya Afya na alitaja kile kiwango ambacho ni kikubwa. Kutokana na hali hiyo, mimi mwenyewe katika kufuatilia baadhi ya vituo zile pesa

wanazolipa za umeme huwa wanakatwa yale madeni yaliyokuwa ya nyuma, yale madeni ambayo walikuwa wanadaiwa kabla, basi pesa zikiingizwa hata waheshimiwa wanaochangia pia zikiingizwa wanakuta zile pesa zinakatwa.

Tunawashukuru sana ndugu zetu Wizara ya Fedha na Mipango akiwemo Mhe. Waziri wa Fedha pamoja na watendaji wake, hivi sasa tupo katika mazungumzo ya kusaidiana kutokana na bajeti yetu baadhi ya bili za umeme zote za vituo hivi za nyuma zilizokuwa zikidaiwa, ili tukiingiza katika zile mita za TUKUZA hivi sasa tusikatwe. Kwa sababu ukiwa unadaiwa deni la nyuma hata uingize ngapi sasa hivi zote zinapigwa pande katika lile deni lilopita.

Kwa hivyo Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu hayo ya Mhe. Naibu Waziri wa Afya naamini hivi karibuni hali yetu itakaa sawa, mbali hiyo *Basket Fund* ambayo inaendelea kutolewa na hiyo kasma inayotolewa kwa ajili ya umeme na vituo vinavyozalisha vinapewa *priority* kubwa zaidi kwa sababu ya kupunguza vifo vya mama na watoto. Mhe. Mwenyekiti, tukiangalia ukurasa wa 98 wa *budget speech* yangu utaona wale *donors* wote ambao wanatoa fedha katika eneo hilo ikiwemo fedha za umeme. Hali hii itakaa sawa hivi karibuni kwa vituo vichache ambavyo vilikuwa na madeni ya nyuma. Ahsante Mhe. Mwenyekiti. *(Makofi)*

**Nam 181**

**Ubora wa Viwango vya Ujenzi wa Barabara**

**Mhe. Ali Suleiman Ali (Kny. Mhe. Jaku Hashim Ayoub) -** Aliuliza:

Kumekuwa na changamoto kubwa ya barabara zetu kuchimbika na kufanya mashimo katika vipindi vya mvua na mara kadhaa maeneo yanayokumbwa na mashimo yanakuwa hayo kwa hayo. Licha ya juhudi za kuyaziba lakini hali hiyo hujitokeza tena kila kipindi cha mvua kazi inakuwa ni hiyo hiyo.

Je, tatizo hili la kuchimbika barabara zetu kila kipindi cha mvua lisababishwa na kiwango kidogo cha ujenzi au nyenzo duni.

**Mhe. Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji** – Alijibu:

Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 181 kama ifuatavyo:-

Mhe. Mwenyekiti, ni kweli kuna changamoto kubwa kwenye barabara zetu zilizojengwa kwa lami na kifusi wakati wa vipindi vya mvua ambapo kuna maeneo kadhaa hujitokeza mashimo mara kwa mara pamoja na juhudi zinazochukuliwa za kuyaziba.

Mhe. Mwenyekiti, kujirudia kwa mashimo hayo mara kwa mara haitokani na kiwango kidogo cha ujenzi bali inatokana na sababu zifuatazo:-

(a) Barabara kuwa chini kuliko ardhi na barabara huwa mara nyingi inajengwa chini ya ardhi na hili ni jambo ambalo hupelekea kutuama maji kwa muda mrefu hata pale mvua zinaposita kunyesha;

(b) Kujaa kwa mchanga ambao unaochukuliwa na maji kutoka kwenye njia zinazoingia mitaani na kutuama kwenye maeneo hayo kwa muda mrefu ambapo hupelekea lami kuoza na baadaye kujitokeza kwa mashimo;

(c) Kufukiwa kwa mitaro na njia za asili ya maji kutokana na ujenzi holela pamoja na uvamizi wa maeneo ya hifadhi ya barabara;

(d) Baadhi ya wananchi kumwaga au kutiririsha barabarani maji machafu kutoka kwenye majumba yao, kukoshea gari pamoja na maji ya mafuta ya kukaangia chipsi na kadhalika. Maji hayo machafu yanakwenda kuharibu barabara zetu.

Mhe. Mwenyekiti, baadhi ya maeneo sugu ni Sharifumsa, Mtoni barabara ya kwenda Kidatu, Kiwanda cha Soda na Saateni kwenye tangi la maji.

Pamoja na juhudi zinazochukuliwa na wizara yetu kupitia Idara ya Ujenzi na Utunzaji wa Barabara za kuyaziba mashimo hayo mara kwa mara, uongozi wa idara pia umekuwa ukichukua juhudi kwa kuwapelekea barua za wito Masheha na wenye nyumba ambazo zinatiririsha maji barabarani, lakini juhudi hizo zimekuwa zikigonga mwamba kwa vile wahusika huwa hawaji au hawajali.
Mhe. Mwenyekiti, napenda kuchukua fursa hii kuwataka wananchi wenye nyumba zao ambazo maji ya kukoshea vyombo yameelekezwa barabarani hasa Saateni kwenye tangi la maji, wanaokosha magari, wafanyabiashara wa mikahawa, wauza chipsi wote hao waache kumwaga maji barabarani kwa vile maji hayo yameambatana na mafuta pamoja na *chemicals* ambazo hupelekea lami kuharibika na kusababisha kujitokeza mashimo ya mara kwa mara kwenye maeneo hayo.

Aidha, Masheha nao watoe ushirikiano wa karibu na Idara ya Ujenzi na Utunzaji wa Barabara kwa kuzuia watu wanaoharibu barabara kwa makusudi, kwani ujenzi wa barabara unagharimu fedha nyingi. Hivyo, ni wajibu wa kila mwananchi kuzitunza

barabara hizo kwa faida yake na kwa faida ya nchi kwa jumla. Ahsante Mhe. Mwenyekiti.

**Mhe. Ali Suleiman Ali:** Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri kwa ruhusa yako naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Kwanza, nimpongeze Mhe. Waziri kwa taaluma yake nzuri na majibu yake mazuri ya ufasaha kabisa ambapo katulia kila mtu karidhika na alivyoyapata.

Lakini Mhe. Mwenyekiti, swali langu liko hapa. Kwa kuzingatia barabara zetu mara nyingi siku za mvua za masika lazima tuzibe viraka kwa hali ya juu na kuna maeneo maalum. Kwa mfano, Mwanakwerekwe *round about*, Amani *round about* na kwengineko.

Kwa maana hiyo, zinapojengwa barabara zetu tunao wataalam wetu wa kiwango cha kuhakikisha kwamba kiwango hiki kinaridhisha, hiki hakiridhishi na hasa tukizingatia sasa hivi tunayo magari mengi makubwa ambayo yamepindukia uwezo wa barabara zetu. Hivyo, wizara kwa makusudi inalionaje hili wakati wa kujenga barabara zetu kiwango kinachostahiki kiwekwe na kiangaliwe na ikiwa hakikufikia barabara hiyo tusiiruhusu kuichukua. Je, Mhe. Waziri atachukua hatua gani pindi likitokea kama hilo.

**Mhe. Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji:** Mhe. Mwenyekiti, napenda kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza kama ifuatavyo.

Tumeangalia viwango ambavyo vilitumika katika kujengea njia hizi ambazo tunazo, na tumegundua kwamba njia nyingi ambazo tunazitumia hapa zimejengwa zamani sana, na zilijengwa kwa viwango vya wakati huo. Kwa wale waliokuwa na umri kama

mimi au kunizidi watakumbuka kwamba zamani njia hapa zilikuwa zinajengwa kwa majembe, pauro na sururu, kwa wakati huo ilikuwa viwango vinatimizwa. Kwa kweli, njia zile tumezirithi kwa wakoloni na baada ya Mapinduzi tulikuwa tunajenga njia mpya bila ya kurekebisha zile njia za zamani.

Kwa hivi sasa Mhe. Mwenyekiti, nataka nilihakikishie Baraza lako tukufu kwamba tunao mkakati kiwizara kwenda kuangalia namna ya kuzitengeneza hizi njia na kwa baadhi ya njia itabidi tuzifumue na kuzijenga upya. Mfano alioutumia Mhe. Mwakilishi kwamba kuna njia inatusumbua sana ya kutoka Mwanakwerekwe mpaka kwenye bonde kubwa pale wenyewe wanaita Kibondemzungu tumeshafanya mpango wa kutafuta fedha ili tuzijenge tena upya, tufumue pale kwenye bonde mita 300 ile njia imejengwa iko chini inafuata bonde.

Kwa hivyo, itabidi sasa ile njia tuinyanyue maana yake ni nini, tutakwenda na *engineers* pale wakajenge, wakatie *culverts* halafu hii njia inyanyuliwe, ili zikija tena mvua maji yapite chini yaende zake baharini. Kwa hivyo, matatizo haya tunayafahamu na tutaendelea kuyafanyia kazi.

Mhe. Mwenyekiti, kwenye suala la udhibiti wa matumizi ya njia hasa magari makubwa kutumia njia zetu hizi hilo linafanyiwa kazi, tunategemea kwenda kupima njia zetu zote hizi halafu baadaye tuweke *signs* zile za njia za kuonesha kwamba maeneo fulani hakuna ruhusa ya gari yoyote iliyokuwa zaidi ya kupindukia tani fulani. Kwa mfano, tani tano kupita huko na tutashirikiana na ndugu zetu wa Jeshi la Polisi kuhakikisha kwamba sheria hizo za matumizi ya barabara zinafuatwa. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti. *(Makofi)*

**Mhe. Panya Ali Abdalla:** Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, nashukuru na mimi kunipatia nafasi hii niulize swali la nyongeza lenye (a) na (b).

Mhe. Mwenyekiti, kwanza nichukue fursa hii kuipongeza sana serikali kwa juhudi kubwa ya ujenzi wa barabara hasa nikielekeza kwenye barabara ya Fuoni ambayo inaonekana imejengwa vizuri kwa kujengewa msingi ambapo maji yanapita pembezoni.

(a) Je, ni lini serikali itajenga misingi pembezoni mwa barabara zetu, ili kuzifanya barabara hizo kuwa madhubuti na haziathiriwi na maji na si kama ilivyo hivi sasa barabara nyingi zimeshaathirika kwa kukosa kujengewa misingi na hatimae zinaathiriwa na maji.

(b) Kwa kuwa mvua kubwa zilizonyesha zimeharibu sana miundombinu yetu ya barabara na kuweka barabara zetu kuwa na mashimo makubwa. Je, ni lini serikali itakwenda kuziba yale mashimo makubwa kabisa ambayo yanaonekana kwa hivi sasa yanaweza kuleta athari ya ajali. Ni lini serikali itazingatia kwenda kuziba angalau yale maeneo yaliyojitokeza mashimo makubwa, ili kuweza kunusuru kusije kukatokea ajali. Ahsante.

**Mhe. Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji:** Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako nijibu kwanza swali (b).

Kwa kweli, tumeshakaa kiwizara na tumeshakubaliana tukatafute fedha ambazo Waziri wa Fedha na Mipango ametuahidi zinaweza zikapatikana, kazi hiyo ya kurekebisha miundombinu yetu ambayo imepata matatizo itaanza mara moja. Kwa hivyo, tutegemee kwamba tutaanza kazi hiyo kuifanya kwa upande wa Pemba tunacho kitengo chetu kule tayari tumeshatoa maagizo waanze kufanya hiyo kazi, fedha tunazo kidogo za kuanzia.

Kwa upande wa Unguja tunaanza kutafuta hizo fedha tukishazipata tu tunaanza kazi hiyo ya kwenda kuziba mashimo yaliyojitokeza pia kurekebisha miundombinu, na tukizingatia kwamba nimekwenda kutembelea njia nyingi nimekuta tatizo kubwa tulilolipata ni madaraja hayakuvunjika lakini pale panapo kiungo baina ya mwisho wa daraja na mwanzo wa njia walikuwa hawakujenga vizuri tunavyotaka maji yalipokuja kwa wingi sana yalivamia maeneo hayo na ikawa michimbuko mingi katika maeneo kama hayo, lakini tumehakikishiwa kwamba kazi ya kurekebisha hilo linawezekana. Kwa hivyo, jibu langu ni kwamba kazi hiyo itaanza mara moja.
Mhe. Mwenyekiti, swali la misingi nataka tu nijibu swali hili kusema kwamba tunapokuwa tunajenga njia nitumie mfano aliotumia Mhe. Mwakilishi kwa njia ya Mwanakwerekwe kwenda Fuoni. Mhe. Mwenyekiti, tulipokuwa tunaijenga upya njia hii tulikaa kitako tukaangalia viwango ambavyo tunavihitaji, lakini pia tuliangalia gharama za kuijenga ile njia.

Mhe. Mwenyekiti, lazima nikiri kwenye Baraza lako tukufu kwamba pengine tulikosea tukaona ili kupunguza matumizi na tupate njia ya urefu zaidi, tuliona kwamba misingi au mitaro ya maji tuitie katika maeneo yale tu ambayo tulikuwa tunayafikiria yanaweza yakatuletea matatizo baada ya mvua za masika. Tukatia misingi hiyo huko lakini imekuja kudhihirika kwamba kuna maeneo mengine ambayo tulihisi kuwa tuta la njia liko juu, lakini na huko pia bahati mbaya kwa kuwa mvua hizi zimenyesha hivi karibuni zilikuwa ni nyingi sana zimeharibu maeneo hayo.

Kwa hivyo, tutarudi tena tukaangalie tena ile *Master Plan* ya mwanzo ya kujenga njia ile, nimeambiwa kwamba ilikuwa tuongeze matumizi ya bilioni 1,100,000,000 kwa ajili ya kujenga hiyo mitaro na misingi ya ziada tutakwenda kutafuta hizo fedha,

ili tuijenge misingi hiyo na mitaro hiyo kuhakikisha kwamba zitapokuja mvua nyengine za masika mwakani hatutopata matatizo ambayo tumeyapata mwaka huu. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.

**Nam. 120**

**Ukarabati wa Jengo la *Beit-el-Ajaib***

**Mhe. Ali Suleiman Ali (Kny: Mhe. Omar Seif Abeid) –** Aliuliza:-

Kwa kuwa kwenye hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Ardhi ya mwaka 2016/2017 wizara ilielezea Baraza kwamba, ukarabati wa *Beit-el-Ajaib* umeanza kwa kukamilisha utayarishwaji wa ramani (*existing drawing*) pamoja na *proposed drawing* kwa kushirikiana na Mamlaka ya Uhifadhi wa Mji Mkongwe na Serikali ya Oman kupitia Wizara ya Urithi na Utamaduni ya Oman ilituma barua ya kuomba kulifanyia matengenezo makubwa jengo hilo.

(a) Je, kazi ya matengenezo ya jengo hilo imeshaanza, na kama haijaanza ni lini inategemewa kuanza.

(b) Je, Serikali ya SMZ imetumia kiasi gani cha fedha kwa ajili ya kazi za awali kwa kukamilisha *existing drawing* pamoja na *proposed drawing*.

(c) Je, gharama halisi ya kazi hiyo ni kiasi gani na nani atakayefadhili fedha kwa ajili ya ujenzi wa jengo hilo la kihistoria.

**Mhe. Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji** – Alijibu:-

Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 120 lenye vipengele (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Mwenyekiti, kazi ya matengenezo ya jengo hilo la *Beit-el-Ajaib* bado haijaanza kwa vile ilikuwa inasubiri jibu la nyaraka (ramani na ripoti) iliyopelekwa *UNESCO*, tulikuwa tunasubiri majibu kutoka huko na majibu ambayo kwa hivi sasa tumepata kibali na katika majibu haya tumeruhusiwa sasa kwamba kazi ya ukarabati inaweza kuanza wakati wowote.

(b) Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imetumia shilingi milioni sitini (60,000,000/=) kwa kazi ya kulihami jengo hilo ili lisianguke, na katika yale maeneo yaliyoporomoka kwa ajili ya kuzuia mporomoko usiendelee na kuzuia hali ile isiendelee kwa kipindi hadi ukarabati utakapoanza. Hakuna malipo yoyote kwa ajili ya ukamilishaji wa *existing drawing* na *proposal drawing*, kazi hizo zimefanywa na wataalam wetu wa mamlaka.

Utayarishaji wa ripoti kubwa ya kitaalamu inayoelezea kazi yote inavyotakiwa kufanywa, ukubwa wa kazi, utayarishwaji wa nyaraka za kazi, mamlaka ilishirikiana na mtaalam maarufu wa ukarabati wa majengo makongwe Antony Steel na kuwasilishwa nyaraka hizo ambazo zimetengenezwa kwa msaada wa Antony Steel kupelekwa huko *UNESCO/ICOMOS* na kupata ridhaa ya kuanza kazi. Mtaalam huyo alilipwa dola za Kimarekani 6,110.

Gharama halisi ya kazi hiyo itajulikana pale ambapo mfadhili ataleta gharama halisi. Tunategemea mfadhili atakuwa ni Ufalme wa Oman itakapopatikana gharama halisi tutakapokuwa tayari na

pia hapo ndio tutaanza kazi hiyo na kujua nani hasa atakayeifanya hiyo kazi. Ahsante Mhe. Mwenyekiti.

**Mhe. Ali Suleiman Ali:** Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji kwa ruhusa yako naomba kuuliza swali la nyongeza.

Mhe. Mwenyekiti, pia nimpongeze Mhe. Waziri kwa kufuatilia uendelezaji wa jengo letu hili la historia na tunalitegemea sana kuingiza fedha mbali mbali za kigeni kwa ajili ya maendeleo ya nchi yetu. Swali langu liko hapa. Katika majibu Mhe. Waziri ametwambia kwamba wametumia milioni sitini kulihami jengo hilo.

(a) Je, milioni sitini hizo zimetumika kwa kitu gani ili kulihami jengo hilo.

(b) Kwa kuwa, jengo hilo linaendelea kuleta athari kubwa na limefungwa kwa watalii wasitumie jengo lile kwa usalama wao na usalama wanaotembeleza watalii katika jengo lile. Lakini kwa makusudi wafanyakazi baadhi yao huwaingiza watalii katika jengo lile kwa siri. Je, wizara hili inalijua na itachukua hatua gani pindi wakiligundua.

**Mhe. Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji:** Mhe. Mwenyekiti, nataka kumjibu swali lake Mhe. Mwakilishi ningependa kusema tu kwamba katika shughuli ambazo tunazifanya huko katika jengo hili kuna wizara zaidi ya wizara yangu ambayo inashughulika na jengo. Swali lake Mhe. Mjumbe lingejibiwa vizuri na wizara inayohusika ambapo ni Wizara ya Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo.
Lakini mimi kwa upande wangu ningependa tu kumjibu kwamba kwa upande wa wizara yetu tunaposimamia uhifadhi wa majengo

haya makongwe, hili ni jengo la *category* 'A' ambalo ni jengo tunategemea kwamba litakuwa vile vile lilivyo, hata likishatengenezwa tunataka tulitengeneze liwe vile vile na haiba yake iwe ya kuvutia na nimeambiwa kwamba watalii wengi wanakuja hapa Zanzibar wa nchi za nje kuja kuliangalia jengo lile. Kwa hivyo, sisi wajibu wetu ni kulihifadhi kuhakikisha kwamba halianguki ili kutafuta fedha kama nilivyosema pale awali kama tutalitengeneza.

Swali la watalii kuingia ndani kwenda kuliangalia lile jengo hili limetokana na agizo la mamlaka kwa sababu mamlaka nao wamesimama hifadhi ya majengo haya wana haki na wana uwezo kisheria kuweza kwenda kuangalia lile jengo na wakahisi kwamba ikiwa watu wanaendelea kuishi hapo au wanaendelea kuingia na kutoka itahatarisha miundombinu ya jengo hilo, basi huwa wanapewa agizo kwamba shughuli hizo zisifanyike.

Lakini pengine watalii hawaendi tena hapo kutokana na agizo hilo. Lakini kama nilivyosema awali wizara husika inaweza ikakupatia jibu kamilifu. Ahsante Mhe. Mwenyekiti.

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wzara ya Fedha na Mipango kwa mwaka wa Fedha 2017/18

*(Majadiliano yanaendelea)*

**Mhe. Mwenyekiti:** Waheshimiwa Wajumbe, majadiliano yanaendelea. Lakini kabla ya kumwita mchangiaji wetu wa kwanza kuna tangazo kuwa Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti ameomba Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati hiyo baada tu ya muda wa maswali na majibu wakutane ukumbi namba mbili.

Sasa naomba nimwite Mhe. Simai Mohammed Said na atafuatiwa na Mhe. Hassan Khamis Hafidh na Mhe. Hidaya Ali Makame ajitayarishe.

**Mhe. Simai Mohammed Said:** Ahsante Mwenyekiti, nianze kukushukuru kwa kunipa nafasi kuwa mchangiaji wa mwanzo asubuhi yetu ya leo. Lakini pia nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu na pia kuwashukuru wananchi wangu wa Jimbo la Tunguu kwa kuweza kufika hapa na kuweza kutoa mawazo yangu, fikra zangu na kuishauri serikali kwa kadri ninavyoamini.

Mhe. Mwenyekiti, wakati tunaelekea kuhitimisha bajeti yetu ya mwaka 2017/2018 hatuna budi kuhakikisha kwamba wizara hii ni katika wizara muhimu juu ya mambo yote ambayo wizara zetu zote nyengine watakuwa wao wanazisimamia kwa ukamilifu. Lakini hasa katika masuala ya fedha ambazo ndiyo inaelekea kutumika katika mambo tofauti ya usimamizi wa serikali, uendeshaji pamoja na kuleta maendeleo kwa wananchi wetu.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya maelezo mfupi sasa nianze kwa kumpongeza Mhe. Waziri kwa kweli huyu ni mtaalam amesoma kwa umakini kabisa sauti yake unamsikia, lakini pia mbwembwe zake unakuwa huzioni anapokuwa anasoma kwa sababu ni waziri wa aina ya kipekee anachokisema anajiamini, anachokileta tunakifahamu na anapozungumza anakuwa anakuangalia wewe nyuma kwa uwakilishi kujaribu kuhakikisha kwamba umempata na ile taarifa imekufikia.

Kwa hiyo, nimpongeze sana Mhe. Waziri na wengine ni vizuri pia wakamuiga aina za mbwembwe ambazo yeye anakuwa

anazitumia hapa, lakini ambazo zimejificha zina mahaba ya kutupendezesha kwetu sisi. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hapo sasa naomba niende moja kwa moja kwenye hoja. Mhe. Mwenyekiti, kwanza niipongeze serikali kwa jumla ya bajeti hii katika makusanyo lakini ukiangalia katika kodi mwaka huu walizozipanga ni bilioni mia nne na arubaini saba na katika Washirika wa Maendeleo ukiangalia bilioni mia tatu ishirini na sita.

Kwa kweli hili ni jambo kubwa kwa sababu ukiangalia mwaka 2016/17 *target* ya Washirika wa Maendeleo ilikuwa ni bilioni hamsini na nane nukta sita. Naamini mwaka huu kutokana na umakini na utetezi kuna ongezeko kubwa kuhakikisha kwamba sasa tutapata bilioni mia tatu na ishirini na sita hili jambo zuri. Lakini pia ukienda katika deni la taifa mwaka 2016 Julai deni lilikuwa lipo kwenye bilioni mia tatu na tisini na nane, lakini mwaka huu tumeona hasa kwamba serikali imeanza kupunguza deni na kulipa na sasa lipo bilioni mia tatu na sabini na saba.

Hivyo, malipo aliyoyafanya bilioni ishirini an moja nukta tatu ni jambo la kujipongeza na naipongeza sana serikali wazidi kuendelea kila mwaka kuhakikisha kwamba deni la taifa linabaki katika mazingira ambayo halitotatanisha na kuleta mapungufu yoyote katika bei yake ya serikali.

Lakini kwenye suala la *MKUZA III*. Mhe. Mwenyekiti, kwenye *MKUZA* ukiangalia kwenye kipato ambacho Mzanzibari ukisoma katika ile *average* ambayo *target* serikali wameipanga ni vizuri wakai-*review* pia inawezekana tumeshaipita, inawezekana tumeikaribia kwa sababu tofauti ya shilingi na dola ipo imekuwa inabadilika. Ukiangalia miaka kumi nyuma dola ilikuwa kwa shilingi mia nane, lakini leo tupo katika shilingi elfu mbili mia

mbili na elfu mbili mia moja mpaka elfu mbili. Kwa hiyo, inawezekana sana katika ile *target* ambayo umeweka kwenye *MKUZA III* basi wai-*review* na mambo mengi mdogo madogo ili waweze kupata takwimu sahihi.

Mhe. Mwenyekiti, naomba sasa niende katika vipaumbele lakini kwenye eneo moja ambalo limenigusa la wananchi wangu nataka nimpongeze waziri kwa jambo kubwa sana hasa kuhusiana na barabara ya Unguja Ukuu kwenda zake mpaka Uzi Ng'ambwa. Kwa mara ya kwanza ukisoma kwenye bajeti hii kisiwa cha Uzi watu mara nyingi kutokana na mazingira yao yapo sawa sawa na Tumbatu hupatikana Mshauri Mwelekezi na kwamba sasa barabara itakuwa katika harakati kuanza kujengwa rasmi.

Vile vile nimpongeze sana Mhe. Waziri na nimuahidi atakapokuja Mshauri Mwelekezi basi nitakuwa tayari kukaa nae kumualika chakula cha mchana au cha usiku pamoja na Mhe. Waziri popote anapotaka twende pamoja, ili na mimi pia niweze kutoa mawazo yangu na wananchi wa Jimbo la Tunguu hasa kwa wananchi hawa wa visiwa hivi ambao wana ndugu na jamaa katika maeneo mbali mbali ya Unguja pamoja na Pemba watakuwa sasa wanaweza kuvuka kwa magari ya moto pamoja na pikipiki, vespa kutoka Uzi kuja zao mpaka Unguja Ukuu na kuja mjini.

Kwa hiyo, Mhe. Waziri hongera sana na Mwenyezi Mungu akijaalia utaweza kufanikisha hili na wananchi wa Jimbo la Tunguu hasa wa Unguja Ukuu, Uzi pamoja na Ng'ambwa watakushukuru sana.

Mhe. Mwenyekiti, nikienda kwenye ukurasa wa 24 suala la *ZIPA*. Mhe. Mwenyekiti, ukisoma katika ukurasa wa 4 kifungu namba 3 naomba ninukuu. Moja ya malengo ambayo *ZIPA* wamejiwekea ni:-

"Kuhamasisha uwezekaji kupitia Maonesho ya Biashara ndani ya Zanzibar na Afrika ya Kusini na kuandaa Mkutano wa Wawekezaji kwa lengo la kufanikisha wawekezaji nchini." Mwisho wa kunukuu.

Mhe. Mwenyekiti, naomba sana japokuwa nina masahihisho au mambo ambayo *ZIPA* tayari wamejitengenezea, ili kuhakikisha kwamba vitega uchumi na mambo ya maendeleo kuhakikisha kwamba mapato yetu na uwekezaji tunaongeza. Kwa hivyo, nimuombe Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Mwenyekiti, kwamba juhudi zifanyike za ziada kuhakikisha ukaribu wa ndani wa uwekezaji wa ndani pamoja na uwepo unaokuja, ili na sisi pia tuingie katika suala la Soko la Ushindani la Afrika Mashariki.

Lakini pia ningemuomba sana katika vipaumbele ambavyo ataviweka ndani ya Taasisi yetu ya *ZIPA* naomba watumie neno ambalo ni *realistic*, vitu ambavyo tutakuwa tunaweza kuvifanya. Ningeomba sana katika suala hili waunganishe nguvu pamoja na Wizara ya Mhe. Haji Omar Kheri, Tawala za Mikoa kwa sababu pale tuna nafasi nzuri sana ya watu ambao wapiganaji wetu, yaani tunaposema tuna *human resource*. Tuna watu wengi pia bado hatuwatumii ipasavyo.

Kwa hiyo, kama kutakuwa na *joint venture* na makampuni mengi kutoka kama nilivyosema katika mchango wangu wa awali Cambodia, waanze kuzipanga hizi fursa katika masuala ya kutengeneza kwa mfano *furniture* na mambo mengine ambavyo vitasaidia katika *domestic consumption*. Kutokana na hali hiyo, tusiangalie wawekezaji kutoka nje, lakini tuangalie sisi katika uwezo wetu tunawezaje kuunganisha nguvu zetu, ili tuweze kupunguza masuala ya *importation* na ku-*relay* katika mambo

mengi ya *importation* kutoka hapa Zanzibar. Sasa hayo ndio naamini yataweza kutusaidia.

Mhe. Mwenyekiti, sasa nataka nigusie kidogo suala la *ZSFF*. Mhe. Mwenyekiti, *ZSFF* wanakwenda vizuri wamefanya miradi mizuri kama Kariakoo kwa watoto wetu Unguja pamoja na Pemba, tumeona pale sasa hivi Michenzani pia panaanza kutumika vizuri pamoja na nyumba za ghorofa pale Michezani na sisi hapa tutaanza kujigamba tukienda kule Tanzania Bara kwa marafiki zetu, tutakuwa na uwezo wa kuwaambia na sisi pia jinsi gani taasisi zao na sisi tunaweza kuingia.

Lakini ningeomba Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri atumie bidii ya ziada kuhakikisha kwamba *ZSFF* nao wanaingia kwa nguvu katika soko la Tanzania Bara, watumie wigo na kuiga kama wenzao Zanzibar *Insurance Corporation* pamoja na *PBZ*. Lakini wanapokwenda pia wanapokuwa kule Tanzania Bara wataona soko ni kubwa pia wazingatie kuunganisha nguvu zao, kwa mfano ikiwa *ZSFF* wataamua kujenga ghorofa mahala ambapo anahisi ataweza kupata kodi nzuri au anahisi mwenzake anataweza kufaidika, basi awaze kuangalia kwamba *PBZ* kama wanaweza kufungua tawi la benki.

Kwa maana hiyo, ni vyema waunganishe nguvu na wawe na *ideas* za *visionary* kuangalia baada ya miaka 20 maeneo watakapokaa, ili maslahi yaende vizuri kwa upande wao pia, lakini mapato yao pia yaongezeke na wanapokuja hapa tuwe tunapata ripoti na mambo mazuri ya kwao.

Lakini pia nataka nizungumze suala la *PBZ*. Mhe. Mwenyekiti, *PBZ* wanakwenda vizuri lakini wakati tunatoka katika Benki ya Watu wa Zanzibar ningeomba sana *PBZ* pamoja na *Zanzibar Insurance Corporation* ikiwezekana *logo* yao ya benki imepitwa

na muda, sasa hivi duniani kuna ushindani na kuna njia za kutumia za *new media* kuwavutia wateja tofauti. Waangalie kama wanaweza ku-*review branding* ya kwa umoja ya *PBZ* pamoja na *Zanzibar Insurance Corporation* kwa ujumla kwa jinsi gani wanavyotaka waonekane. Kwa mfano, kampuni ya simu ya *Zantel* ile *Z* ukiangalia kwa kule unaona kama ile ni *Zantel*, lakini gharama ya ile *logo* ukija kusikia kutengeneza ni pesa nyingi sana.

Sasa watafute kitu ambacho ukikiona kutoka mita mia mbili kwenye *board*, basi unaweza kujua kwamba ile ni *Peoples' Bank of Zanzibar* na ile pale ni *Zanzibar Insurance Corporation*. Lakini ukiangalia katika *PBZ* bado katika utoaji wa huduma ningependa wakazane zaidi lakini yaanze kutoka mavazi yao. Unajua mavazi Mhe. Mwenyekiti, pia yana mvuto wake kwa hivyo wa-*review uniform* zao, lakini pia katika utoaji huduma.

Kwa mfano, Zanzibar ni nchi ya Kiislamu pamoja na watu wake pia na wanapokuja wakati wa sala za Ijumaa na sisi tuna-*deal* na utalii unakwenda wakati mwengine mabenki unakuta wafanyakazi wanakuwa wanazongwa na wengine hawapo kwa ajili ya ibada. Sasa wakati mwengine katika utoaji wa huduma utafutwe utaratibu wa kutafuta watu ambao pengine wao hawatakazwa na ule muda wa ibada, ili na wao pia waweze kubaki pale na ile huduma iendelee. Kwa sababu ibada ya Ijumaa wengine wanaanza kutoka saa sita mpaka saba na nusu, lakini pia Ijumaa ni mwisho wa wiki kwa mujibu wa siku za kazi.

Sasa wengine wanapokuja mjini hasa wawekezaji kutoka mashamba wanafuata huduma hii unakuta wakati ule wanakosa ile huduma. Kwa hiyo, huduma iendelee na kuhakikisha wateja wote wanakwenda katika mabenki wanapata ile huduma. Lakini pia na mvuto kama nilivyosema uzidi.

Nikiendelea na mchango wangu naomba nizungumzie suala la *Zanzibar Insurance Corporation.* Mhe. Mwenyekiti, nimeangalia katika historia ya kampuni hii na jinsi walivyoingia kwa kasi kwa upande Bara. Mhe. Mwenyekiti, naomba sana Mhe. Waziri apokee pongezi zangu kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Tunguu kuipongeza kwa dhati kabisa *Zanzibar Insurance Corporation* kwa bidii wanavyokwenda nazo kwa jinsi gani matawi yao yameimarika.

Hivi sasa kwa takwimu ukiziangalia wanapata au wanapokea mapato yao zaidi katika Mikoa ya Tanzania Bara kuliko Zanzibar, wana wateja wengi wazidi kuimarika. Naomba sana wazidi kujitangaza kwa kutumia mabango ya barabarani na sisi Wazanzibari tutakapopita Tanzania Bara tutakapotembea mikoani tuone kampuni zetu zinaonekana njiani na sisi tujisikie. Lakini katika kujisikia hivyo sio yawekwe mabango kwa kutumia fedha bure lakini pia wa kujitangaza, tunapita pahala na sisi pia tunakuwa tunakumbushwa kuwa mabalozi wazuri kwa ajili ya taasisi hizi. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, sasa naomba niende kwenye suala la *ZRB*. Mhe. Mwenyekiti, *Zanzibar Revenue Board* ni taasisi moja muhimu, ni taasisi mama kwa upande wa wizara hii kwa sababu mapato yote yanakwenda hapa. Niwapongeze kwa jinsi walivyobadilika, hapo kale tunasema zamani *Zanzibar Revenue Board* mtu ulikuwa unaweza kuona maadui hasa wafanyakazi wao jinsi *approach* walivyokuwa wanakwenda kuwaona wawekezaji pamoja na wafanyabiashara wazalendo mbali mbali wa ndani.

Lakini ukiangalia leo *Zanzibar Revenue Board* unapoingia kwenye ofisi yao ni katika ofisi moja Zanzibar ambayo wanatakiwa taasisi nyengine waweze kuiga, ukiingia ndani

unakuta ulinzi ni mzuri, kuna *parking* ya kutosha, ukienda kusimama njiani ukimkuta mtendaji wa taasisi hii anakusalimia anakuuliza nikusaidie nini japo kuwa sio kazi yake anakuongoza. Huo ndio mfano, pia unapomuangalia anakuchekea japo kuwa pale wewe umeumizwa unadaiwa kodi, lakini unapoingia pale kidogo na jinsi unavyopokewa unaingia moyo kwamba hii taasisi ni ya kwetu hapa nimekuja kupata huduma na naamini mtu utasaidiwa.

Kwa hiyo, mimi niwapongeze sana *Zanzibar Revenue Board* kwa kubadilika. Lakini niombe pia taasisi nyengine ambazo zina-*deal* na wananchi na wafanyabiashara tofauti waige mfano wa *Zanzibar Revenue Board.*

Mhe. Mwenyekiti, *tagert* ya *Zanzibar Revenue Board* ya ukusanyaji wa bilioni mia tatu na arubaini na saba ni fedha nyingi, na katika eneo moja ambalo *Zanzibar Revenue Board* watatakiwa wakusanye ni katika sehemu ya biashara ya Utalii. Mhe. Mwenyekiti, *Zanzibar Revenue Board* wanawekewa *tagert* ya mwaka mzima, kwa mfano wanatakiwa wakusanye kiasi hiki lakini katika *revenue collection* hasa katika masuala ya mahoteli unakuta kwamba *rate* wanayowekewa ni ile ile ya mwaka mzima kwa mfano unamwambia mtu utatakiwa ulipe dola mia *per person*.

Sasa ni sahihi kum-*charge* dola mia katika mwezi wa Julai na Agosti, lakini kum-*charge* mgeni dola mia mwezi wa Mei, mwezi wa Novemba ambapo ana hoteli pengine vyumba 80 au 70 ndani, ana vyumba unamwambia kuwa 10 ndio vilivyolaliwa 70 viko vitupu, tutakuwa sisi hatumtendei haki.

Suala la *seasonal rates* duniani kote linatumika. Vile vile kuna suala la *lastminute.com booking* ukienda kuangalia unapata, kuna

*last minute cancellations* unakuta watu unajaza vyumba. Kuna pia *weekend rate,* kuna *contract rate.* Sasa mtalii anapotoka Ulaya anauzwa zaidi ya mara tano au sita na hii yote inatokana na *commission*. Lakini ukimwambia leo mtu wa hoteli a-*charge* dola 100 *per person* na yule mgeni hamtoi yeye peke yake, anauzwa kutoka Italy, ikiwa ni Uingereza au ikiwa ni Marekani mpaka anafika Zanzibar anakuwa ameshauzwa zaidi ya mara tatu au mara nne, na hao wote kati kati wanapata *commission*. Lakini sisi kwa upande wa Zanzibar tunabakia kumkamua huyu aliyekuwepo hapa hoteli alipe ile iliyokuwepo.

Sasa inawezekana ipo kwamba wapo mahoteli kwenye suala la *comply* hawalipi ipasavyo, nakubali mimi. Lakini kitendo cha ku-*generalize* kutumia lugha ndani ya viongozi wa serikali kusema watu wa mahoteli wanatuibia, kitendo cha kuzungumza lugha ndani ya Baraza la Wawakilishi kwamba wawakezaji hawa-*comply* wanatuibia fedha zetu ni kosa na sio vizuri kwa sababu wawekezaji wetu ni lazima tuwapende na tuwasimamie. Lakini pia haiwezekani tukasema kwenye *corruption* mtendaji mmoja wa serikali anapokosea kwamba wafanyakazi wote wa serikali wawe ni wala rushwa, tunamsimamia yule ambaye ametenda kosa hapo ndipo haki inapotendeka.

Mhe. Mwenyekiti, sasa ukiangalia kwenye sekta ya utalii ukenda mwaka 1999 tulikuwa tuna-*collect* hapa bilioni moja kwenye *Zanzibar Revenue Board* wakati Rais alikuwa Dkt. Salmin Amour Juma. Leo ukiangalia tupo kwenye mabilioni na hakuna viwanda, hakuna madini, hakuna *oil and gas* ni sekta ya utalii. Sasa inakuwaje tunasema kwamba hawa wawekezaji hawa-*comply* wote.

Mhe. Mwenyekiti, sasa cha kufanya ni ku-*review* maeneo yote ya sekta ya utalii, wale ambao wanastahiki kuingia katika *seasonal*

*rate*. Kwa sababu suala moja ni bora tuwe tunaweka vitanda vyetu vinajaa kuliko kubakia na kitanda kitupu, mwezi wa Novemba na Disemba ni miezi kimya.

Kwa kweli niliwahi kuzungumza hapa ni jinsi gani ya kuondoa *visa fees* kwa ajili ya *East African* watu ambao wanaishi ndani ya Jumuiya ya Afrika Mashariki pamoja na Addis Ababa ambapo kuna watu ambao wanafanya katika *International Communities Diplomatic Missions* tuweze kuwaangalia kuwaleta Zanzibar katika miezi ya kimya. Nikazungumza suala la *green seasons* kwa mwezi wa Machi, Aprili na Mei pamoja na mwezi wa Septemba, Oktoba na Novemba, ili kuhakikisha kwamba katika miezi ya kimya tunabadilisha mawazo na fikra za wale ambao wanapenda kutembea kwa ajili ya mapumziko kuja Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, hiyo *visa fees* nikashauri kwa wale ambao wanaokuja Zanzibar moja kwa moja, ina maana sisi kama tunasema tunaondoa *visa fee* kama unakuja Zanzibar tutakukamua wewe upande wa huku. Mimi naamini mapato hapa tutaweza kuona tofauti na tutaweza kuwasaidia wawekezaji na ninaamini *ZRB* watafaidika zaidi.

Lakini Mhe. Mwenyekiti, katika suala la utangazaji wa Zanzibar. Mhe. Waziri ningemshauri sana, anataka mapato na anataka fedha lakini hataki kuitangaza Zanzibar. Narudia tena Mhe. Waziri anataka mapato mengi anawawekea *target ZRB* mwaka mzima wapate hiki na hiki, lakini *ZRB* iko miezi wakienda katika mahoteli kuangalia wanapokaa na watu wanaona kabisa vitanda ni vitupu, tunawawekea *target* katika miezi ambayo hawawezi kukusanya mapato. Hii miezi inayotoka sasa hivi ni mwezi wa 5 na mvua hizi tulizotoka nazo, ukienda katika mahoteli vitanda vitupu. Hata wewe Mhe. Mwenyekiti, leo katika maeneo ukitaka kwenda kupumzika katika *rate* kama mtu anakuwa anakuchaji

dola 100, basi atakuambia lala bure lipa chakula tu uende zako ukapumzike. Maana yake bora kile kitanda kitumike.
Mhe. Mwenyekiti, yapo mahoteli yanafunga mikataba na mahoteli katika kipindi kama hiki ambapo mtu ukienda katika *normaly* ya *high season* ana- *charge* dola 130 mpaka dola 140. lakini katika miezi hii ana-*charge* dola 49 mpaka dola 50 *half toll* na anafanya hivyo kwa sababu ya kuhakikisha kwamba wale wafanyakazi wake wanaendelea kutoa huduma, wanachangamka na hoteli vile vyumba havikai vikafungiwa. Pia unapata fedha japo kidogo kulipa mishahara.

Mhe. Mwenyekiti, hadi leo hata ukiangalia katika mahoteli haya ya Watanzania Wazanzibari waliyokuwanayo. Unakwenda katika hoteli za kawaida mtu ana-*charge* shilingi 50, anaambiwa alipe dola 9, dola 9 ni shilingi 18 *minus* 50 anabakiwa na shilingi 30 alipe *breakfast*, umeme na mshahara anabakiwa na kiasi gani. Hivi tunawatendea haki, hao ni Wazanzibari wazalendo wanafanya biashara. Kwa hivyo, lazima tuangalie katika mazingira hayo.

Mhe. Mwenyekiti, suala jengine nizungumzie utangazaji. Mhe. Mwenyekiti, namalizia dakika zangu nimeshakuona. Mhe. Mwenyekiti, hili ni gazeti la Afrika ya Kusini, angalia Nairobi wanatangaza wao wenyewe, lakini ukiangalia humu ndani kuna *rates* wanazitoa wanafanya, angalia kuna *rate* ya kwenda kutoka Fuket hapa ni Thailand, Abudhabi na Seychelles nchi tatu unalala kwa siku 13, sawa. Mhe. Mwenyekiti, hapa unalipa *Rand* 20,999 sawa na dola 1700 kwa siku 13 *all inclusive flights accommodation* pamoja na *taxes per person*. Kwa hivyo, Zanzibar tuna-*charge* hali kutokana na mazingira yetu, na ukiangalia hili gazeti ambapo tuna two *flights a week the main* kuja Zanzibar, hakuna eneo hata moja wanatangaza Zanzibar, ni Mauritius, Seychelles na nchi nyengine. Kwa hivyo, Mhe. Waziri atumie

fedha kuitangaza Zanzibar, wizara inayohusika asione tabu kuwapatia fedha kwenda kuitangaza Zanzibar. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, kwa kumalizia pale mjini Zanzibar zamani palikuwa pana *Tour Operator* ameandika kwenye ubao nje anatoa *free transfer* kutoka *Stone Town* kwenda mpaka *Airport*, *transfer* bure kwa mzungu yeyote, wewe ukigonga mlango unapewa bure. Lakini mzungu akiingia ndani anamuuliza unataka kufanya *Space Tour*, unataka kwenda *Prison Island*, akimwambia aa sitaki, anamwambia aa sasa itakuwaje nikupe *transfer* bure. Kwa hivyo, hakuna *transfer* bure, nunua kitu kwanza halafu ndio nitakupa hiyo *transfer* bure kutoka mjini kwenda uwanja wa ndege.

Mhe. Mwenyekiti, nimuombe sana Mhe. Waziri ajitahidi na ninamtakia kila la kheri katika bajeti yake. Mimi bajeti hii kwa hali ilivyo naunga mkono kwa asilimia mia juu ya mia, nimuombe tu mambo madogo madogo ambayo yanaondoka *Airport* kama suala la *domestic card* hizi wawapatie wageni katika ndege wajaze, wakifika pale *Airport* wasipate vikwazo sana, haya masuala ya takwimu ndege zote duniani hizi *backing cars* wanajaza kwenye ndege.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hayo, nakushukuru sana kwa kunipa fursa hii. Mimi kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Tunguu naunga mkono hoja mia juu ya mia. Ahsante sana kwa kunisikiliza. *(Makofi)*

**Mhe. Mwenyekiti:** Ahsante sana Mhe. Simai Mohammed Said wa Jimbo la Tunguu. Nilimwita Mhe. Hassan Khamis Hafidh lakini sijamuona. Naomba nimwite Mhe. Hidaya Ali Makame, Mhe. Dkt. Makame Ali Ussi, ajitayarishe.

Lakini Mhe. Hidaya Ali Makame kabla ya kuendelea naomba tutambue uwepo wa wageni wetu wa leo ambao ni wa Mhe. Spika wa Baraza la Wawakilishi Zanzibar, nao ni kutoka Shirika la Ndege la *Turkish Airline*, wageni wenyewe ni kama wafuatao:

1. Ndg. Geral Miraji Issa - Meneja wa Shirika
2. Ndg. Ahmed Sahin - Mkurugenzi wa Shirika hilo.

Karibuni sana. *(Makofi)*

Sasa naomba nimwite Mhe. Hidaya Ali Makame akifuatiwa na Mhe. Dkt. Makame Ali Ussi na Mhe. Hamza Hassan Juma ajitayarishe.

**Mhe. Hidaya Ali Makame:** Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipatia na mimi fursa ya kuweza kuchangia machache juu ya hotuba hii ya Wizara ya Fedha na Mipango.

Mhe. Mwenyekiti, nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia bado tukiwa kwenye hali ya uzima na afya na tukiendelea na mfungo mtukufu wa Ramadhan. Niwaombe tu wananchi wote wa Zanzibar waendelee kufunga Ramadhan hii Karim kwa nia safi na kwa kuitendea haki, ili kupata malipo mema mbela ya *Allah*.

Mhe. Mwenyekiti, nianze kwa kumpongeza sana Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango kwa hotuba yake hii ambayo inatupa moyo na kutupa matumaini makubwa wananchi wa Zanzibar, lakini pia kwa wizara zote ambazo anazisimamia na kuziendeleza vizuri kwa kuzipatia mapesa, ili ziweze kufanya kazi na kuwatumikia wananchi wa Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, moja kwa moja niende kwenye hotuba hii katika ukurasa wa 39 kuhusu Mamlaka ya Uwekezaji na Uendelezaji wa Vitega Uchumi (*ZIPA).* Mhe. Mwenyekiti, nimpongeze tena Mhe. Waziri kwa kazi kubwa aliyoifanya katika kipindi hiki tangu kuwepo kwenye wizara hii mpaka sasa hivi tunaona mabadiliko makubwa kwenye wizara hii, lakini na utendaji wa umakini wake na hali ya ukakamavu na kujua kwamba nini kinapaswa kutendwa kwenye wizara hii, nimpongeze sana Mhe. Waziri.

Lakini ningependa sana kumuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Mwenyekiti, juu ya mamlaka hii ya *ZIPA* aliangalie sana suala la wawekezaji wanapokwenda kupata hizi leseni au niseme *lease* kwa kupitia hii Mamlaka ya Uwekezaji. Mhe. Mwenyekiti, hapa kuna migogoro mikubwa ambayo inapatikanwa kupitia wananchi na hawa wawekezaji wetu.

Mhe. Mwenyekiti, suala la upatikanaji wa *lease* ni suala jepesi sana kwa sababu wanapokwisha kupata *lease* pale wale wawekezaji wanakwenda kwenye sehemu ambazo wamepangiwa kuwekeza ikiwa kwenye mahoteli au kwengine. Mhe. Mwenyekiti, lakini tunaona hapa kwamba wananchi hawashirikishwi ipasavyo hususan kwenye haya maeneo ambayo yanawekezwa kwa sababu mwekezaji anapokuja hapa aidha ameshakuwa tayari mwenyewe ameshalenga sehemu gani anakwenda kuwekeza. Kwa hivyo anafika hapa kwa kutaka ile *lease* au na vile vitu vyengine kama vibali ili kwenda kuwekeza sehemu hiyo, lakini wengine wanapangiwa na wizara ni maeneo gani watakwenda kuwekeza.
Lakini wanapokuwa na taratibu hizi hakuna taratibu zinazochukuliwa kwa kukutana na hawa wananchi waliomo kwenye haya maeneo ambayo hawa wawekezaji wanakwenda

kufanya hiyo biashara ya uwekezaji. Kwa hivyo, kunakuwa kuna migogoro ambayo inajitokeza hapa baina ya wananchi, serikali na wawekezaji.

Mhe. Mwenyekiti, ningemuomba sana Mhe. Waziri suala hili kwa sasa alifuatilie na aliwekee kipaumbele, ili kuona kwamba hawa wawekezaji wanapokuja je, hizo sehemu ambazo wanataka kwenda kuwekeza wananchi wameshughulika nazo vipi kwa masuala ya kilimo, lakini pia kwa masuala yao mengine ya kujitafutia maisha.

Kwa hivyo, tumeona kwamba hawa wawekezaji wao wanapokwisha kupata hivi vibali, basi wanatafuta magari ya kwenda kuweka sawa hayo maeneo, hawajali kama kuna vipando vya wananchi, hawajali kama kuna kitu gani wananchi wamefanya pale. Wao kwa vile lile eneo wameshapatiwa na hati zote wameshapata wanazo, kwa hivyo wao wanajijua kwamba hakuna kitakachowakwaza wala hakuna kitakachowakamata wao wasiweze kufanya zile shughuli zao za uwekezaji, na wananchi wanakuwa hawakubali juu ya suala hilo.

Kwa kweli, kama mwananchi tayari keshafanya masuala yake ya kilimo kwenye mahala pale, unakuta yeye ndio kategemea pale, kula yake itoke pale na masuala mengine. Kwa maana hiyo, unakuta sana wananchi hawa ni wale wakulima na wakwezi, lakini hawapewi ile haki ya uwananchi kwa sababu hawashirikishwi kwenye kuwapatia hawa watu haya maeneo ya uwekezaji, kwa hivyo wananchi wale wanakuwa wanajihisi wao wanadhalilika, wananyanyasika na haki zao hazifuatwi.

Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, ningemuomba sana Mhe. Waziri suala hili aliangalie na alitizame kwa umakini zaidi. Tunataka sana nchi yetu iendelee na maendeleo yapatikane, kwa sababu

hayo maendeleo yatakapopatikana, basi sisi wananchi wa Zanzibar ndio tunaonufaika na ndio tunaofaidika. Hivyo, kwa vile sisi ndio tunaofaidika na sisi ndio tunaonufaika tunataka sana na tunajua sana kwamba ardhi ni mali ya serikali, kwa vile ni mali ya serikali na serikali ndio ina mamlaka ya kufanya chochote kile kinachoamulika kinachotakiwa. Lakini waangalie na hawa wananchi wao ambao wapo ndani ya nchi hii na wanazitegemea ardhi zile zile kwa kufanyia mambo yao mengine ya kujitafutia riziki na kufanya pirika zao nyengine za kimaisha.

Mhe. Mwenyekiti, nikitoka hapo niende kwenye suala la ujenzi wa mitaro. Nimpongeze sana Mhe. Waziri, katika hotuba yake hii ametuambia kwamba katika kipindi kilichopita kwenye mwaka wa fedha 2016/2017 wamemalizia mitaro ya maji iliopo Mtopepo. Lakini katika bajeti hii ya mwaka wa fedha 2017/2018 pia ametwambia kwamba kuna mitaro ambayo itafanyiwa marekebisho na mengine itatengenezwa zaidi, ila hakututajia ni mitaro ya wapi na wapi na ni sehemu gani ambazo zitawekewa hiyo mitaro.

Mhe. Mwenyekiti, tukiangalia sehemu nyingi katika nchi yetu hii kwa sasa mvua kidogo tu au mvua ndogo tu ikinyesha basi tunaona maji yanajaa na kufurika katika maeneo hayo. Kwa hivyo, kuna haja kubwa ya maeneo mengi kuwekwa hii mitaro. Kwa vile yeye tayari ameshatuambia hapa kwamba mradi huu bado unaendelea na utaendelea kuchimba hii mitaro, basi aje atwambie tu ni maeneo gani kwa kipindi hiki itafanyiwa hiyo mitaro, ili wananchi wajue wajiweke tayari kwa kulikamilisha hili na kusaidiana na serikali yao, ili kuona mazingira yanakuja na mazingira yanakaa sawa katika maeneo yetu haya.

Mhe. Mwenyekiti, pia Mhe. Waziri katika hotuba yake hii amelizungumzia suala la ujenzi wa ofisi za serikali. Mhe.

Mwenyekiti, tunaziona ofisi nyingi za serikali kwamba kiwango chake hakikidhi au hakiko vizuri. Kwa kweli, ukienda kwenye ofisi hizi wakati mwengine utaogopa hata kutizama juu au utaogopa kutizama chini, kwa sababu imani yako haikupi hasa kwamba wewe kweli ndio unakaa pale au unakwenda mule kufanya kazi zako au wale watendaji ambao wamo mule, wanafanya zile kazi zao masaa 24 au muda wote wa kazi ambao wamepangiwa kufanya zile kazi.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli majengo mengine hayaridhishi na hali yake iko vibaya, kwa sababu ni majengo ya siku nyingi na tayari yameshakuwa mabovu. Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, ningemuomba sana Mhe. Waziri kupita kwako Mhe. Mwenyekiti suala hili nalo alipe kipaumbele ili kuhakikisha kwamba ofisi hizi, zinakuwa nzuri na zinaridhisha kwa sababu ndio ofisi ambazo tunazitegemea nazo kwa serikali yetu. Lakini pia watendaji wake ili nao wawe na moyo wa kutenda hizi kazi zao kwa ukamilifu au kwa umakini zaidi, basi majengo haya nayo yaimarishwe ili yawe mazuri zaidi.

Mhe. Mwenyekiti, pia niende kwenye suala la benki niipongeze sana Benki ya *PBZ* kwa kazi zake ambazo inafanya za kuwahudumia wananchi wa Zanzibar, inafanyakazi muda wote masaa 24, ili kuwapatia wananchi mahitajio yao pale mtu anapohitaji kwenda kupata huduma. Lakini Mhe. Mwenyekiti, kuna changamoto kubwa ambazo zinaikabili benki hii. Zipo changamoto nyingi tunajua, lakini maeneo mengi yao yapo mjini. Kwa mfano, ukenda Kwerekwe mjini, ukenda Malindi mjini, ukenda Mlandege mjini, ukenda huko Shangani pia nako ndio huko mjini.

Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, japokuwa hizi *ATM* nazo ndio sasa hivi zimeenea zinapelekwa huko maeneo ya nje ya mji, lakini

bado tunakuta kwamba *ATM* hizi haziko kwenye umakini zaidi, kwa sababu kuna *ATM* ambayo imefunguliwa hapa KMKM Kibweni, hii *ATM* imefunguliwa hivi karibuni.

Lakini, kwa kweli Mhe. Mwenyekiti, mpaka muda huu kama utakwenda si chini ya mwezi na zaidi tangu ifunguliwe basi *ATM* hii bado haifanyi kazi, na tunajisifu kwamba pale tayari angalau sisi tunaotoka kule Kaskazini, mtu akishapata yale masafa ya kutoka Nungwi mpaka pale, angalau anapumua kutokana na hizi vurugu zinazokuwepo huku anaona pale ndio keshapunguziwa masafa, lakini bado *ATM* ile haifanyikazi. Kama imeanza kufanyakazi basi haizidi siku mbili au wiki.

Kwa hivyo, ningemuomba sana Mhe. Waziri kupita kwako Mhe. Mwenyekiti suala hili nalo aliangalie na awaangalie wananchi walioko mashamba, ikiwa Kaskazini, Kusini au ikiwa Magharibi suala hili nalo aliangalie kwa kuwatafutia wananchi hawa wepesi wa huduma hizi za benki.

Kutokana na hali hiyo, kuna haja ya benki hii kuweka matawi yake kila *centre* ya mkoa, ili wananchi hawa nao waweze kupata nafuu ya huduma hii, kwa sababu siku mbili hizi zilizopita kuna pencheni za wazee ambazo zimetoka, kwa kweli kulikuwa kuna mtihani mkubwa wa msongamano ndani ya benki hizi zote ukienda zimejaa, yaani ile harufu ya zile pesa zinavyonukia uzuri wake basi huisikii unasikia jasho la watu.

Watu hawa ukiwaangalia wengi wao wanakuwa ni watu wazima ambao hawajiwezi zile purukushani za kusongamana na watu hawawezi, lakini unakuta bado kwa vile ndio wana shida waende kwenye benki hizi ili wapatiwe huduma. Unamkuta mzee katoka shamba pale tokea saa 12 asubuhi kapanga foleni na Ramadhan hii mpaka saa 12 jioni kwa kweli ni mtihani. Hivyo, kuna haja

Mhe. Mwenyekiti, kufanya kila hali katika mikoa kutafuta *center* kuweka huduma hii ya benki japo matawi madogo tu, ili huduma hizi ziwe nzuri na ziwe endelevu kwa wananchi.

Vile vile, namuomba sana Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Mwenyekiti, akiangalie kijiji cha Nungwi sasa kilivyo kijiji, kile sasa hivi umekuwa ni mji mkubwa ambao una kila hadhi ya kuwekwa *ATM* pale. Kwa kweli kijiji cha Nungwi kina mahoteli makubwa, wafanyabiashara wakubwa pamoja na wavuvi na wakulima pia wanatumia huduma hizi za benki wanapata shida.

Wakati mwengine, mtu anakuwa na shida pengine ata elfu hamsini tu, basi inabidi atoke Nungwi aje mjini, na mjini kwenyewe ukija wakati mwengine ndio kama hivyo unakuta mitihani mtu aende na kurudi si chini ya siku tatu kwa kufuata ile huduma. Kwa hivyo, nimuombe Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Mwenyekiti, akiangalie kijiji cha Nungwi sasa hivi kutokana na hadhi yake iliyonayo na mji jinsi ulivyokuwa maana Nungwi ya sasa na ya zamani tofauti.

Kwa kweli sasa hivi Nungwi imekua na ina haja yakuwekewa hii *ATM* nayo katika kijiji kile au hata kama usiiweke pale Nungwi, lakini japo maeneo ya karibu ikiwa Mahonda au Kinyasini pia itakuwa umewapunguzia ule msongamano au ule mwendo mkubwa wa kuweza kufuata huduma hii mjini, ambapo pengine mtu hata hiyo nauli ya shilingi elfu mbili ya kutoa kule kuja huku anakuwa hana, hususan ukiangalia hawa walimu wetu wa skuli ambao nao wanapatiwa huduma hizi kwa kupitia hizi benki zetu. Kwa hivyo, nimuombe Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Mwenyekiti, akaliangalia suala hili kwa kushirikiana na hizi benki, ili wakaweza kupatiwa pale na wao hii huduma ya *ATM* au haya matawi madogo madogo kama kuwekewa haya maeneo husika ya mashamba.

Mhe. Mwenyekiti, nisingependa kuseme mengi juu ya hotuba hii kwa sababu naiona imesheheni kila kitu na maelezo yake yako kwenye umakini zaidi na yanaonekana na yako wazi. Kwa maana hiyo, nimpongeze sana Mhe. Waziri kupita kwako Mhe. Mwenyekiti kwa hotuba hii, aendelee kuimarisha maendeleo ya wananchi wa Zanzibar. Lakini pia aendelee kuziangalia wizara hizi zilizomzungumza juu ya kuzipatia mapesa, ili ziweze kufanya kazi kwa wakati, hususan huu wakati kwa sababu pesa zinapatikana, lakini huu wakati uzingatiwe kwa asilimia. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, kwa kumalizia niseme naunga mkono hotuba hii asilimia mia moja. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti. (*Makofi*)

**Mhe. Mwenyekiti:** Ahsante sana Mhe. Hidaya Ali Makame kwa mchango wako, Mwakilishi wa vijana kutoka Kaskazini Unguja. Sasa naomba nimwite Mhe. Dkt. Makame Ali Ussi, atafuatiwa na Mhe. Hamza Hasssan Juma na Mhe. Ali Khamis Bakar ajitayarishe.

**Mhe. Dkt. Makame Ali Ussi:** Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa fursa hii na mimi niwe mmoja kati ya waliochangia wizara hii adhimu Wizara ya Fedha na Mipango moyo wa nchi, kwa sababu bila ya wizara hii hakuna jambo lolote linaloweza kwenda.

Kwanza nianze kwa kumpongeza sana Mhe. Waziri wa Fedha na Mipnago kupitia kwako Mhe. Mwenyekiti, pamoja na watendaji wote wa wizara hii kwa kazi nzuri ambayo wanaifanya. Nasema kazi nzuri kwa sababu nimeyapitia pitia maelezo hapa nimeona jinsi walivyoyaeleza na nimeona jinsi walivyokusanya mapato, kwamba mapato yamezidi matumizi kwa kiasi kikubwa sana, na hivyo kuuwezesha Mfuko Mkuu kupata akiba itakayosaidia baadae.

Kwa hivyo, nasema hongereni sana Wizara ya Fedha na Mipango, wanatumia vyema zile *Philosophical Issues of Management* za fedha ambazo zinatutaka sote tuwe na udhibiti halisi kwa kutumia *Regional Social Control* ambayo inatuwezesha kubaini changamoto mbali mbali zinazojitokeza ambazo mara nyingi huwa kama za kawaida. Changamoto hizi katika *Philosophical Issues of Management* huwa zinaitwa *New Normal* yaani kitu kipya, kitu ambacho si cha kawaida kinatokea halafu kinakaa kawaida, lakini wao sasa wameanza kuyashughulikia ambapo kama kitu kipya cha manufaa wanakiendeleza vizuri na kitu kipya sicho cha manufaa wanaki-*address* na kukitoa kisiendelee. Narudia hongereni sana. *(Makofi)*

Sasa mimi nianze kwa bajeti lakini kabla ya hapo niseme moja kwa moja kwamba ninayoeleza sikusudii kuzuia kifungu wala sitaki maelezo kwa sababu naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

Kwa kweli kazi nzuri iliyofanywa bila ya shaka inahitaji pongezi lakini kuna mambo madogo madogo hakuna mkamilifu, kuna mambo madogo madogo, ambayo kwa kweli yanapaswa tuyazingatie. Kwanza katika kitabu hichi pameainishwa matumizi na mapato sasa matumizi na mapato haya hatuwezi kuyachambua kama kuna maendeleo kama hatuna *reference* ya nyuma kama miaka miwili iliyopita angalau sasa hapa pana mwaka mmoja tu. Lakini kwa ukweli ni kwamba yamekwenda vuziri matumizi ni madogo kuliko mapato.

Sasa nikienda hapa kwenye mapato kodi, kuna kodi au kuna mapato ya kodi ambayo yako *TRA*, *ZRB* na *PAYEE* halafu pia kuna mambo ya mikopo ya ndani. Lakini moja kwa moja mimi niende kwenye gawio kutoka *BOT* naona hapa kuna zero lakini

mwaka jana sijaona kama kulikuwa na chochote au hakikuwepo. Sasa mwaka jana ingekuwa kuna kitu kimeelezwa hapa tungejua sasa kwamba hili ni jambo la kawaida *new normal*, ambayo sasa mnataka kuishughulikia ili isiwepo tena mapato yale yawe yanapatikana. Kwa hivyo, nashauri tu ile mikakati inayoendelezwa zipatikane hizi fedha, basi iendelezwe na itiliwe mkazo ili ziweze kupatikana kwa njia zinazostahiki.

Halafu nikienda kwenye Kodi za Bohari, hizi bohari kama zipo moja, mbili, tatu au ngapi zinajulikana na *rate* zake ziko *fix*, lakini hapa kuna asilimia 15 ya malipo ya Kodi za Bohari sasa sijui. Kutokana na hali hiyo, Mhe. Mwenyekiti napendekeza ufuatiliaji ufanyike, ili zikusanywe kodi hizi kama ambavyo zinatarajiwa kwa sababu bila ya shaka bohari hizi tumezikodisha.

Lakini pia hapa hapa kwenye bohari nizungumzie kwamba dunia hii hivi sasa inaweza kutokea majanga ya aina yoyote wakati wowote, kama vile vita nje huko wenzetu tunasikia mara kwa mara, hawa wazalishaji wa mchele pengine nao waje wagombane inakuja kuwa matatizo, kama hatuna maghala ya kutosha ya kuweza kuhifadhi chakula angalau kwa mwaka tukasubiri vipindi vile vya misuko suko vikamalizika tunatumia kile tunachokipata, basi nadhani atunaweza kuingia kwenye misuko suko sana. Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, nashauri tuzingatie sana suala la ujenzi wa maghala ya akiba, wenzetu wanayo maghala ya akiba miaka mia chakula ikitokea matatizo wanacho. Hapo kwa kitabu nimemaliza.

Mhe. Mwenyekiti, sasa niende kwenye shughuli za kiuchumi. Uchumi wa Zanzibar unakuwa *characterized* na uchumi wa visiwa, yaani umo una sifa za uchumi wa visiwani ambavyo uko *confirmed* umeangukwa na maji kwa hivyo utakuwa kwa mujibu eneo tulilonalo, eneo ni dogo kwa hivyo uchumi wake tuupate

humo humo ndani ya kidogo. Kwa hivyo, lazima tuzidishe kuzalisha kwa eneo ili tuweze kukuza uchumi wetu, hatuwezi kukuza kwa ku-*extend* eneo kwa sababu liko *so limited* hata tukisema tunakuza bado tutafika pahala hatuna tena sababu.

Sasa uchumi unachangiwa na uzalishaji na utoaji wa huduma hii ipo hata kwenye vitabu vingi vya Wizara ya Fedha vimeandika hivyo, na huduma hizi kwa bidhaa mbali mbali ambazo kasi ya ukuwaji wa pato la taifa hutegemea sana uimara wa vianzio hivi ambavyo hutegemea tena sana pia nyenzo kama vile maliasili, rasilimali watu na uwekezaji ikibebwa sana na teknolojia ya kisasa.

Kwa maana hiyo, ili pato liongezeke lazima kuimarisha sekta ya kilimo, kwa sababu kuna mipango hapa imeshapangwa tayari Wizara ya Fedha inafuatilia. Hivyo, Wizara ya Fedha na Mipango ihakikishe kwamba pamoja na bajeti iliyopangwa kwenye kilimo kwa sababu huko ndio kwenye uzalishaji wa chakula, basi na wao wafuatilie, ili uzalishaji huo uweze kuongezeka si kufuatilia tu bali kuongeza hata fedha, ili wazalishaji waongezeke, uzalishaji wa mazao ya chakula na biashara ni muhimu sana.

Mhe. Mwenyekiti, nataka niseme kwamba zao la karafuu tunasafirisha kwa wingi, kwa sababu hatulitumii sana hapa, isipokuwa tunalitumia sana kwa dawa tu, lakini kama ingelikuwa tunalitumia nadhani hata huo utafutaji wa zao letu kuu ungekuwa mdogo. Kwa kweli tunaona hapa watu wanalima kila siku mpunga, muhogo na hautoshi bado tunaula wote tunaozalisha na ziada tunaagiza kwa wenzetu Tanzania Bara. Kwa hivyo, tuimarishe sana kilimo hasa utafiti ili tuweze kupata mahitaji ya chakula cha kutosha hapa nchini.

Sekta ya viwanda nayo hatuna budi pia kuikuza kwa sababu tutaweza kuzalisha vitu hapa ambavyo, vitatupunguzia kuagizia vitu vingine kutoka nje. Sekta ya fedha kwa upande wa kodi hizo nazo ziimarishwe kuna bandari bubu huko ziko nyingi zinashughulikiwa, najua tena zinashughulikiwa sana lakini bado iko haja ya kutia mkazo kuingia bandari bubu ili kila kinacholetwa au kila kinachosafirishwa kiende kwa fulani kuongeza mapato ya nchi, bandari bubu pia kuna *tax* bubu na hizo pia zishughulikiwe.

Halafu sekta ya maliasili ikiwemo uchimbaji huu wa mafuta tunategemea kuchimba mafuta Mwenyezi Mungu atujaalie tuyapate. Mhe. Mwenyekiti, kuna nchi zilichimba mafuta zikaacha zile kazi zao za kawaida, kama vile kilimo wakashughulikia mafuta matokeo yake mafuta pengine yakaja yakazorota kidogo kilimo wamekiacha misuko suko ya uchumi ikatokea. Kwa hivyo, nashauri Wizara ya Fedha na Mipango kwa kupitia kwako Mhe. Mwenyekiti, isimamie mwendelezo wa kilimo wakati huo huo mwendelezo wa mafuta, ili tuweze kupata tija kubwa zaidi.

Lakini pia tuangalie kunakochimbwa mafuta siku zote kuna *environmental repercussion* nyingi sana, kwa hivyo pia tujaribu sana tuje tudhibiti *environmental repercussion* zinazoweza kutokea ili tusije tukapata athari ya uchimbaji wa mafuta, kwa kupata mambo ambayo yanasababisha maafa kwa jamii.

Mhe. Mwenyekiti, hata maliasili kama hayo mawe yanayochimbwa basi nadhani Wizara ya Fedha na Mipango twendeni tukaangalie humu mnamochimbwa tunaweza kufanya nini tukasaidia Wizara ya Fedha, ili muweze kufanyiwa kitu ambacho kitaweza kuzalisha. Halafu ardhi yetu hii inapungua siku zote na nasema Wizara ya Ardhi ndio inayohusika, lakini nasema

kuna mipango Wizara ya Fedha inashughulika na mipango ya kuona kwamba mahali fulani tunaweza kusaidia jambo fulani ili uchumi wetu uendelee.

Kwa hivyo, nasema na hili pia waangalie ardhi yetu kwa miaka mingi tunasema kilomita hizo zilizotajwa kwa miaka mingi tunasema lakini inaliwa na maji ya bahari inapungua, lakini tada tiliopo ndio zile zile za miaka ya nyuma, kwa hivyo nadhani Wizara ya Fedha sasa nayo ione haja ya kapanga mipango na hili la ardhi kupungua lishughulikiwe.

Halafu kuna sekta ya biashara sasa kuna *SME* hizi nazo ni muhimu Wizara ya Fedha tujitahidi sana kuzisimamia hizi *SME* kupitia wizara zinazohusika, ili kuziwezesha ziweze kutoa ajira kwa vijana na vile vile kuweza kuongeza uchumi wa nchi, kwa sababu hawa *Small and Medium Enterprise* hawa ndio wengi kuliko hawa wafanyabiashara wakubwa. Hata ukiangalia mapato yanayopatikana kwa wafanyabiashara wadogo ni mengi kuliko mapato yanayopatikana na wafanyabiashara wakubwa waliopo. Nadhani iko haja sasa ya kuishughulikia sana hii sekta *SME*.

Mhe. Mwenyekiti, sasa niende kwenye mfumko wa bei. Utulivu wa bei ni muhimu kwa maendeleo ya kiuchumi, bei zinapopanda huathiri sana hali ya maisha ya watu hususan masikini, jamii inakosa utulivu wa maisha na wakati mwengine huweza kusababisha ukosefu wa amani. Mhe. Mwenyekiti, nashauri kama nilivyosema mwanzo kama tuweze kuzalisha bidhaa nyingi, tujenge maghala, ili tuwe na vyakula vya kutosha, ili huu mfumko wa bei duniani usituathiri sana maana yake bei zikipanda huko duniani na sisi hapa tunapata matatizo.

Sasa niingie kwenye udhibiti wa *assets*, yaani *liquid assets* pamoja na zile *fixed assets*. Tumeona katika ziara zetu mimi ni

mjumbe wa Kamati ya *PAC*, kwa hivyo nimeona katika ziara zetu kwamba kuna matatizo kidogo ya udhibiti wa fedha. Wakati mwengine inatokezea ubadhirifu pengine hata si ubadhirifu ni uzembe tu umetokea inaonekana mtu kaiba kumbe wala hajaiba, imetokezea uzembe pale kwa sababu yeye ndio *responsible* anakutwa na kitahanani. Kwa hivyo, kuna mambo ambayo kwa kweli tunastahiki kuyashughulikia.

Kwa mfano, lazima tuangalie kwamba zinaweza kutokezea *operation risk* ambazo kwa kweli tunaweza kusababisha upotevu wa vitu. Kwa hivyo, nasema ni vizuri sana tukawa na vitu kama *Asset Register* tukaweza kurekodi vitu vyetu vyote haya mabuku ya kumbukumbu nyengine mbali mbali za matumizi ya fedha yakawa yanapitiwa mara kwa mara, ili upotevu unapotokea unajulikana haraka haraka na unasawazishwa haraka haraka.

Mhe. Mwenyekiti, nikienda tena kwenye suala la *risk* ambayo inaweza kutokezea na kusababisha upotevu kwa kupitia *human resource* ni kwamba, mara nyingi sana unaweza ukakuta mahala kuna mhasibu pengine shughuli zake zilikuwa ni *administration* lakini kawekwa mhasibu hii kwa bahati mbaya. Lakini, hivi sasa naona hili jambo linashughulikiwa ipasavyo. Kutokana na hali hiyo, naiomba Wizara ya Fedha na Mipango kupitia kwako Mhe. Mwenyekiti izidi kutia mkazo kuweka watu ambao wanao *qualifications* zile ambazo zitaweza kuendeleza udhibiti wa fedha bila ya kupotea.

Mhe. Mwenyekiti, sasa naomba nizungumzie suala la takwimu. Takwimu zetu kwa kweli tunajua *population* hapa ni 1.3 milioni na mipango yetu ya kiuchumi na maendeleo tunaipanga kwa kuangalia hiyo takwimu. Lakini, Mhe. Mwenyekiti ukitizama kuna watu wanaingia kwa wingi, kuna watu wanazaliwa kwa wingi na halafu ukiangalia hasa wakati takwimu zilipokuwa

zinachukuliwa watu wengi walijificha hawakutaka kujitokeza kuhesabiwa. Kwa hivyo, nadhani kama ingewezekana kufanya sensa ya dharura tukajua *actual* ni watu wangapi, basi ingekuwa ni vizuri sana na mipango yetu ya maendeleo tungeweza kuipanga vizuri.

Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu tukipanga maendeleo tukizingatia watu milioni 1.3 wakati wako milioni 2 au milioni 2.5 hatuwezi tukapanga mpango ambao utakuwa *effective* kwa maendeleo ya watu. Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti nashauri sana elimu kwanza itolewe, ili watu wanapohesabiwa wasijifishe watu wengi huko vijijini walikuwa wanajificha kabisa hawataki wahesabiwe sababu watakuwa wanazijuwa wenyewe, pia na kuna watu wengine walikuwa wanashawishi hasa msikubali kuhesabiwa. Kwa maana hiyo, nashauri sana sana hizi takwimu zichukuliwe sawa kwa kipindi cha miaka 10 nadhani kinachukuliwa, nadhani hapa katikati tuwe na *assessment* nyengine kuhakikisha kwamba ile takwimu iliyopatikana ni sahihi kabisa.

Baada ya kusema hayo, Mhe. Mwenyekiti niseme narudia kuunga mkono hoja hii ya Hotuba ya Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango, kwamba ni nzuri na nashauri wenzangu tuiunge mkono kwa asilimia mia, ili mipango hii iliyopangwa iweze kutekelezwa kwa ufanisi. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti kwa kunipa fursa. *(Makofi)*

**Mhe. Mwenyekiti:** Ahsante sana Mhe. Dkt. Makame Ali Ussi kwa mchango wako. Lakini, kabla sijamwita Mhe. Hamza Hassan Juma, naomba tutambue tena wageni wetu wa leo nao pia ni wageni wa Mhe. Spika wa Baraza la Wawakilishi Zanzibar. Wageni hao ni kutoka Australia.

Wageni wenyewe ni:

1. Mr. Anton Hardy
2. Mrs. Jenny Hardy.

Karibuni sana, karibuni sana. *(Makofi)*

Sasa naomba nimwite Mhe. Hamza Hassan Juma atafuatiwa na Mhe. Ali Khamis Bakari na Mhe. Hassan Khamis Hafidh ajitayarishe pamoja na Mhe. Omar Seif Abeid.

**Mhe. Hamza Hassan Juma:** Mhe. Mwenyekiti, mimi nataka nikushukuru kunipa nafasi hii nikaweza kutoa mchango wangu wa mawazo ikiwemo hotuba ya Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango pamoja na maoni ya wananchi wangu ambao waliokuja kunishauri mambo mbali mbali kuhusu kuchangia Hotuba hii ya Wizara ya Fedha na Mipango.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli Mhe. Waziri kitabu chake kimesheheni mambo mengi mazuri sana na tunashukuru kwa mwenendo huu, kama Mhe. Waziri ataweza kuyasimia vizuri yale ambayo anayokuja kutuahidi kama anavyoahidi kwenye hotuba yake hii ya bajeti, naamini kila mwaka tutakuwa tunapiga hatua za maendeleo. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri ameonesha wazi wazi yale aliyoyaeleza humu ukuaji wa mapato asilimia ime-*reflect* mpaka ndani ya ukumbi huu imeonekana kweli mapato yamekua na kwa kuwa mapato yamekua, basi hata sisi ukiangalia Wajumbe wa Baraza la Wawakishi suti zetu zinaonesha zinang'ara kwa kukua kwa mapato. Tunakushukuru sasa Mhe. Waziri wa Fedha, ili *style* uliyoitumia ya Kidonge indelea kuitumia kila mwaka. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, makofi hayo yanadhihirisha kwamba kweli Waheshimiwa Wajumbe wameridhika na kile ambacho unachokifanya. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, kwenye bajeti hii kama nilivyosema mwanzo kitabu kinajieleza mafanikio mazuri. Lakini na mimi kuna kadhia ya wananchi wangu nitamuomba sana Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Mwenyekiti anisikilize pamoja na Mhe. Mwanashera Mkuu, kwa sababu katika ile asilimia mia moja ya kitabu, basi kuna asilimia 20 ya wananchi itabidi nipate maelezo ya kutosha.

Mhe. Mwenyekiti, kabla kuingia kwenye kitabu nitaanza na kadhia ya wananchi wangu. Naanza na suala la hatua iliyochokuliwa na Wizara ya Fedha na Mipango kupitia Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango kwa wale wafanyakazi tisa ambao Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango alichukua hatua ya kuwasimamisha kazi ili uchunguzi upite.

Mhe. Mwenyekiti, sisi kama Baraza tunampongeza sana Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango kwa jitihada zake, na kwa sababu kuna mambo mengine hasubiri tumwambie sisi, yale ambayo anayogundua kupitia vyanzo vyake mbali mbali anaweza kuyafanyia kazi kwa haraka. Kwa kweli si busara kusubiri jambo linaharibika mpaka unasubiri wakati wa bajeti tena lishaoza, ndio tunakuja kulizungumza yeye anapopata taarifa anachukua hatua za haraka.

Sasa zoezi lile sote tumeliunga mkono, lakini kimsingi tulikuwa tukihitaji maelezo kidogo kwa sababu toka Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango amechukua hatua ile sasa hivi muda umekuwa mrefu sasa. Hivi sasa karibu mwaka mmoja, kwa sababu sisi tunaongozwa na Katiba na Sheria za nchi tuangalie Sheria ya Utumishi wa Umma inaelezea wazi wazi mfanyakazi

anaposimamishwa kwa uchunguzi atapata nusu mshahara kwa muda wa miezi sita, lakini vile vile kuna *examption* katika sheria hizo, kwamba Waziri anaweza akaona kwamba anahitaji kuendelea na uchunguzi zaidi anaweza kuongeza muda kwa hatua ile ya *suspension*.

Mhe. Mwenyekiti, naomba Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango aje anipe hatua kwa sababu tulipata taarifa kwamba kuna bodi iliundwa, ambayo ilikuwa na watu wazito sana, taasisi nzito sana, tunaamini ile Ripoti ya Uchunguzi imeshamfikia Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango. Kwa hivyo, tunategemea ili haki itendeke, ile ripoti kama imeshafanyiwa kazi na kama kuna hatua zozote zilizochukuliwa.

Mhe. Mwenyekiti, kitu ambacho wananchi wangu wamenilalamikia, kwamba mpaka hii leo bado wameekwa *pending* wanaendelea kupata nusu mshahara, lakini hawaridhiki kwa sababu hawajisii kama wamefanya makosa. Sasa kama nilivyosema mwanzo hatua aliyoichukuwa Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango tunaiunga mkono baada ya kusikia harufu mbovu akachukua hatua ya haraka kabla pahala hapajaoza.

Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Mwenyekiti, wakati atakapokuja kutoa majumuisho, basi hili doa tu kidogo alirekebishe, ili niweze kuja kuiunga mkono hotuba yake kwa asilimia mia moja. Tatizo au hofu yangu muda kila ukizidi kwenda kuna baadhi ya sheria tutakuwa tunazikiuka, baada ya ile nia nzuri ya Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango kuweza kuwachukulia hatua watu wale ikaenda vyengine, sasa jambo ambalo hatulipendelei.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hayo sasa nakuja kwenye hotuba yenyewe. Mhe. Mwenyekiti, katika kitabu cha Mhe. Waziri wa

Fedha na Mipango, ameeleza lile lengo alilokusudiwa au alilowekewa kukusanya karibu bilioni 824, kuna malipo ya kodi mapato milioni 447 na zile ambazo zisizo na mapato yasiyo na kodi fedha za wafadhili. Lakini kuna bilioni karibu 33 hizo tuliziweka *reserve* kwa ajili ya kuweka ile nakisi ya bajeti.

Mhe. Mwenyekiti, katika makusanyo yale kwa kweli tunashukuru taasisi zetu ambazo tulizo zikabidhi kazi za kutukusanyia mapato *ZRB* pamoja na *TRA*, kwa kweli wamefanya kazi nzuri sana katika lile lengo ambalo walilopangiwa kwa muda wa miezi tisa waliweza kuvuka lengo karibu asilimia 108.6, hili ni jambo la kupongezwa sana, Mhe. Mwenyekiti, tunawaomba waendelee na isije ikawa ile hadithi ya mgema uko mbele simalizi, lakini hadithi ya mgema sisi wenyewe Waswahili tunaijua.

Kwa hiyo, kwa kiasi fulani *ZRB* kidogo walijirekebisha wamekaza kamba na kwa sababu Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango tumemuona mara tu baada ya kuchaguliwa alifanya vikao vingi na watendaji hawa, na zile kauli zake pamoja na miongozo yake naamini iliweza kusaidia sana watendaji wale wakaweza kumsikia na wakaweza kujitahidi na kuongeza mapato. Lakini, *TRA* na wao vile vile wameongeza mapato karibu kwa asimilia 109 sawa na *ZRB* 109. Kutokana na hali hiyo, Mhe. Mwenyekiti, wao tunawaomba waongeze jitihada, ili kuhakikisha kwamba mapato yetu yanaongezeka na taasisi zetu zinatononoka pamoja na kuweza kufanya mambo mengine.

Mhe. Mwenyekiti, naomba maelezo kidogo wakati atakapokuja Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango kuhusiana na zile *PAYEE*, katika ile *PAYEE* wafanyakazi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wanaofanyia kazi zao hapa Zanzibar, tulitegemea tupate karibu bilioni 21 lakini tumepata bilioni 15. Mhe. Mwenyekiti, sasa naomba Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango wakati

atakapokuja atuweleze kwa kumalizia *quarter* kwa sababu hii ni ripoti ya miezi tisa. Kwa hiyo, tutegemee ndani ya kipindi kikimalizika cha mwaka mmoja, yaani miezi kumi na mbili, tutegemee na ile iliyobakia bilioni 6 tutaweza kuipata bilioni kama 5.25 je, itaweza kupatikana au kwa mwaka huu tutakuwa ndio tumepata kasoro kwenye *PAYEE*.

Mhe Mwenyekiti, nasikitika sana kwa upande wa Fedha za Washirika wa Maendeleo, tulitegemea tupate karibu bilioni 3.26 lakini matokezeo mpaka kufikia kipindi hichi cha miezi tisa tumepata karibu bilioni 58.61 sawa sawa na asilimia 18 hii kwa kweli ni *alarm* ambayo amewekewa Mhe. Fedha na Mipango pamoja na sisi wananchi wa Zanzibar kwamba "Mtegemea cha ndugu hufa maskini".

Tumezoea sana kusikia tu Washirikia wa Maendeleo, Washirika wa kila tunachokipanga tunaangalia zaidi Washirika wa Maendeleo, lakini matokeo yake ni hiyo hapo katika 3.26 tumepata karibu 58. Mhe. Mwenyekiti, hii ndio inatuambia tuongeze jitihada ya mapato yetu ya ndani, ili kuhakikisha kwamba uchumi wetu tunaotegemea kwa mapato yetu sisi wenyewe kwa jitihada zetu.

Mhe. Mwenyekiti, katika bajeti hii sisi wajibu wetu Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango ameshaeleza ukomo wake hapa wa kufikiria mapato, sasa sisi tumueleze fikra zetu ili kuweza kumuondoa hapa kumuongezea zaidi fikira nyengine katika kujaza mapato ya nchi. Sasa nitaingia kidogo katika eneo hilo.

Mhe. Mwenyekiti, Wizara ya Fedha na Mipango ndio wizara mama. Kwa kuwa Wizara ya Fedha na Mipango ndio wizara mama inatakiwa kuwalisha na taasisi nyengine, ili waweze

kuongeza mapato katika taasisi zao na vile vile na fedha ziongezeke katika Mfuko Mkuu wa Serikali. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, mimi ni Mwenyekiti wa Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi wa Baraza la Wawakilishi, kwa kweli kamati yangu imegundua kuna mapato mengi sana bado hatujaweza kuyakusanya na nitakuja moja baada ya nyengine.

Kwanza, naanza katika Uwanja wa Ndege wa Zanzibar. Mhe. Mwenyekiti, uwanja wa ndege unajiendesha kutokana huduma za uingiaji wa abiria na uondokaji wa abiria na uingizwaji wa mizigo na utokaji wa mizigo. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, kuna baadhi ya ndege kubwa ambazo ndege hizo zinasafirisha mizigo mbali mbali kutoka nchi tofauti kwenye nchi nyengine, ndege zinashindwa kutua Zanzibar kwa sababu hakuna mzigo wa kuchukua. Kwa nini na wala sio kama mizigo inakuwa haipo, mizigo inakuwa ipo lakini tatizo kuwa hatuna x-*ray machine* ya *cargo* pale *airport*.

Kutokana na hali hiyo, namuomba sana Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango kupitia kwako Mhe. Mwenyekiti, *x-ray machine* ya *cargo airport*, hivyo naomba waangalie namna gani tutaweza kushirikiana na Mamlaka ya Viwanja wa Ndege, ili iwekwe pale ili ndege kubwa *Emirates* na nyengine ziweze kutua, kwa ajili ya kupakia mizigo hapo tutakuwa tumeongeza mapato ndani ya serikali.

Mhe. Mwenyekiti, eneo jengine ambalo tunahisi tunaweza tukaongeza mapato ni eneo ambalo tumelizungumza sana na ninamshukuru sana Mwanasheria Mkuu kupitia kwako Mhe. Mwenyekiti, jana kwa kweli alifanya kazi ya kizalendo sana alipokuwa akichangia Hotuba ya Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji,

Nishati na Mazingira. Mhe. Mwenyekiti, ukenda katika ukanda wa utalii ni aibu kuna makuta mengi, hakuna mradi kuna mapori mengi, hakuna mradi watu wamejaa na *leases* majumbani mwao.

Mhe. Mwenyekiti, kuna wawekezaji mbali mbali sasa hivi wapo na wengine wanakuja na wanaondoka wanashindwa kupata maeneo ya kuwekeza, tena ni wawekezaji wa maana kabisa. Mhe. Mwenyekiti, leo watu kukaa na *leases* majumbaji mwao watu kutujengea makuta, makuta yameshaoza leo watu wanataka kuja kuwekeza.

Kwa hivyo, naomba sana Mhe. Mwenyekiti, mwekezaji yeyote hawezi kupewa *lease* mpaka apate *recommendation* ya *ZIPA*. *ZIPA* wao ndio wanaombwa mtu anataka kufanya mradi *ZIPA* ndio... Mhe. Simai Mohamed Said ondoka. Mhe. Simai hapo ondoka tunazungumza Bajeti ya Serikali. Mhe. Mwanasheria Mkuu pamoja na Waziri watusikilize, muondoe. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, naomba kwanza muondoe Mhe. Simai Mohamed Said.

**Mhe. Mwenyekiti:** Mhe. Hamza Hassan Juma naomba uzungumze na kiti.

**Mhe. Hamza Hassan Juma:** Mhe. Mwenyekiti, nimekuomba Mhe. Simai Mohamed Said aondoke tutazungumza vitu hapa vya bajeti ya nchi.

**Mhe. Mwenyekiti:** Mhe. Hamza Hassan Juma naomba uongee na kiti kwa sababu hao unaozungumza nao nina imani kama mnavyomsikia waziri mahiri kwa hii bajeti yupo makini na anakusikia. *(Makofi)*

**Mhe. Hamza Hassan Juma:** Ahsante. Mhe. Mwenyekiti, ukiangalia sheria za nchi muwekezaji kabla ya kuwekeza anatakiwa apeleke *request* yake *ZIPA*, kwa hiyo *ZIPA* anaeleza aina ya mradi anaoufanya. Kwa maana hiyo, namuomba sana Mhe. Waziri Fedha na Mipango kupitia kwako Mhe. Mwenyekiti, kwamba aidha ashirikiana na kamati yangu au kamati nyengine yoyote twende tukakague watu waliopewa *leases* na miradi iliyofanywa.

Mhe. Mwenyekiti, kuna watu wengine wanayo maeneo makubwa lakini ukiingia ndani, na ndio maana katika yale makuta wanaweka mageti makubwa, ili mtu asipate kuingia ndani kuangalia nini kilichofanyika. Kuna vibanda katika mradi wake walioupeleka *ZIPA* atajenga hoteli yenye vyumba ishirini na nne, thalathini, arubaini unaingia ndani ya kuta vyumba vitatu. Mhe. Mwenyekiti, hayo ni mapato ya serikali yanapotea.
Vile vile kuna wengine hata hivyo vibanda viwili, vitatu hapana, halafu tunasema aa maana yake uchumi mdogo, uchumi mdogo. Mwalimu Julius Kambarage Nyerere alisema uchumi tunao lakini tunaukalia. Siku aliposema hivyo watu wakasema aa Mwalimu Nyerere maana wale walifikiria vyengine. Lakini Mwalimu Nyerere alisema uchumi tunao tunaukalia kwa sababu tunazo rasilimali hatuzitumii. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, namuomba Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango pamoja na Mhe. Mwanasheria Mkuu kupitia kwako Mhe. Mwenyekiti, kwamba waandae safari na mimi nitawapeleka. Juzi nilipata bahati ya kwenda Mexico na mimi bahati nzuri nikenda pahala popote lazima nijifunze nilichokiona halafu nije kuishauri serikali yangu. Mhe. Mwenyekiti, tulikwenda kule *Cancun* katika lile eneo la utalii wameweka kama *buffer zone*, eneo la utalii ni maeneo ya mahoteli matupu, upande huku wa pili ndio kuna nyumba za kawaida na vitu vyengine tofauti.

Mhe. Mwenyekiti, kuna safari moja aliwahi kuja aliyekuwa Makamo wa Rais wa Kenya Mr. Kalonzo Musyoka akatembelea maeneo ya Nungwi, akenda Lagema pamoja na sehemu nyengine. Akamwambia Mhe. Waziri Kiongozi wake wakati ule ni Mhe. Shamsi Vuai Nahodha kwamba Zanzibar ni nchi ya kushangaza sana kwamba bado mnategemea mapato kutoka kwa wahisani wa nje. Akasema nyinyi nchi yenu ni pesa, ile Zanzibar yenyewe ni pesa.

Mhe. Mwenyekiti, naomba sana Wizara ya Fedha na Mipango kwa kushirikiana na *ZSSF*, Shirika la Nyumba, pamoja na Tume ya Mipango wafanye tathmini nyumba zilizokuwepo mfano Nungwi, Matemwe, kwetu Pwanimchangani, ule ukanda wa pwani, wananchi wale uandaliwe utaratibu zijengwe nyumba za kisasa ikiwa za maghorofa au nyengine kwa kukaa kwa kushirikiana nao waondolewe kule pwani, ili wapandishwe juu wajengewe nyumba za kisasa zenye huduma zote. Maeneo ya pwani yabakie ni maeneo ya utalii tutakusanya pesa nyingi sana. Hayo ndio tuliyoyaona waliyofanya wenzetu. Mhe. Mwenyekiti, naamini Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango ni msikivu, ziara hiyo ataiandaa kwa kushirikiana na Mhe. Mwanasheria Mkuu tutakwenda kuwaonesha hayo maeneo. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, nataka niondoke hapo nije *ZUSP*. Kwa kweli ninashukuru nilipiga kelele kwa muda mrefu sana, lakini sasa hivi namshukuru sana Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango kwa kushirikiana na Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ, kwamba ile mitaro ambayo iliyoanzwa kujengwa imeanza kuleta *relief* kubwa kwa wananchi wetu.

Kwa mfano, Jang'ombe, Chumbuni, Shaurimoyo, Kwamtipura ilikuwa wakati wa mvua lazima watu waende na vidau, tunawashukuru sana na Mwenyezi Mungu atawalipa kwa hiki mlichotufanyia. Mitaro ile sasa hivi mvua zikinyesha ndani ya masaa mawili maji huyaoni tena. Kwa kweli tunawashukuruni sana. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, namuomba Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango kwa kushirikiana na Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ, waangalie mpango mkuu wa lile bwawa la Mwanakwerekwe. Tunaamini hawa hawa mliowapa kazi ya kutengeneza hii mitaro mkiwapa na kazi ya pale maji yale wataweza kuyaondoa ili eneo lile litumike kwa shughuli nyengine za maendeleo.
Mhe. Mwenyekiti, nikija katika upande wa *ZIPA* tena narudi. Kwa kweli Kamishna wa *ZIPA* ni rafiki yangu sana kuliko sana, lakini namuomba sana kupitia kwako Mhe. Mwenyekiti kwamba aondoe urasimu, bado wawekezaji wanakuja wanazungushwa kwa muda mrefu. Wawekezaji wanakuja na *capital* wanataka kuwekeza anawazunguusha sana. Nikisema hivyo nadhani atakuwa amenifahamu. Nitazungumza mfano mmoja, Zanzibar sasa hivi ni nchi ambayo inajengwa, kuna muwekezaji anataka kuwekeza kiwanda cha nondo, sasa hivi karibu ya miezi tisa hajapata jawabu. Je, ardhi hatuna au vipi.

Kutokana na hali hiyo, namuomba Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango kupitia kwako Mhe. Mwenyekiti, kwamba hili *specific* wakati atakapokuja anieleze kwamba ardhi hatuna au hatuna kitu gani. Mwekezaji huyu ana viwanda karibu nchi tano za Afrika anataka kuja kuwekeza kiwanda cha nondo, ili kupunguza bei ya nondo ambayo itakayoweza kuzalishwa. Sasa mpaka leo anazunguushwa huku na kule, utafikiri pembeni hapa tunakuja kwenye kazi. Mhe. Mwenyekiti, naomba taarifa pamoja na

maelezo je, mwekezaji huyu tuambiwe kama ardhi ipo ajue na kama haipo ajue mtaji wake aupeleke sehemu nyengine.

**Mhe. Mwenyekiti:** Ahsante Mhe. Hamza Hassan Juma umepewa dakika zako 20 nimekuongezea na tano kwa hivyo nakuomba umalizie. Hizo tano nazo pia zimeshamalizika. *(Makofi)*

**Mhe. Hamza Hassan Juma:** Naomba mbili.

**Mhe. Mwenyekiti:** Kwa hivyo, nakupa dakika moja umalizie.

**Mhe. Hamza Hassan Juma:** Mhe. Mwenyekiti, ah! haya bwana. Mhe. Mwenyekiti, naomba sana kuna jambo ambalo nitazidi kumkumbusha Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango kupitia kwako kuhusu suala la Mfuko wa Barabara. Katika eneo ambalo tunaridhika sana na matumizi yake ni Mfuko wa Barabara unatusaidia sana, na kwa bahati nzuri sasa hivi mfuko ule tumeupa kazi nyengine baada ya kufanya Ugatuzi wa Madaraka Mikoani, mfuko ule utakwenda mpaka kwenye Halmashauri, hakuna hata mheshimiwa mmoja aliyekuwa hana barabara mbovu za ndani ya jimbo lake.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa sisi ndio tunaopitisha bajeti, basi tunamsamehe Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango kwa bajeti hii, lakini kwa bajeti ijayo tunaomba ile *road toll* ya mafuta ambayo inakwenda kwenye Mfuko wa Barabara niliomba tuongeze shilingi hamsini, ili ile *capital* iwe kubwa Mfuko wa Barabara upate pesa nyingi kwa ajili ya barabara zetu za ndani ziweze kushughulikiwa.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hayo machache nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ya upendeleo na namuomba Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango kupitia kwako Mhe. Mwenyekiti, awe

msikivu katika yale tuliyoyaeleza tunaamini tutaweza kwenda vizuri. Naunga mkono hotuba hii kama nilivyosema kwa asilimia 80, asilimia 20 nikishakupata jawabu nzuri kwa wale wananchi wangu naamini nitaimaliza kwa asilimia 100.

**Mhe. Mwenyekiti:** Ahsante sana Mhe. Hamza Hassan Juma kwa mchango wako. Sasa nimwite Mhe. Ali Khamis Bakar huyu ameniomba dakika kumi, nitampatia dakika kumi akifuatiwa na Mhe. Hassan Khamis Hafidh na Mhe. Omar Seif Abeid ajiandae.

**Mhe. Ali Khamis Bakar:** Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi mchana huu kwa kuweza kuchangia hotuba ya Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango.

Nianze na Benki ya Watu wa Zanzibar. Mhe. Mwenyekiti, naomba kuipongeza kwa juhudi kubwa sana ambazo wanazifanya kwa kuwahudumia wananchi ambao kwa kiasi kikubwa sasa hivi wanaendelea na harakati zao za kujipatia yale ambayo yanastahiki katika benki yao.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya pongezi hizo mimi nianze kusema kwamba benki hii sasa hivi imekuwa na wateja au watumiaji wengi sana ambao Unguja na Pemba idadi ya watu imekuwa kubwa na harakati za watu zinaendelea siku hadi siku kwa kuweza kufika katika benki zetu hizi na kuweza kupata huduma.

Mhe. Mwenyekiti, tunaona kadhia kubwa ambayo inawakumba wananchi katika suala zima la benki wakati ambapo wanakwenda kwa kupata huduma. Mara nyingi tumeona kuna baadhi ya wananchi wanaweza wakafika pale kwa ajili ya kutaka kutoa pesa kwenye *ATM*, wakati mwengine mtu anakwenda kwa sababu anapunguza ule msongamano wa ndani ya benki kwa kukataa

pengine foleni imekuwa kubwa ana *ATM* yake anakwenda pale anataka atoe pesa.

Lakini jambo la kusikitisha wakati mwengine unaweza ukatoa pesa, pesa zile zisitoke ukaambiwa rudi ndani, ukifika ndani kunakuwa kuna kazi nyengine ambayo kubwa, muda wako umeshapotea na pengine ulikuwa na harakati unakimbilia kitu inakuwa ni usumbufu kusema kweli.

Mhe. Mwenyekiti, namuomba sana Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango haya matatizo kidogo kuhusu *ATM* zetu, ambazo kuna matatizo yanayojitokeza aweze kuyafikiria, ili wananchi pale wanapokwenda katika kutoa pesa, basi zipatikane pesa zile ili wapunguze ile mirundikano ya mle ndani pamoja na waweze kupata mahitaji yao kama wanavyokusudia.

Mhe. Mwenyekiti, wakati mwengine unaweza ukenda kwenye hizi *ATM* kwa mfano kama kule Pemba. Sisi mara nyingi benki zetu tunazotumia ni Chake Chake na Wete. Nimuombe sana Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Mwenyekiti, juzi nilisema hapa kwenye Wizara ya Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira kwamba Wilaya ya Micheweni sasa hivi nayo imekuwa kubwa watu wanatoka Makangale, wengine Mnarani, wengine Kiuyu Maziwang'ombe wanakimbilia kwenda Chake Chake ama Wete. Tukiangalia hapa katika kipindi hichi ambacho mvua zimenyesha inakuwa ni shida mabarabara yamekatika ilimradi pakupita inakuwa shida.

Mhe. Mwenyekiti, nimuombe sana Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango kwa sababu ni msikivu sana ambaye ukimwambia kitu siku ya pili tu kinaendelea kufanyika. Kwa hiyo, atuangalie sana watu wa Micheweni kutuwekea angalau *ATM* itatusaidia kwa sababu mtu anaweza akatoka Konde anakwenda Chake Chake

katumia nauli pengine shilingi 2,000 kwa kwenda kutoa shilingi 30,000.
Mhe. Mwenyekiti, namuomba Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango aliangalie, watu mishahara yao haizidi shilingi 300,000 au 400,000 lakini 500,000 basi kama *ATM* ipo Micheweni itaweza kutupunguzia mrundikano mkubwa ambao unakwenda kukaa kule Chake Chake au Wete. Kwanza hiyo foleni tu ya humo barabarani, mabarabara yamekatika ya kuweza kufika Chake Chake, lakini kama Micheweni ipo mtu pengine kenda kumuangalia mgonjwa pale anafika kabisa kwenye *ATM* anatoa pesa.

Mhe. Mwenyekiti, namuomba sana Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango, awaangalie watu wa Wilaya ya Micheweni wanapata shida tena kubwa watu wanatoka mbali wanakimbilia Wete na Chake Chake kwa ajili ya kufanikisha suala hili.

Mhe. Mwenyekiti, nikitoka hapo nije katika Mfuko wa Hifadhi ya Jamii ya *ZSSF*. Kwanza, niwapongeze kwa kazi kubwa ambazo wanazifanya kutoa huduma kwa jamii, lakini kuhusu majengo niwapongeze kwa majengo makubwa ambayo wanayajenga, ili kuupendezesha mji wetu. Lakini Mhe. Mwenyekiti, hapa napata masikitiko na nilikuwa natoa ushauri kwamba azma ya serikali sasa hivi ni kuona kwamba mji wa Zanzibar unapendeza na wao wana kasi kubwa ya kuweza kusukuma juu ya majengo haya, bado tunawaona kwamba wanayaendeleza. Jambo la kusikitisha kwamba majengo wanayajenga mazingira ambayo kidogo hayaridhishi.

Kwa mfano, kuna majengo hapa zaidi ya manne au matano yanajengwa lakini yametupwa. Mhe. Mwenyekiti, kwa uoni wangu majengo yale kama yameweza kujengwa katika mazingira ya mji wenyewe, basi lile lengo kwa upande wao lingefikia.

Lakini na ile azma ya serikali ambayo inataka kuufanya mji wake kuwa wa kisasa basi nayo vile vile ingeweza kupatikana kama majengo yale wangeyaweka katika maeneo ya Darajani, Mazizini, tungepata kuona mji wetu tayari umeanza kupendeza, mtu yeyote ambaye akifika pale Darajani anaanza kuona kweli sasa Zanzibar mambo yameanza kuwa mazuri. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, nikitoka hapo nije kwenye Wizara ya Fedha na Mipango. Kwanza nimpongeze Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango kwa kazi kubwa anayoifanya kwa kusimamia majukumu yake yeye pamoja na watendaji wake. Naomba nimuulize Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango kupitia kwako Mhe. Mwenyekiti, kuna utaratibu gani wa vile vitendea kazi wanavyovinunua kuvipeleka katika mawizara kwa mfano vespa, baiskeli, pikipiki na magari.

Mhe. Mwenyekiti, kweli tumeona kuna vifaa pale vinakaa ambavyo ni vichakavu wao vimeshawashinda kwa mfano labda pengine katika matumizi yao ya kiofisi havitumiki tena lakini vipo. Mhe. Mwenyekiti, nafikiri jambo zuri vifaa vile vingepigwa mnada basi wapo watu ambao vingeweza kuwasaidia na wao vikaweza kuondoka katika mazingira ya pale kuweza pengine kuondosha taka taka na lile eneo likaweza kutumika kwa masuala mengine. Kwa kweli tumeona pale kuna vifaa vinakaa kwa miaka kadhaa mwisho wa siku vinaharibika au pengine vinaanza kuibiwa chombo kimoja kimoja, maslahi yanakuwa hayapo. Lakini kama vifaa vile vingeliuzwa, basi nina imani japo robo ya pesa ingelipatikana, ili kuweza kusaidia baadhi ya mambo mengine.

Mhe. Mwenyekiti, naomba nimuulize tena Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango kupitia kwako kuhusiana na suala hili hili. Je, wana utaratibu gani wa hivi vifaa wanapovinunua kuwapelekea watu

katika maofisi. Tumeona kuna magari, baiskeli na vespa ambazo zinapelekwa katika taasisi hizi za serikali miaka mitatu pengine linanunuliwa gari la milioni mia tano lakini miaka mitatu haifiki gari ni bovu.

Je, hawawawekei labda pengine angalizo la kuwaambia kwamba jamani wizara imeshatoa vifaa hivi, lakini tunataka gari hii au vifaa hivi vifike angalau miaka mitatu au miwili au angalau tuone kwamba ile juhudi ya serikali inapofanya yale masuala ya kuwasaidia wananchi au wizara zake husika na wao wanajijali na wanaijali ile serikali na wanavijali vile vyombo.

Mhe. Mwenyekiti, lakini utaiona gari ya serikali nasikitika kwamba kule Tanzania Bara kuna mwewe pale anaangalia kila jicho lake palipo jema na baya akiliona jambo ambalo silo, basi utasikia loh! mwewe ameangalia mazingira fulani. Sasa hapa mwewe hayupo, mwewe ni sisi wenyewe tunaangalia yale masuala ambavyo yanakwenda.

Mhe. Mwenyekiti, jambo la kusikitisha unaweza ukaikuta gari ya serikali (SMZ) imepigwa mzigo wa kuni ni mtihani au imebebea vitu ambavyo havileti tija na azma na lile jambo ambalo linakwenda. Kutokana na hali hiyo, namuomba sana Mhe. Waziri Fedha na Mipango kupitia kwako Mhe. Mwenyekiti, suala hili aliangalie kwamba zile taasisi husika zinazopelekewa hivi vifaa, basi wavitunze na wajuwe kwamba mcheza kwao hutunzwa na wao ndiyo wanaotumia. Sasa wakivitumia vizuri na kuvitunza vitu vile vitawafaa wao na mwengine atakayekuja.

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea na mchango wangu sasa niende katika Mfuko wa Barabara. Niwapongeze watu hawa kuhusiana na habari nzima ya barabara na kazi kubwa ambayo wanaifanya. Lakini Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango naomba niseme kupitia

kwako Mhe. Mwenyekiti, kwamba hapa mara hii tumeona sote kadhia kubwa ambayo imewafika wananchi juu ya mabarabara yetu jinsi gani yalivyopata kupasuka, mabarabara mengi yamenyofoka, madaraja yamekatika na kadhalika.

Mhe. Mwenyekiti, kuhusiana na habari nzima ya Mfuko wa Barabara kwa pesa ambazo zimewekwa kama kuna kifungu cha kuweza kusaidia kuhamishiwa katika eneo hili napendekeza sana kwamba hizi pesa zilizopo ni kidogo, kwa sababu barabara nyingi zimekatika na hapa huu ndio Mfuko Mkuu wa Hazina ambapo barabara za ndani na za vijijini zote zinategemea kutengenezwa na serikali na yeye ndie mshika fedha. Kwa hiyo, naomba sana hapa Mhe. Mwenyekiti, apaangalie kwa macho mawili.

Kwa mfano, sisi kule majimboni kwetu sasa hivi zile barabara ndogo ndogo ambazo Mhe. Naibu Waziri wa Mawasiliano anasema sio za kwake hazipitiki. Kwa hivyo, ni vyema sasa Mhe. Mwenyekiti, aziangalie na kuona fungu lao analifanya angalau kuwa zuri ilimradi haya matatizo yanaepukika.

Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu umenipa dakika kumi na mimi sitaki nikukere. Mwisho kabisa kuhusu maslahi ya wafanyakazi. Mhe. Mwenyekiti, nimalizie kwa maslahi ya wafanyakazi. Lakini kwanza nimpongeze Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango kwa juhudi kubwa alizozifanya katika maslahi mazima mara hii, kuona kwamba wananchi wote walipata maslahi yao kuhusiana na habari ya mishahara.
Mhe. Mwenyekiti, kuhusu masuala ya wale ambao wanachukua pencheni, kuna malalamiko kidogo kwa wale wanaostaafu hucheleweshewa pencheni zao. Mhe. Mwenyekiti, namuomba Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango kupitia kwako Mhe. Mwenyekiti, kwamba waangaliwe watu hawa kama tayari wameshatumika kwa muda mrefu na wakahangaika katika serikali

yao na wizara yao kuhusiana na kwamba jamii wanaisaidia kwa hali moja au nyengine.

Mhe. Mwenyekiti, jambo la kusikitisha baada ya kustaafu inakuwa wanapata shida, mtu leo anapanda gari anaambiwa njoo Chake Chake, mara nenda Wete mara nenda Unguja, wanacheleweshewa zile pencheni zao kuweza kufika kwa wakati. Mhe. Mwenyekiti, naomba sana liangaliwe suala hili kwa sababu wanaohangaika ni wazee wetu, baada ya kustaafu kwao wao wanahitaji kwamba wapumzike na kile ambacho walikifanyia kazi kuweza kufika kwa wakati.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hayo naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

**Mhe. Mwenyekiti:** ahsante sana na mimi nakushukuru Mhe. Ali Khamis Bakar. Sasa naomba nimwite Mhe. Hassan Khamis Hafidh, atafuatiwa na Mhe. Omar Seif Abeid na Mhe. Hussein Ibrahim Makungu ajitayarishe.

**Mhe. Hassan Khamis Hafidh:** Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kunipa fursa hii mimi Mwakilishi wa wananchi wa Jimbo la Welezo, sasa hivi saa 6:30 ili niweze kutoa mchango wangu kwa wizara hii muhimu, wizara makini, Wizara ya Fedha na Mipango inayoongozwa na Dkt. Khalid Salum Mohammed.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza nichukue fursa hii kumpongeza Mhe. Rais wa Zanzibar kwa kumuona na kumteuwa Dkt. Khalid Salum Mohammed kuwa Waziri wa Fedha na Mipango. Naamini wizara hii inaongozwa na watu makini, kuna Dkt. Khalid, kaka yangu Khamis Mussa, kuna Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Fedha wote hao ni watu makini na wanafanya kazi nzuri. *However* changamoto ndogo ndogo hazikosekani pahali popote. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, watu wengi wanaulizana mbona hizi wizara siku hizi inakwenda vizuri, huyu Dkt. Khalid Salum Mohammed kaja na uchawi wa Kidonge nini? Nawaambia *as longer as* hata ukiwa uchawi wa Kidonge, lakini maadam kazi zinafanyika vizuri na pesa zinapatikana, basi sio tatizo aendelee kutumia uchawi wa Kidonge aliokuja nao umsaidie kuendesha Wizara ya Fedha na Mipango pamoja na mengineyo yajayo usoni. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, nitaanza mchango wangu na Shirika la Bima. Shirika hili ni miongoni mwa taasisi zilizokuwepo katika Wizara ya Fedha. Mhe. Mwenyekiti, naomba kunukuu ukurasa wa 27 unasema kwamba:

"Lengo kuu la Shirika la Bima la Zanzibar ni kutoa huduma za bima mbali mbali vikiwemo vyombo vya moto, bima ya moto, bima ya vyombo vya baharini na vyenginevyo".

Mhe. Mwenyekiti, Shirika la Bima linafanya kazi nzuri, limekusanya karibu bilioni 20, hiyo tu ni kuonesha kwamba inafanya kazi nzuri. Nachukua fursa hii kuwasifu sana watendaji wote pamoja na Mkurugenzi wao Abdulnasir Ahmed Abdulrahman (Machungwa) kwamba wanafanya kazi nzuri.

Mhe. Mwenyekiti, hii dhana ya bima ilianza nchi za wenzetu nchi zilizoendelea. Lengo kuu la bima ni kumlinda mwananchi anapopata maafa, kumlinda mwananchi anapopata ajali, lakini siyo kulinda gari au chombo cha moto au nyumba. Mhe. Mwenyekiti, naomba kutoa mfano, hivyo naomba nisikilizwe kwa makini.

Mhe. Mwenyekiti, tarehe nimeisahau pale Welezo ilitokea ajali ya gari ya *harrier* ilipinduka kwa bahati mbaya au nzuri ile *harrier* ikamgonga mtu, kumgonga yule mtu akakatika miguu na ile *harrier* nayo ikawa nyang'anyang'a yule dereva naye aliumia lakini akaweza kupoa. Mhe. Mwenyekiti, jambo la ajabu yule aliyegongwa na ile *harrier* mpaka leo ni mlemavu kazi anashindwa kufanya amekuwa maskini ana watoto sita Shirika la Bima halijamlipa hata pesa moja.

Mhe. Mwenyekiti, jambo la ajabu na la kusikitisha Shirika la Bima wameilipa gari mpya milioni 21, imelipwa gari. Kwa kweli najua utaratibu ambao upo si utaratibu mzuri wa kumuangalia mwananchi. Kwa hiyo, naomba kutoa ombi Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Mwenyekiti, kwamba hapa kuna kitu kinaitwa daladala labda wengine humu hawapandi sisi tunapanda daladala.

Mhe. Mwenyekiti, daladala zinatusababishia ajali tofauti siku zote zinatuulia wananchi wetu, siku zote zinawagonga wananchi wetu. Mhe. Mwenyekiti, naomba Shirika la Bima liandae program maalum lisiwe linaangalia gari sasa, isipokuwa liwe linamuangalia mwananchi kwa sababu nchi za wenzetu mtu akipata ajali analipwa, mtu akipata ajali ameshindwa kufanya kazi atalipwa mpaka afe na Shirika la Bima la wenzetu. Lakini leo hii Mhe. Mwenyekiti, Shirika la Bima la Zanzibar linaangalia gari linamuacha mtu aliyepata ajali aidha kapoteza uhai au kapata ajali ambayo ni ya kudumu hawezi kufanya kazi.

Mhe. Mwenyekiti, nililiomba hili mwaka jana, naliomba tena leo ajali zimekuwa nyingi za waendesha daladala, lazima Shirika la Bima lije na program ya kumuangalia mwananchi, si kuiangalia gari iliyogongwa na kulipwa gari mpya au pesa nyingi, hiyo moja.

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea na mchango wangu naomba kuzungumzia kuhusu *Zanzibar Revenue Board (ZRB)*, kazi yake kubwa kwa mujibu wa Katiba nafikiri ni kukusanya mapato. Kwanza, naomba kuchukua fursa hii kumpongeza Kamishna Amour Hamil Bakari anafanya kazi nzuri kwa sababu amekusanya bilioni 109 hii ni kazi nzuri. Lakini si peke yake na Mkuu wa *TRA* kaka yangu Mcha na yeye anafanya kazi nzuri amekusanya bilioni 152 hii ni kuonesha kufanya kazi nzuri. Wapewe pongezi lazima tuwashukuru pesa hizi tutazihitaji wao wanafanya kazi nzuri. *(Makofi)*

Lakini Mhe. Mwenyekiti, naomba kusema machache hii *ZRB* ina kazi ya kuwatafuta wasiolipa kodi, pia ina kazi ya kukusanya mapato, ina kazi ya kuwashtaki wasiolipa kodi kwa wakati na wasiolipa kodi inavyotakiwa.

Mhe. Mwenyekiti, naomba kutoa rai Mexican walikuwa na kitu kama hichi walipoona kwamba ili wakusanye mapato yao kwa vizuri wakaunda taasisi mbili tofauti, taasisi moja ikawa kazi zake kukusanya mapato kama *ZRB*, lakini taasisi nyengine ikawa ina jukumu jengine la kuwatafuta wasiolipa kodi, wasiolipa kodi kwa wakati pamoja na kuwashtaki.

Mhe. Mwenyekiti, Mexican wamepata ufanisi mkubwa na sasa hivi nchi yao ni miongoni mwa nchi zinazoingiza mapato makubwa kwa sababu taasisi mbili zinafanya kazi tofauti, lakini taasisi yetu ya *ZRB* inafanya mambo mengi inashindwa kuwa na ufanisi wa kukusanya mapato. Mhe. Mwenyekiti, kuna utafiti umefanyika unasema Zanzibar kama itajipanga vizuri inaweza kukusanya mapato makubwa kulikoni inavyokusanya. Mhe. Mwenyekiti, naamini kama tutafuata utaratibu Mexican tunaweza tukakusanya mapato makubwa.

Mhe. Mwenyekiti, nikitoka hapo nakwenda kunako wahasibu Mhe. Mwenyekiti najua wahasibu wako kwa Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango, lakini wahasibu wakuu na wahasibu wasaidizi kama sikosei kwa mujibu wa utumishi walitakiwa kulipwa mapesa kama wakurugenzi, ili waweze kupata pesa za kuwatosha kidogo ili ule ubadhifu upunguwe. Lakini Mhe. Mwenyekiti, wahasibu hawa leo hii wanalipwa pesa, lakini za ukurugenzi au ukurugenzi usaidizi lakini hawalipi maposho kama wakurugenzi. Sasa jambo la kusikitisha na kushangaza mhasibu mkuu huyo huyo ndiye mwenye mafuta ndiye mwenye kila kitu anawapa watendaji, lakini yeye mwenyewe hana si unamfungulia mlango na unakuwa uwazi.

Mhe. Mwenyekiti, kama tumeiga wenzetu wa Bara wale wahasibu wanawapa mshahara wa ukurugenzi, lakini wanawapa na stahiki zote za kama mkurugenzi. Mhe. Mwenyekiti, kwa lengo la kupata ufanisi kwa hawa wahasibu wafanye kazi vizuri kwa uaminifu naomba wapewe stahiki kama wakurugenzi lakini wapewe na maposho yote kama ya wakurugenzi. Naamini itatusaidia katika kupata ufanisi wa kuendeleza nchi yetu na kufanya kazi zao vizuri.

Mhe. Mwenyekiti, nikitoka hapo sasa naomba kuuliza swali hapa Zanzibar tunagemea zao letu kuu ni karafuu. Mhe. Mwenyekiti, katika kuokoa zao la karafuu kuna watu wamepata ajali, tumekuwa tukifuatilia wananchi wetu wengi walopata ajali katika mazao ya karafuu hawajalipwa pesa zao, unapokwenda unaambiwa Wizara ya Fedha, unapouliza unaambiwa Wizara ya Fedha.

Mhe. Mwenyekiti, namuomba Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango kupitia kwako wakati atakapokuja kufanya majumuisho aeleze kuhusu hawa watu waliopata ajali kwa ajili ya kuokoa zao la taifa

la karafuu atawalipa lini. Mhe. Mwenyekiti, namuamini, waziri makini, isipokuwa naomba maelezo kuhusu hili atawalipa lini mpaka wengine wanafika kufa hawajalipwa pesa zao na wanatakiwa walipwe fidia. Sasa wanapouliza wanaambiwa Wizara ya Fedha, masikini mpaka wengine wanakufa hawajalipwa fidia. Mhe. Mwenyekiti, naomba maelezo kuhusiana na suala la kuwalipa fidia hawa watu.

Mhe. Mwenyekiti, nikitoka hapa nakwenda *ZIPA*. Napenda sana kuchukua fursa hii kumpongeza Mkurugenzi Mkuu wa *ZIPA* kaka yangu Salum Nassor anafanya kazi nzuri sana ya kuwatafuta wawekezaji waje kuwekeza Zanzibar. Zanzibar imeanza kung'ara na kupendeza. Lakini nataka kutanabahisha nakuomba kitu kimoja.

Mhe. Mwenyekit, nchi za wenzetu baada ya ku-*realize* kwamba unapowaita wawekezaji wa nje wakiwa wengi kinachojitokeza faida wanayoipata wanaichukua nchini kwao inakuwa haibakii nchini, kwa maana hiyo nchi inakuwa haifaidiki. Kwa hiyo, Mhe. Mwenyekiti naomba *ZIPA* waandae programu maalum ya kuwatafuta wawekezaji wazalendo na kuwapa maeneo wawekeze ndani, ili faida inayopatikana ika *expand* na ku-*exchange* ndani ya nchi itakuwa hayaendi. Mhe. Mwenyekiti, kwa mfano wale Wataliana walioekeza mahoteli mbali mbali wanapata faida zote zinakwenda Ulaya *instead* ya kubakia, lakini tunamshukuru sana Mzee Said Bakhresa anawekeza nchini, leo hii kafungua Mtoni, kafungua huku, kafanya hivi, mwekezaji mzalendo anakuwa anawekeza nchini mali haitoi nje.

Mhe. Mwenyekiti, kwa hiyo naiomba sana *ZIPA* waje na programu maalum ya kuwahasisha wawekezaji wazalendo *instead* ya kuwahamasisha wawekezaji wa nje kuja nchini, itakuwa ndio

ule msemo wa kizungu "*We consume, we produce, but we are not consume, and we consume what we are not produce".*

Mhe. Mwenyekiti, wawekezaji wazalendo wakiwa wengi wataweza kuondosha umasikini kuliko kuwa *encourage* wawekezaji wageni kuja kuwekeza, faida yote wakaichukua nchini kwao na kwenda kununua maboti ya kuishi katika visiwa sisi tukabakia masikini.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hapo naomba nizungumzie Mfuko wa Hifadhi ya Jamii (*ZSSF*). Mhe. Mwenyekiti, naomba kumpongeza Mkurugenzi Mkuu wa *ZSSF* anafananya kazi nzuri, lakini najua *ZSSF* wanajenga majumba wanajenga majengo mbali mbali isipokuwa wanatumia taasisi za nje kama vile China na wengineo.

Kwa hivyo, naomba sana Mhe. Mwenyekiti sasa umefika wakati wa kuhakikisha yake majengo tunayojenga tutumie wajenzi wa ndani, ili tutuwe ajira na kutoa zile pesa ziweze ku-*circulate* na ku-*rotate* kwa lengo la kukuza uchumi *instead* ya kumtafuta China au Mjerumani, yaani wageni watupu waje kujenga, fedha nyingi tunawalipa. Kwa mfano, barabara unampa mgeni aje kujenga pesa anachukuwa nchini kwao, lakini ukipa mjenzi wa ndani zile pesa zinabakia zinasaidia familia pamoja na mambo mengine mengi.

Mhe. Mwenyekiti, kwa hiyo naiomba sana *ZSSF* huu mpango wao wa kujenga majumba na kujenga maeneo ya uwekezaji ni mpango mzuri, lakini wawape na wajenzi na wawekezaji wa ndani, ili waweze kujenga nyumba na wasiwape wajenzi wa nje kwa sababu wao wanachukua zile pesa na sisi tunabakia kuwa masikini.

Mhe. Mwenyekiti, kuna Mfuko wa Barabara uko chini ya Wizara ya Fedha na Mipango. Mhe. Mwenyekiti, naomba nikuombe *please* huu Mfuko wa Barabara ufanye *research* na uwangalie wapi kuna mahitaji ya kujengwa zile barabara za ndani. Kwa mfano, leo na wala sikatai lakini hayumkiniki kujenga barabara ya Kikwajuni wakati *facilities* zote Hospitali ya Mnazimmoja, Soko la Darajani mambo yote yako mjini, lakini unakwenda kuwaacha wananchi wa Welezo, wananchi wa Magharibi, wananchi wa wapi wakati ambapo kule mzazi mpaka leo inabidi azalie ndani ya nyumba au anapata matatizo wakati anapokwenda hospitali kwa sababu hakuna barabara.

Mhe. Mwenyekiti, nakuomba sana Mfuko wa Barabara uangalie maeneo yenye watu wengi ambapo ni Magharibi ikiwemo Welezo. Halikadhalika iangalie maeneo yenye shida sifikirii sikatai wa Kikwajuni wasipewe lakini aa! Kikwajuni haifanani na Welezo barabara. Mgonjwa kumtoa Welezo mpaka kumfikisha Hospitali ya Mnazimmoja inakuchukua masaa matatu au kumtoa kule Michikichini mashimo matupu hatari na magari hayakubali, lakini kumtoa Kikwajuni mpaka Hospitali ya Mnazimmoja unatumia dakika nne. Sasa inakuwaje leo Mfuko wa Barabara inakwenda kujenga barabara ya Kikwajuni na kuacha barabara ya Welezo au kuacha barabara za Magharibi.

Mhe. Mwenyekiti, tufanye utafiti tugundue wapi kuna mahitaji tuweze kupeleka maendeleo, tusipeleke maendeleo maeneo ambayo sisemi kama hakuna mahitaji, lakini si mahitaji ya lazima ukilinganisha baina ya Welezo na Magharibi na ukilinganisha na Kikwajuni. Mhe. Mwenyekiti, Mfuko wa Barabara uangalie maeneo yenye mahitaji kama Welezo na Magharibi.

Mhe. Mwenyekiti, nikitoka hapo nakwenda katika *PBZ*. Vile vile nachukua fursa hii kuwapongeza wanafanya kazi nzuri sana, leo si

jana na wala leo haitokuwa kesho, *they are doing a good job* hasa Juma Ameir pale Mkurugenzi anafanya kazi nzuri ya kimapinduzi tena ya kizalendo kabisa.

Lakini zipo changamoto ambazo kwa mfano unakwenda kwenye *ATM* pale kupata pesa inakuwa tatizo na dunia imeshasogea tujaribu kutumia, ili tupate teknolojia za kileo kwa sababu leo hii ukienda *PBZ* pale unaweza ukataka pesa zako mwenyewe ukaona adha si ndogo ukajuta kwanini umekuja kuitia benki, kila unapokwenda unaambiwa mtandao haufanyi kazi, unaambiwa mtandao hivi aaa! Haipendezi pesa yako mwenyewe unataka ukatibiwe unaweza ukaikosa itabidi ukakope na pesa unayo kwa sababu sijui mtandao haufanyi kazi, sijui mtandao umeruka, sijui mtandao umefanya hivi aaa! Hayapendezi hayo. Mhe. Mwenyekiti, tumeamua kufuata teknolojia basi bora tutumie pesa tupate *accuracy* teknolojia ambayo mtu akihitaji kitu chake akipate. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea na mchango wangu sasa naomba nizungumzie kuhusu suala la pencheni ya wazee. Mhe. Mwenyekiti, wazee wetu wamefanya kazi nzuri ya kimapinduzi wametuzaa, wametulea, wametusomesha, wametutizama, wametupindulia nchi, wametuweka pazuri. Kwa hivyo, ninalotaka kumuomba Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango kupitia kwako Mhe. Mwenyekiti, kwa wazee hawa wanapopewa pencheni mshahara *Alhamdulillah* Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kapandisha kima cha chini cha mshahara kama alivyoahidi kutoka shilingi 150,000/- mpaka shilingi 300,000/-.

Lakini je, hawa wazee jamani waliotuzaa, waliotupindulia, waliotuwekea nchi pazuri na wao tunawatazamaje pencheni yao inapanda lini, wanalalamika pencheni yao ndogo na wao

wapandishiwe. Mhe. Mwenyekiti wapandishiwe pencheni yao hawa wazee wamefanya kazi nzuri, wanajitahidi, wamejitahidi leo hii wanataka kupumzika tena wasiwe omba omba. Mhe. Mwenyekiti, naomba iwepo programu maalum mshahara ukipanda na pencheni ya wazee itapanda. Lakini jengine la kukumbuka kwamba penye uhai na majaliwa tunaweza sote tukawa pencheniya, kwa maana hiyo unapotengeneza kuwaekea pencheni nzuri ya wazee basi unajitengenezea na wewe mwenyewe.

Kwa maana hiyo, Mhe. Mwenyekiti, namuomba sana Mhe. Waziri wakati atakapokuja basi anieleze amejipanga vipi kuhusu kuiongeza pencheni ya wazee, wanalalamika pencheni yao ndogo, mishahara inapanda yao haipandi na wamefanya kazi nzuri maskini ya Mungu, hebu tuwaonee huruma. Mhe. Mwenyekiti, naamini Dkt. Khalid Salum Mohamed ambaye ni Waziri wa Fedha na Mipango kwa kushirikiana na Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa hili watalisikia na jawabu litakuwepo zuri la kimapinduzi lenye kuleta maendeleo ya kuwatetea wakulima na wakwezi wapinduzi wa nchi hii. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, tukiangalia kwenye 53 kuna ujenzi wa ofisi ya serikali programu hii ya kujenga maofisi ya serikali mradi umepangiwa jumla ya shilingi bilioni 5.57 kwa ajili ya utekelezaji wa programu mbali mbali za Ujenzi wa Ukarabati wa Majengo ya Serikali.

Mhe. Mwenyekiti, hapa nataka kumtanabahisha Mhe. Waziri naomba anisikilize kwa makini na hoja hii ndio itakuwa mchango wangu wa mwisho.

Mhe. Mwenyekiti, kwenye majenzi, kwenye manunuzi, kwenye kukarabati, kwenye mambo haya yote ndipo watu wanapokuwa

wanapiga kofi kwa meno kwamba pesa hizo watapata kula. Mhe. Mwenyekiti, sio siri juzi Mhe. Rais wa Zanzibar alipokwenda Pemba kule Wizara ya Afya kuna jengo linataka kujengwa tulimuona kwenye TV. Jengo lile lilipangiwa shilingi milioni 270 kujengwa. Mhe. Rais wa Zanzibar akashtuka hii! jengo hili shilingi milioni 270 akasema labla shilingi milioni 50.

Sasa hapa ndio tuone jinsi gani kunako mambo haya pesa zinapopigwa buti. Mhe. Mwenyekiti, mfano huo kama hautoshi kulikuwa na jengo la Spika wa zamani la Wizara ya Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo linataka kujengwa kwa ajili ya Shirika la Magazeti ilipangiwa shilingi milioni 275 kama sikosei. Mimi mjumbe wa kamati tukaweka mkwala tukasema haiwezekani ku-*repair* ikiwa Chuo cha Utalii kimejengwa kwa shilingi milioni 200, kufanya *repair* nyumba ile ndogo ya chini milioni 270 aaa! Hee! Mnataka kutufanya sisi wagonjwa hatukubali, hatutaki hapa ipo namna. Mhe. Mwenyekiti, leo jengo lile limefanyiwa *repair* kwa shilingi milioni 140 na tuna ushahidi kwamba hawa waliolifanyia *repair* jengo lile wametumia shilingi milioni 90, shilingi milioni 50 wamepata faida lakini lilikuwa limepangiwa milioni 270.

Mhe. Mwenyekiti, kama hiyo haitoshi twende Pemba kule kunakokaa wazee Pemba kunaitwa Limbani Pemba, kuna jengo limejengwa kwa zaidi ya shilingi milioni 120 Limbani Pemba ukiliangalia saruji imetiwa kiraka milango imetiwa rangi tu, bati limetiwa jeupe la kawaida unapokwenda kwenye vitabu unakuta shilingi milioni 120zimetumika. Mhe. Mwenyekiti, namuomba Mhe. Waziri katika mambo haya ya ununuzi mambo haya ndipo watu tena wapochukua hizi pesa za serikali wakafanya kama zao bila huruma, ndio maana Zanzibar inabakia kuwa masikini lakini kuna watu wanakuwa matajiri.

Mhe. Mwenyekiti, namuomba Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango anzishe Idara Maalum yeye ndiye mwenye kuzitoa pesa, nchi za wenzetu pesa wanayoitoa wanaiangalia imetumika kwa matumizi sahihi na imepatikana ile *value for money* kama haijapatikana, je kile kinachonunuliwa ni sahihi kinakwenda na ile *market* ya wakati ule.

Lakini, sio tunatoa tu tukishatoa basi, kwa sababu Wizara ya Fedha na Mipango imetakiwa kutoa chukuweni na wala hakuna suala la ufuatiliaji, lazima iwe inafuatia ilichokitoa kimetumika matumizi sahihi, kilichotolewa kimefanyika kinachotakiwa, ilichokitoa kinakwenda na *value for money* isiwe kimetolewa shilingi milioni 270kumbe ilikuwa inataka kutumika shilingi milioni 100Kwa utaratibu huu, Mhe. Mwenyekiti tutakuwa hatuendelei, tutakuwa kila siku hapo hapo lazima tulichokitoa tukijuwe.

Mhe. Mwenyekiti, ni vyema Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango anzishe idara tunamuamini Dkt. Khalid Salum Mohamed ya kuratibu kilichotolewa kuhakikisha kilichotolewa kinatumika kwa usahihi na kinatumika *according the value* Mhe. Mwenyekiti wakati mwengine tunatiwa changa la macho, katika kununua ama kujenga utaambiwa jengo hili, basi hivyo mtu binafsi anaweza kufanya *repair* nyumba ile pale kwa shilingi milioni 270 si ujanja tu wakutaka kujinufaisha nafsi yake.

Mhe. Mwenyekiti, hatutaki kusema mengi ushahidi kama huo tunao mwingi tunaletewa kila siku hasa hizi tenda. Mhe. Mwenyekiti, tenda ziko tenda tatu zimetoka juzi tunao ushahidi wa kutosha ambapo hizo tenda ukiziangalia na ukizifuatilia zote zina ujanja ndani yake.

Mhe. Mwenyekiti, hatutaki kutoa ushahidi hapa isipokuwa tunakwambia tu leo, kwamba haya masuala ya tenda, ujenzi, pamoja na mambo kama haya uyafuatilie kwa kina kuna watu wanatupiga bao serikali kila siku inakuwa haina pesa, lakini pesa nyingi inatumia katika kuwatafutia wananchi wake maendeleo isipokuwa kuna wajanja wachache wanajinufaisha matumbo yao.

Mhe. Mwenyekiti, kitabu chako ukurasa wa 53 katika masuala ya ujenzi; ununuzi; pamoja na tenda uwe muangalifu sana lazima uunde kamati au tume maalum ya kufanya *analysis* ya mambo haya ya tenda, ujenzi pamoja na manunuzi. Mhe. Mwenyekiti, ushahidi tunalewa na watu hao hao wanaofanya kazi katika taasisi hizo hizo wanatuletea ushahidi wa kutosha, hatutaki kuutoa leo tunauweka, lakini wanatuletea bwana tenda ile kapewa mtu fulani, lakini kapewa mtu fulani kwa sababu katoa gari, tenda ile kapewa mtu fulani kwasababu katoa hichi, tunaambiwa na hao hao Mhe. Mwenyekiti na ushahidi wanatuletea. Mhe. Mwenyekiti, siku hizi kila anayenijia namwambia niletee ushahidi unaletwa na ushahidi, tunambiwa tenda ile kapewa mtu kwa sababu katoa hichi, Mhe. Mwenyekiti, kwa utaratibu huo tunakuwa hatuendelei. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, tunarudisha vitu vyetu tunawacha kwa leo tunakuamini, lakini tunakuomba sana ukalisimamie hilo namuona Mhe. Mwenyekiti tayari anataka kuwasha taa yake. Leo sina mengi naomba kuunga mkono hoja hiyo ya Wizara ya Fedha na Mipango asilimia thamanini asilimia ishirini mpaka wakati atakapokuja kufanya majumbuisho Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango na kunipatia ufafanuzi kuhusu hoja yangu walioanguka katika kuliokoa zao kuu la nchi hii karafuu atawalipa lini pesa zao zile za ruzuku zinaitajwe pesa za fidia, watalipwa lini pesa za fidia asilimia ishirini atawalipa lini wote karibu watu mia mbili mpaka mia tatu.

Baada ya hayo machache Mhe. Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja asilimia thamanini naomba kuwasilisha.

**Mhe. Mwenyekiti:** Ahsante sana Mhe. Hassan Khamis Hafidh Mwakilishi wa Welezo. Sasa naomba nimwite Mhe. Omar Seif Abeid anafuatiwa na Mhe. Hussein Ibrahim Makungu na Mhe. Mohamed Said Mohamed ajitayarishe.

**Mhe. Omar Seif Abeid:** Mhe. Mwenyekiti, na mimi nashukuru kwa kunipa ya kutoa mchango wangu kwenye Wizara hii adhibu ya Fedha na Mipango. Wizara ambayo tokea tuanze bajeti hii sijawahi kuona mambo namna hii, kwamba hakuna misuguano, hii ni dalili ya kutosha kwa namna ya kipekee kwamba Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango Dkt. Khalid Salum Mohamed ni mtu mwenye uelewa na uwezo wa kufanya kazi. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, nachukua fursa hii kumpongeza sana, kwa sababu ya mambo mazuri ambayo ameyaanisha na nina amini kwamba kama hakutayatekeleza asingeweza kuyaandika kwenye kitabu hiki. Kwa hiyo, nachukua nafasi hii kumpongeza sana Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango kwa bidii pamoja na juhudi yake anayoichukua katika kusimamia mapato ya nchi hii.

Mhe. Mwenyekiti, ni ushahidi tena wa wazi kuwa uwezo wa Dkt. Khalid Salum Mohamed katika kazi hizi ni pale alipoweza kutekeleza kauli azma ya serikali ya kuongeza mishahara ya kima cha chini. Wizara ya Fedha na Mipango nasema hongereni sana, kuanzia mwenyewe Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu, Makamishna wote wa Fedha na watendaji wote hongereni. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, pia pongezi zangu hizi zinakuja kwenye ukurasa wa 5 pale nilipoona kwamba wameweza kukusanya

kufikia makusanyo ya bilioni 448.15 kwenye makadirio yenu. Hili ni jambo kubwa, ni jambo la kufurahisha na ni jambo ambalo sisi wawakilishi pia tunatakiwa tuliunge mkono, kama alivyosema Mhe. Mwenyekiti wa Wenyeviti pale, kwamba sisi wawakilishi pamoja na kuwa tunasema lakini pia tunao uwezo au tuna wajibu wa kumshauri Mhe. Waziri njia gani ya kuweza kupita, ili akaongeza zaidi hayo mapato.

Mhe. Mwenyekiti, nina ushauri wangu mmoja ambao naona huo kama tukiutumia utaweza kuendelea kutusaidia. Serikali kipindi kilichopita kwenye bajeti ile walikuwa na mpango wa kununua mashine za elektroniki, kwa ajili ya kutolea risiti kwa wafanyabiashara wetu.

Mhe. Mwenyekiti, wengi tunafahamu jinsi ya wafanyabiashara, siku zote mfanyabiashara ni mtu aliyekuwa anapendelea kupata yeye zaidi faida na ndio maana ya biashara. Maana ya biashara na lengo la biashara ni kufanya ili na wewe ukapata faida, biashara halali ambayo haina tatizo. Lakini pamoja na uhalali huo kuna kodi ambayo inatakiwa ilipwe kwa ajili ya maslahi ya wananchi wa nchi hii. Sasa naomba kumuuliza Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango kupitia kwako Mhe. Mwenyekiti, huu mpango wa kununua hizi *EFD machines* vipi upo au umepotea kabisa? Kama umepotea kwa nini umepotea, na kama upo kwa nini hatuufanyi, ili tukaongeza mapato yetu.

Mhe. Mwenyekiti, wafanyabiashara nachukua ile historia ya kule Tanzania Bara, Rais John Pombe Magufuli yeye alisisitiza ununuzi na uuzaji wa kila kitu kutumia hizi *EFD machines* ambao umeleta manufaa makubwa.

Lakini si hilo tu nilipendekeza kuwepo kwa faini za moja kwa moja kwa watu watakaotumia vibaya au wanaofanya makosa ya

barabarani. Mhe. Mwenyekiti, suala hili ni jambo ambalo nililisikia kwa upande wa Tanzania Bara linaleta faida kubwa, na pia ukiachilia mbali kuleta faida, lakini pia linapunguza athari ya ajali za barabarani, kwa sababu mtu anajua kwamba mimi nitakapofanya kosa ninapigwa faini pale pale na pesa zinaingia kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali. Naomba sana Mhe. Mwenyekiti, suala hili ambalo nimeomba ya kuwepo kwa hizi mashine za kielektroniki za kutolea risiti na kuwepo ka faini za papo kwa papo hili shauri naona ni vyema likazingatiwa.

Mhe. Mwenyekiti, vile vile wenzangu wamezungumzia juu ya uwekezaji na usimamizi wa mali za umma. Mhe. Mwenyekiti, naomba kufahamu tukiachilia mbali *ZANTEL* ni makampuni mangapi ambayo serikali kwa hapa Zanzibar yana *shares* zake. Nilitaka niyajue na vipi malipo yao au hisa zao zinavyopatikana na faida serikali inayoipata kwa hayo makampuni mengine ukiachilia mbali *ZANTEL*.

Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu pale serikali inatoa pesa zake kwenye makampuni hayo, ni vyema tukaweza kufahamu na kujua ni makampuni gani na ni kiasi gani cha fedha, ambazo wanatakiwa walipe katika faida na vipi utoaji wao wanaziwasilisha kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali.

Mhe. Mwenyekiti, pia kwenye Mashirika na Makampuni Binafsi vipi ulipaji wao wa mapato je unaendana na kile wanachokichuma, kwa sababu nina wasi wasi wa kufanyika kwa ujanja. Kwa hiyo, namuomba sana Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango kupitia kwako Mhe. Mwenyekiti, suala la makampuni pamoja na wawekezaji wafuatiliwe vyema mitaji yao na wajue uhalisia wa mitaji na biashara wanazozifanya, ili kuweza kujua uhalisia wa kodi wanayohitajika kulipa na vipi wanalipa, kwa

sababu bila ya kuwasimamia vizuri nina wasi wasi kwamba kodi za serikali zinaweza zikapotea.

Mhe. Mwenyekiti, lakini pia wenzangu Mhe. Mwenyekiti wa Wenyeviti alizungumzia maeneo ya uwekezaji. Mhe. Mwenyekiti, maeneo ya uwekezaji sio siri serikali tunapoteza mapato makubwa sana kwenye maeneo ya uwekezaji, wawekezaji wengi wamepewa *lease* lakini maeneo yale hawayaendelezi, wakati wangeendeleza maeneo yale wangeweza kuongeza kipato watu wetu wakaweza kupata ajira, wangelipwa mishahara, Mfuko wa *ZSSF* ungetanuka ukawa mkubwa wakaweza kwenye *ZSSF* na mambo mengi serikali ingepata kodi kutoka huko. Lakini sio siri Mhe. Mwenyekiti kwamba wawekezaji au watu wengi waliopewa maeneo ya fukwe hawayaendelezi.

Mhe. Mwenyekiti, na mimi naungana na Mhe. Hamza Hassan Juma kwamba wale wote, ambao wamepewa maeneo kwa ajili ya uwekezaji wakashindwa kuyaekeza wafutiwe, hakuna sababu ya kuendelea kuwaachia maeneo wakayatumia bure au wakayaweka bure ikawa serikali haina faida yoyote. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, jambo hili linaniumiza sana kuona kwamba kuna maeneo mengi ukienda katika Jimbo langu la Konde eneo la Makangale sijui viwanja vingapi vimepimwa, watu wangapi wamepewa *lease*. Lakini ukienda kuna hoteli tano zaidi ya viwanja 100 vimepewa, watu wamepewa *lease*, ukienda maeneo ya Kusini Wambaa huko na kwengine, yaani maeneo tofauti wawekezaji wamepewa *lease* lakini maeneo hawayaendelezi. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, namuomba Mhe. Mwanasheria Mkuu kwamba turekebisheni sheria, kama sheria ina mapungufu wale wote ambao tumewapa maeneo ambayo hawayaendelezi, basi tuweze

kuwanyang'anya tuwape watu wengine ambao wana nia thabiti ya kuendeleza, ili serikali ipate mapato. Mhe. Mwenyekiti, lengo letu hatukuwapa ardhi zile kwa ajili kwenda kufanya maonesho au kama ulivyosema kuna baadhi yao wanakuja kufanya biashara wanapewa maeneo yale kwa bei ndogo wanayolipia ikisha wao wanaingiza kwenye *internet* wanauza, hii itakuwa haitusaidii kitu.

Kwa hiyo, Mhe. Mwenyekiti najua kwamba kuna watu hapa ukisema hivi wanaumia, lakini mimi siumii. Mhe. Mwenyekiti, narudia tena kuna maeneo mengi narudia tena kusema kuanzia Kusini, Mashariki, Wambaa, Ndagoni, Vitongoji, Mtambwe, Konde maeneo mengi yako Pemba ambayo wamepewa lakini ukizihesabu hoteli sijui ziko ngapi.

Nadhani Mhe. Waziri wa Habari, Utalii Utamaduni, na Michezo atakuwa anajua, lakini nilisahau kumuuliza kwa Pemba kuna hoteli ngapi ambazo zinafanya kazi. Vile vile maeneo mangapi ambayo wamepewa watu wa uwekezaji. Mhe. Mwenyekiti, tunapoteza mapato makubwa na jambo hili naomba sana kwamba serikali itizame na ilichukulie hatua mara moja.

Mhe. Mwenyekiti, pia Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango jana kwenye swali langu wakati alipokuwa akinijibu alinifurahisha aliponiambia, kwamba anaanza kukusanya kodi au kuwasiliji wafanyabiashara kwenye hiyo *block*, kwa maana kila mtu anakaa kwenye *zone* yake kuwajua. Sasa bado sijaridhika na naona kwamba bado kuna wafanyabiashara wengi ambao wanaendelea kufanya biashara bila ya kutoa risiti.

Mhe. Mwenyekiti, naomba itengenezwe sheria japo ya kuajiri wale wakusanyaji kwa muda, ili wawekwe mle waweze kusimamia vizuri makusanyo na kuhakikisha kwamba wafanyabiashara hawa kila mmoja analipa kodi na anatoa risiti.

Mhe. Mwenyekiti, tunapotoa risiti ina maana unapata kulipa kodi ya serikali, ukilipa kodi ya serikali uchumi unakua.

Mhe. Mwenyekiti, Wizara ya Fedha na Mipango ina mambo mengi, leo nilitaka niulize swali moja ambalo pia linaniuma. Nilitaka nijue hasa mahitaji ya matumizi ya mafuta kwa hapa Zanzibar kwa mwaka na uletaji wake tunapokea kiasi gani, tani ngapi za mafuta tunazipokea au lita ngapi za mafuta tunazipokea. Vile vile kodi au tozo ambayo inakatwa je inalingana na uhalisia wa mafuta yanayoletwa hapa nchini.

Pia naomba kujua kwa mwaka huu wa fedha kupitia hii biashara ya mafuta kwa wanaoleta mafuta, wameilipa serikali kiasi gani ya kodi, kwa sababu kuna asilimia tozo ile tunayolipa kila tunaponunua mafuta sisi tunalipa. Kwa kweli kama alivyosema Mhe. Hamza Hassan Juma kwamba yeye anapendekeza kuwa iongezwe na mimi nakubali kwa sababu tuna mahitaji mengi, na ile ni moja katika njia tunayopatia, kwa sababu shilingi moja moja au senti hamsini, au shilingi mia na hamsini kwenye lita ya mafuta ni nyingi sana. Kwa hiyo, Mhe. Mwenyekiti wasi wasi wangu kwamba hakuna uwazi kwenye biashara ya mafuta, nina wasi wasi kidogo. Kwa maana hiyo, naomba kujua ni tani ngapi za mafuta na kiasi gani cha fedha kinakusanywa cha kodi kupitia hii biashara ya mafuta.

Mhe. Mwenyekiti, nikitoka hapo nakwenda kwenye Mfuko wa Hifadhi ya Jamii. Mfuko wa Hifadhi ya Jamii ni kimbilio la wanyonge mtu akishamaliza kustaafu anategemea apate kitu kimsaidie kwenye maisha yake, kwa sababu anakuwa tayari muda wake wa kazi umekwisha. Kwanza nawapongeza kwa kazi nzuri wanazozifanya, lakini pia Mhe. Mwenyekiti namuomba Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango kupitia *ZSSF* kwamba watanue

wigo wa kibiashara wasiende tu kwenye upande mmoja au wa majengo tumeona kama wanataka kununua meli.

Lakini hiyo meli wanayotaka kununua basi napendekeza kama wanao uwezo wanunue moja, mbili, hata ziwepo meli za *ZSSF* au maboti kama yale ya abiria kwa sababu ya kutanua wigo wa kibiashara. Jambo hili litasaidia sana kwa sababu ni kitu kinachotumika kila siku, au ifungue benki ambayo itaweza kukopesha au kufanya biashara kama serikai imeona mtaji wake ni mdogo iwaongezee mtaji, ili waweze kutanua biashara zao.

Mhe. Mwenyekiti, sina wasi wasi na hili isipokuwa wasi wasi wangu ni kitu kimoja ambapo tayari nimejibiwa, lakini bado nina wasi wasi nacho narudia kulizungumzia tena. Mhe. Mwenyekiti ni kwamba baadhi ya waajiri wana tabia ya kutokuwasilisha michango ya wafanyakazi wao. Mhe. Mwenyekiti, naomba sana *ZSSF* kwa sababu wanazo *data*, wanacho kila kitu ofisini kwao wasisubiri kwamba watu wawafuate wao, hapana. Hivyo, ni vyema waanze kuyafuatilia makampuni yote kwa undani, ili wajue uhalisia wa wafanyakazi wangapi na uhalisia wa mishahara, waifatilie ikiwezekana hata mabenki kuweza kujua uhalisia wa mishahara ya wale wafanyakazi, kwa sababu bado ni wasi wasi kwamba wengi wanadangaya.

Mhe. Mwenyekiti, naona unaniangalia kidogo lakini nakuomba unipe dakika tano.

Mhe. Mwenyekiti, mambo kama haya ni kilio kwa watu wetu na *ZSSF* kama nilivyosema ndio kimbilio. Kwa hiyo, wafanye bidii kubwa kuhusu kusimamia michango ya wafanyakazi, michango ya wafanyakazi hawa ni haki yao si haki ya waajiri ambao wana makampuni binafsi, wao lengo lao ni kujinufaisha tu.

Mhe. Mwenyekiti, sasa nije kwenye *PBZ*…

**Mhe. Mwenyekiti:** Mhe. Mjumbe naomba umalizie…

**Mhe. Omar Seif Abeid:** Mhe. Mwenyekiti, nakuomba dakika mbili au tatu kwa hisani na heshima kubwa nakuomba.

**Mhe. Mwenyekiti:** Mhe. Mjumbe, ndio maana nikamwambia nakuomba umalizie kwa dakika mbili. *(Makofi)*

**Mhe. Omar Seif Abeid:** Mhe. Mwenyekiti, haya ahsante.

Mhe. Mwenyekiti, *PBZ* ni benki yetu, ni benki yetu wazalendo, Benki ya Watu wa Zanzibar ambayo inapendwa sana na sote tunaifurahia. Mimi binafsi nafurahia na ni ukweli usiofichika kwamba ndio mkombozi wetu, yaani ni benki yetu, ndio ukombozi wetu. Lakini Mhe. Mwenyekiti, kuna tatizo moja au mawili kidogo, kwanza ni msongamano.

Mhe. Mwenyekiti, inapofika mwisho wa mwenzi msongamano *PBZ* unakuwa ni mkubwa, watu wanapata shida. Sasa Mhe. Mwenyekiti, namuomba sana Meneja Mkuu na Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango nauomba alisimamie ikiwa kuna uwezekano wa kufungua matawi mengine yafunguliwe, ili tupunguze msongamano wa watu. Msongamano wa watu umekuwa ni mkubwa Mhe. Suleiman Makame Ali yeye alizungumzia kuhusu kuweka *ATM*, *ATM* tumesema kwamba zipo na zinasaidia *ATM*, na ni vyema *ATM* zikaongezwa maeneo mbali mbali, lakini hata matawi kufungua matawi ni bora.

Na mwisho Mhe. Mwenyekiti, naomba sana *PBZ* waangalie jinsi wao wanavyowakopesha wafanyakazi wa serikali na makato, kama inawezekana wawapunguzie kidogo riba wafanyakazi wetu

ni masikini wengi ni wa kima cha chini, wapunguziwe kidogo riba wanayokatwa. *(Makofi)*

Baada ya hapa Mhe. Mwenyekiti, kwa heshima natamka kwamba naiunga mkono hotuba hii kwa asilimia mia, na nawaomba wenzangu tuiungeni mkono hotuba hii tumpitishie Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango bajeti yake, ili aweze kutekeleza malengo yake. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti. (*Makofi*)

**Mhe. Mwenyekiti:** Ahsante sana Mhe. Omar Seif Abeid kwa mchango wako sasa naomba nimwite Mhe. Hussein Ibrahim Makungu akifuatiwa na Mhe. Mohamed Said Mohamed na Mhe. Panya Ali Abdalla ajitayarishe.

**Mhe. Hussein Ibrahim Makungu:** Ahsante Mhe. Mwenyekiti, na mimi kunipa nafasi. Awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu mchana huu kufika hapa kujadili bajeti hii muhimu sana katika nchi yetu.

Lakini nikushukuru sana Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi hii kuchangia hotuba hii ya Mhe. Waziri wetu wa Fedha na Mipango, ambaye ni mpenda kabisa kwa juhudi zake kubwa pamoja na watendaji wake wote kwa kazi nzuri wanayoifanya. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, hii wizara ina kazi kubwa. Kwa kweli, wanafanya kazi bila ya wao Mhe. Mwenyekiti hawa wenzetu, basi hatuwezi kufanya maendeleo yoyote ukiangalia barabara zetu, elimu, afya, maji tunahitaji kutoka kwao. Mhe. Mwenyekiti, ninawapongeza, nawashukuru na Mwenyezi Mungu awazidishie sana umahiri wao wa kufanya kazi.

Mhe. Mwenyekiti, nianze mchango wako kwenye ukurasa huu wa 26 kifungu namba 44 katika Benki ya Watu wa Zanzibar *PBZ*.

Mhe. Mwenyekiti, ninaipongeze sana benki yetu na niseme ninawapongeza kwa kazi yao kubwa na kwenye kitabu chao wameandika mafanikio wamepata karibu faida wametengeneza faida karibu bilioni kumi na nane *point* sabini nne (bilioni 18.74). Kwa kweli, hii jambo zuri na la kuwapigia mfano na tuwape moyo benki yetu hii waweze kuendelea kufanya kazi vizuri katika nchi yetu. *(Makofi)*

Vile vile, niipongeze *PBZ* Mhe. Mwenyekiti kwa kutoa mikopo wa wananchi au raia wetu wafanyabishara au masikini kwa njia mbali mbali kuwainua, wametoa mikopo karibu bilioni tisini na mbili *point* sitini na nne (bilioni 92.64). Hili jambo ni la kupigiwa mfano Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu bila ya kupewa mkopo huwezi kuendelea hasa wafanyabiashara wadogo wadogo.

Mhe. Mwenyekiti, naomba kutoa ushauri juzi katika Bajeti ya Wizara ya Afya hapa tumeona, Mhe. Waziri alisema wamepelekwa wataalamu kusoma nje karibu wataalamu wengi wanafika hamsini au zaidi kusoma fani mbali mbali za udaktari. Lakini, Mhe. Mwenyekiti hawa madaktari wanapokuja hapa wanapoajiriwa kazi pale Hospitali ya Mnazi Mmoja kututibu sisi, nadhani bila ya wao nasema hata kuishi itakuwa ni mtihani kwa sababu wataalamu wa afya ni muhimu sana.

Sasa, wanapokuja hapa kufanya kazi Mhe. Mwenyekiti naomba kupitia benki serikali iwaangalie, Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango awape upendeleo fulani wa kuwakopeshe nyumba, gari madaktari hawa, ili waweze kukaa. Mhe. Mwenyekiti, tumeona madaktari wetu wengi wakimaliza kusoma nje, serikali inawasomesha miaka saba au mitano wakija hapa baada ya muda mfupi wanakwenda Tanzania Bara kufanyakazi kwa ajili ya maslahi.

Mhe. Mwenyekiti, naomba sana Mhe. Waziri awaangalie hawa madaktari wetu wakishakuja na fani mbali mbali ya matibabu tuwakopesha gari japo moja, nyumba japo ndogo, ili wawafunge wasiweze kuondoka na walipe kwa mishahara yao. Mhe. Mwenyekiti, nitoe mfano mmoja siku moja nilikuwa na mgonjwa anataka kutiwa ile dawa nusu kaputi, ili apate kulala afanyiwe *operation* basi daktari akawa yupo Bububu kule jimboni kwangu kipindi kile, basi yule daktari hana hata usafiri Mhe. Mwenyekiti na daktari muhimu, ikabidi nikamwambie nenda pale KMKM pale Jimboni kwangu uchukuwe *ambulance* uje mara moja hapa.

Kwa kweli, daktari yule akenda lakini mimi mwenyewe nilikuwa na huruma sana. Kwa hiyo, daktari kama huyu anahitaji kunusuru maisha binaadamu mwengine yeye hana hata usafiri. Kwa hiyo, Mhe. Mwenyekiti naomba hawa watu wakopeshwe kwa sababu wanakuwa hawana vigezo vya kuweka nyumba rahani au kitu chochote. Mhe. Mwenyekiti, serikali kupitia Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango iwaangalie iwakopeshe nyumba za bei nafuu na gari, ili waweze kututumikia vizuri. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, Benki yetu ya *PBZ* pamoja na kwamba Waheshimiwa Wajumbe wamesema, lakini nataka niseme jambo moja ambalo kidogo benki yetu inakuwa inazidiwa hasa kwa wakati ule mwa mwisho wa mwezi inakuwa foleni kubwa na wananchi wanapata tabu kupata fedha zao, lakini katika kitabu chao nimekiona Mhe. Mwenyekiti, wananzisha kuweka *ATM* nyingi sana katika maeneo mbali mbali, hilo litasaidia sana. Hivyo, ninawapongeza ndugu zetu wa *PBZ* waendelee kufanya hivyo, kwa ajili ya kuondosha msongamano pale kwa ile benki wakati wa mwisho mwezi kwa masuala ya mishahara.

Mhe. Mwenyekiti, ninawashukuru sana sisi kama Waheshimiwa tukienda pale *PBZ* kwa kweli, tunapata heshima kubwa

tunapokewa vizuri, ninawapongeza kwa juhudi zao hizo. Ukienda Dar-es-Salam Kariakoo mara nyingi nakwenda pale nikifika tu na kazi nzuri wanayoifanya hata wafanyakazi wao wanaowaweka pale kutoka Zanzibar, yaani ukifika tu wanakujua Mheshimiwa njoo ingia hapa fanya hivi, unapata faraja kubwa, unajisikia raha sana. Kwa hiyo, Mhe. Mwenyekiti naomba waongeze juhudi hizo kuwatambua Waheshimiwa na kuwapa *facility* nzuri na kazi nzuri hizo za benki. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea na mchango wangu katika hotuba hii. Kwanza nimpongeze sana Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kazi kubwa aliyoifanya. Lakini jambo moja niseme aliahidi Mhe. Rais wa Zanzibar katika kampenzi zetu juzi 2015 mwaka juzi hapa aliahidi kama ataongeza mshahara asilimia mia kwa wafanyakazi wetu wa serikali, na suala hili kalitekeleza juzi na tumeona wafanyakazi wameanza kulipwa fedha zao waliahidiwa na Mhe. Rais wa Zanzibar katika kampeni. *(Makofi)*

Vile vile, Mhe. Rais wa Zanzibar pia aliahidi kutoa pencheni kwa wazee waliofikia miaka 70 na kazi hiyo inafanyika Mhe. Mwenyekiti. Kwa hivyo, nampongeza sana Mhe. Rais wa Zanzibar kwa nia njema ambayo anayo kwa taifa hili la Zanzibar. Lakini pamoja na yote niseme kwamba Mhe. Mwenyekiti bila Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango mambo haya yote hayatekelezeki kama vile huu mshahara ulioongezwa basi wafanyakazi wetu hawawezi, hawa wazee wetu pencheni hawawezi kupata. Sasa yote naomba nimpongeze Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango kwa juhudi zake pamoja na Mhe. Rais wa Zanzibar kwa kuliona hili la kuona wananchi wenzetu kuweza kuwasaidia.

Mhe. Mwenyekiti, huu mfano wa kutoa pencheni kwa kweli naomba nimpongeze sana Mhe. Rais wa Zanzibar, yaani nchi zilizoendelea ndio zinatoa pencheni kama hizi, kwa mfano ukiangalia kama Canada na nchi nyengine zilizoendelea ndizo zinazotoa pencheni. Lakini katika nchi za Afrika sijaona kuwa wazee wanapewa pencheni. Kwa hivyo, nimpongeze Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyezi Mungu amzidishie hekma na busara kuweza kuwasaidia wazee hawa. Mhe. Mwenyekiti, kodi ikiongezeka basi naomba pia hawa wazee wetu pia tuwaongezee fedha ipande angalau wafike elfu hamsini kwa mwezi basi itakuwa ni jambo la faraja sana. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, niendelee katika ukurasa wa 5 kifungu 12 katika Sekta hii ya Utalii. Mhe. Mwenyekiti, katika sekta hii niipongeze sana hasa katika sehemu ya kukusanya kodi, ukusanyaji wa mapato vianzio vyetu. Mhe. Mwenyekiti, niwapongeze sana katika ukurasa huu wa 12 wamesema *ZRB* na *TRA* kwa miezi tisa tu Mhe. Mwenyekiti, wameweza kukusanya bilioni mia nne arubaini na nane ponti kumi na tano sawa na asilimia hamsini na tatu (bilioni 448.15).

Mhe. Mwenyekiti, nimepiga hesabu hapa haraka haraka Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango pamoja na watendaji wake kwa kukusanya fedha *TRA* na *ZRB*, yaani nawapongeza sana kwa dhati na Mwenyezi Mungu shahidi awazidishie moyo huo. Kwa kweli, nimepiga hesabu haraka haraka tu hapa Mhe. Mwenyekiti, nimeona tunakusanya kodi Zanzibar kwa mwezi karibu bilioni hamsini tunafikia karibu. Kwa hivyo, jambo hili la kujipigia mfano sana bilioni hamsini sio fedha kidogo kwa mwezi. *(Makofi)*

Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango kupitia kwako Mhe. Mwenyekiti, ajitahidi sana na hawa vijana wetu wanaofanyakazi ukiangalia kama huyu Kamishna wetu wa

*ZRB* Amour anafanyakazi kubwa kwa uzalendo mkubwa, ukiangalia pia huyu Mcha Naibu Kamishna anafanyakazi kwa imani kubwa ya nchi yetu. Lakini, Mhe. Mwenyekiti hawa watu wanafanyakazi ni kama rafiki kwa walipa kodi, nawapongeza sana na wala hawawanyanyasi au kuwaonea, yaani wanafanya kama urafiki na wanawaelimisha, kwa sababu mlipa kodi maisha umuelimishe uwe rafiki yako ujenge naye kila kitu mnawasiliana. Kwa hiyo, wanakuwa wanafurahi walipa kodi na wanalipa kodi. Kwa hivyo, nawapongeza sana imani hiyo wanayo na wanafanya kazi hiyo kwa urafiki na walipa kodi.

Vile vile, Mhe. Mwenyekiti hawa watendaji wanafanya kazi kubwa wanakwenda kwenye sehemu za biashara kufatilia, kwa sababu mlipa kodi kama hujamfatilia Mhe. Mwenyekiti halipi kodi kwa hiari bado muamko wao ni mdogo walionao. Kwa hivyo, hawa wafanyakazi wetu wa *ZRB* na *TRA* wanafanya kazi wanakwenda na vijana wetu wadogo ukitizama lakini wana uzalendo.

Sasa Mhe. Mwenyekiti hawa mpaka wanajenga uadui wakati mwengine na wafanyabiashara, kwa sababu vile wanawaambia lipa kodi anakuwa hayuko sawa na wale watu waliomzunguka au jamii wakati mwengine. Kwa hiyo, naomba sana Mhe. Mwenyekiti tuangalie hawa *staffs* wetu wanafanya kazi kubwa katika kukusanya haya mapato.

Mhe. Mwenyekiti kuna siku ya sherehe ya Siku ya Mlipa Kodi. Mhe. Mwenyekiti, nilisikia kwenye vyombo vya habari lakini sina uhakika, nilisikia kitu kama hicho, kama aliwaahidi hawa watendaji wetu kama atawapa asilimia 5 kwa makusanyo watakayotapata *ZRB* na *TRA*. Sasa sijui hili Mhe. Mwenyekiti kama Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango anawapatia hawa ndugu zetu wafanyakazi hawa *ZRB* na *TRA* hii asilimia 5.

Kwa kweli, kama nilivyosema wanafanya kazi kubwa bila ya wao hizi fedha hatuwezi kukusanya, kwa sababu wanapokwenda kwa wafanyabiashara Mhe. Mwenyekiti wakapewa rushwa akaambiwa chukua hichi usiandike chochote hapa niache mimi wanaweza wakapewa hivyo. Lakini wakipewa asilimia fulani ile posho wale wanajisikia vizuri wanajisikia imani na wanafanya kazi kwa bidii. Kwa hivyo, naomba hii asilimia 5 Mhe. Mweyekiti sijui ikoje kama wanapata hawa ndugu zetu wa *ZRB* na *TRA*. Lakini kama wanapata, basi nitafurahi ili wapate kuongeza bidii na muamko wa kazi, ili waweze kukusanya kodi vizuri sana.

Mhe. Mwenyekiti, niende kwenye mpango wetu wa serikali haya mambo ya kodi. Serikali inatoa *exemption* Mhe. Mwenyekiti, hasa ukiangalia mwezi huu wa Ramadhani inatoa *exemption* ya tende, mchele, unga na sukari. Kwa kweli, naipongeza sana serikali kwa nia njema na Mwenyezi Mungu anatusaidia kwa sababu mwezi huu ni mwezi mkubwa sana sisi Waislamu tunafanya ibada saa zote na tunafunga. Kwa hivyo, na wananchi wetu wengine masikini wanyonge, tunaweza kuwasaidia kwa hali hii ya kutoa *exemption* tende, mchele na *exemption* hii ninavyoijua mimi sijui Mhe. Mwenyekiti kwa mtazamo wako ni *zero duty* ya *text*, kwa hivyo unakuwa hulipi ushuru kama kontena za tende, mchele, unga.

Sasa hawa wafanyabiashara Mhe. Mwenyekiti tufuatilie hapa nalo, hii tende sasa hivi ukitizama bei yake juu inauzwa karibu elfu thalathini na zaidi na wananchi wanashindwa kununua. Kwa hiyo, ushuru mtu hajalipa, ukitizama Arabuni tende kontena nzima inafika milioni saba, milioni nane inafika kontena ya tende. Lakini hapa inauzwa tende bei ghali. Kutokana na hali hiyo, tuwafuatilie wafanyabiashara je wanafanya kweli kwa nia njema kodi yetu hawatoi halafu wanawauzia watu kwa bei kubwa

wanapa faida mara mbili. Kwa hivyo, tufatilie madukani kama hii kazi inafanyika kwa sababu ukiangalia mchele, sukari, unga sasa hivi bei juu hawa wananchi wanashindwa kununua Mhe. Mwenyekiti na hii kodi yetu wanachukuwa.

Kwa hivyo, naomba sana tufatilie suala hili madukani kuangalia bei wanavyouza ni kweli na juu tukitizama na bei ya huko Warabuni tende wanavyonunua ni sawa. Sasa kama wanasamehewa ushuru ili wapate faida wao watie faida ndogo walipe *freight* za kontena lakini ushuru hawana. Nafikiri ni vyema tuangalie Mhe. Mwenyekiti vipi kazi wanavyofanya katika maduka.

Mhe. Mwenyekiti, hapa ukiangalia mtu analete meli mbili anatumia fursa hii kuleta *exemption* ya mchele, unga meli mbili, sasa huu mchele hata sifahamu unauzwa bei za ajabu. Kwa hivyo, tuangalie Mhe. Mwenyekiti kuna mtu anaweza kuuza mchele miaka miwili dukani kwake usimalize. Kutokana na hali hiyo, Mhe. Mwenyekiti namuomba Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango aliangalie pamoja na kulifuatilia suala hilo.

Lakini Mhe. Mwenyekiti, nije kwenye maandalizi ya kuanzisha mfumo utozaji wa kodi katika *electronic*. Kwa kweli, hili jambo zuri sana na ninampongeza Mhe. Waziri katika kitabu chake ameandika nimekisoma jana usiku vizuri sana nimeona suala hili, hasa hii katika *electronic E-tax,* hii wanatumia dunia nzima Mhe. Mwenyekiti, niliwahi kwenda China kipindi fulani lakini nitaeleza baadaye. Hivi sasa hii *E-tax* ndio inafanya kila kitu kuhusu masuala ya kodi kwenye *E-tax.* Sasa tukiangalia kodi hii ya *E-tax* itatusaidia sana Mhe. Mwenyekiti na sijui Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango ameipanga vipi, lakini naomba aifuatilie zaidi.

Mhe. Mwenyekiti, ukiangalia wageni wetu wanaokuja kutoka nje sasa hivi hasa kama *charter* kubwa kubwa *flight* zinakuja asubuhi ndege tatu ndege nne. Kwa kweli ninaona ajabu sifahamu kwa sababu watalii wengi wanashuka na watalii wale wa hadhi ya juu, yaani wanalipa fedha nyingi sana na wala hawalipi pesa ndogo ndogo, sasa wanakwenda katika hoteli gani, hiyo haijulikani.

Sasa wanapokwenda kwenye hoteli hizo Mhe. Mwenyekiti, kuna asilimia 18 ya *VAT* walipe kama chumba dola eflu mbili walipe asilimia 18 karibu dola mia nne au zaidi. Lakini ukitizama kuna wengine kodi wana *9 dollars* karibu ya hizo hoteli ndogo ndogo. Mhe. Mwenyekiti, hizi *charter flight* tuangalie sana hawa wageni wanapokwenda huko wanalipa kodi kwa mujibu wa chumba au wanalipa kodi kwa mujibu wa hii *9 dollars* kwa *person*. Sasa tuangalie hawa wageni walipe *VAT* kama chumba kuna vyumba hapa Zanzibar vinafika dola elfu mbili, elfu tatu kwa usiku mmoja. Kwa hiyo, ukitizama chumba dola elfu mbili, elfu tatu ushuru wake au asilimia 18 dola mia sita kwa mgeni mmoja.

Sasa tuangalie hawa wageni tuwafatilie hili *E-text* itatusaidia, lakini tuangalie pale pia kuanzia sasa tuko *local*, lakini tuangalie wageni wanaofika pale tujue wanakwenda kufikia hoteli gani kama ile *charter* moja inakuwa na wageni mia tatu mia nne wanakwenda mfano Kiwengwa au wapi tufatilie Mhe. Mwenyekiti.

Kwa mfano, Mhe. Mwenyekiti kuna kipindi nampongeza sana Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango wakati nilipokuwa natoka Dodoma kwenye Bunge nikafika pale nikaona watu wa *ZRB* wametanda pale *Airport* nikaona Daah! Leo kuna nini hapa, lakini nikafuatilia pale nikaona wanafuatilia hawa wageni wanakwenda wapi, mahoteli gani. Kwa hivyo, tuangalie hizi *charter flight* tangu zinapotoka Mhe. Mwenyekiti huko wanapotoka kwenye

*tour operators* wao, kwa sababu wale hawalipi hapa wale wanalipa *full board* kula, kulala, *transport* yaani, kila kitu wanalipa kule.

Kwa hivyo, tufuatilie *tour operators* walioko kule hawa ndugu zetu wa *ZRB* pia waende kule wakafuatilie kama wanavyotoka hapa wafanyabiashara *tour operators* kwenda kufuatilia wageni na sisi tutoke hapa sasa twende tukafuatilie wageni wetu wanaokuja Zanzibar kupitia *tour* gani na wanalipa kiasi gani hawa wageni, kwa sababu hawa wafanyabiashara pengine wanatudanganya inawezekana kuwa mgeni dola mia analipishwa kumbe ni dola elfu tatu kule au dola elfu mbili kule.

Mhe. Mwenyekiti, ni vyema tuangalie hizi kodi zinavyolipwa kwa wageni hawa. Lakini, sasa hivi tuangalie Mhe. Mwenyekiti inapokuja ndege ile watu wa *ZRB* wakae pale *airport* watizame mgeni huyu anakwenda hoteli gani na hoteli anayokwenda chumba bei gani kwa muda huu kwanza kabla haijaanza hii *E-tax* tufuatilie hii kodi Mhe. Mwenyekiti tuna shida nyingi katika majimbo yetu tuna shida ya maji, elimu, afya sasa hizi fedha ndio Mwenyezi Mungu katupa neema yetu hii. Leo watu wadogo kawa wanakuja wawekezaji wanatuibia kodi yetu. Kwa hiyo, mimi naomba sana tufatilie kuanzia sasa wageni wanaoshuka wanakwenda wapi, hoteli kiasi gani na chumba kiasi gani ili tupate ile kodi halali kabisa.

Mhe. Mwenyekiti, niendelee katika ukurasa wa 24, kukalisha uwekezaji wa miradi 13 yenye thamani ya dola za Kimarekani mia moja thalathini na mbili *point*...

**Mhe. Mwenyekiti:** Mhe. Mjumbe, kabla hujaendelea naomba nimpishe Mwenyekiti, aendelee na huu mjadala.

*Hapa Mhe. Mwenyekiti (Shehe Hamad Mattar) alikalia kiti*

**Mhe. Mwenyekiti:** Mhe. Hussein Ibrahim Makungu endelea.

**Mhe. Hussein Ibrahim Makungu:** Ahsante Mhe. Mwenyekiti, naendelea kwenye ukurasa wa 24.

"Kukamilishwa uwekezaji wa miradi 13 thamani ya U$ 132.38 milioni".

Mhe. Mwenyekiti, hili jambo zuri sana na wawekeji wana imani kuja kuekeza hapa kwa sababu tumeona kwenye kitabu cha Mhe. Waziri hapa hizi dola za kimarekani 132 wawekezaji wanakuja kuekeza hapa. Lakini hapa ukiangalia uwekezaji huu pia utatoa ajira kwa wananchi wetu 625 wameandika kwenye kitabu cha Mhe. Waziri.

Hili jambo la kupigia mfano na jambo zuri sana na tukiangalia uwekezaji huu sana unakwenda kwenye mahoteli na kwenye mikahawa ya kitalii. Kwa hivyo, niwapongeze sana Mhe. Waziri jitihada kubwa aliyoifanya na Mhe. Rais wetu, kwa sababu bila ya wawekezaji kuwa nao karibu kuwaonesha imani ya nchi hii amani iliyokuwepo nchi hii maendeleo hawa waekezaji watakuwa hawaji hapa. Lakini kama tunashirikiana nao vizuri basi wawekezaji watakuja kuekeza na sisi tutapata ajira Mhe. Mwenyekiti, shida kubwa ni ajira na kipato nchi hii tupata kuongeza na sekta hii ya utalii ni uti wa mgongo kwenye nchi yetu. Kwa hiyo, nakupongeza Mhe. Waziri ajitahidi sana hawa wawekezaji awe karibu nao, ili kuwavutia kuwekeza wasiwe na ghofu mtu pesa kama hizi kutumia dola milioni 132 kwenye nchi hii kama hii Afrika inataka moyo mkubwa na uzalendo.

Tukiangalia mfano mzuri hapa mfanyabiashara wetu maarufu kabisa Said Bakhresa anawekeza kule karibu milioni 40 kule Fumba pale, Mtoni Marine karibu dola sijui milioni ngapi jambo la woga mimi ningekuwa mimi ningelikuwa naogopa ningesema labda kuna moja mbili. Lakini ukiwapa moyo wafanyabiashara Mhe. Mwenyekiti wanakuwa wanapata moyo wakuwa hawana wasi wasi wanajua fedha zao zitarudi na faida juu. Kwa hivyo, nampongeza Mhe. Waziri aendele kuwa nayo karibu sekta hii utalii tuweze kupiga hatua kubwa katika nchi yetu hii ya Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, nije katika ukurasa wa 14 usimamizi wa Mfuko wa Miundominu. Wizara ya Fedha na Mipango imekusanya bilioni 20. Mhe. Mwenyekiti, hili jambo zuri sana katika usimamizi wa mfuko wa miundombinu hili jambo ni muhimu miundombinu yetu ukitizama sasa hivi mibaya tena sana hasa huu Mfuko wa Barabara umekusanya amekusanjya yeye kwa uadilifu wake na kuipa serikali ili  Wizara ya Mindombinu kufanyaka kazi zao.

Kwakweli, nampongeze sana na hizi fedha bilioni 20.95 amekusanya kwa muda wa miezi tisa tu. Ni jambo la kupigiwa mfano na Mwenyezi Mungu akuzidishie kazi yako mzuri uliofanya hiyo. Lakini Mhe. Mwenyekiti, tuangalie serikali na juzi nilisema mimi naomba sana hizi fedha tunapata bilioni 20 kwa barabara zetu angalau za ndani. Ukiangalia fedha hizi tunapata kwenye kodi lakini barabara zetu za ndani mbovu kama mimi barabara yangu ya Mwanyanya Mhe. Mwenyekiti, itengenezwe kwa sababu imetiwa kifusi mara mbili na serikali hii sasa hivi ni mara ya tatu itakuwa na sasa hivi juzi nimeenda jimboni naona aibu wapiga kura wetu wanatulaumu sana shimo linafika mimi naweza kuingia nusu kwenye shimo barabara imechimbika.

Leo Mhe. Waziri wa Mawasiliano nimemwambia nimemuomba japo gari moja mbili nitachangia mafuta wananchi wanalalamiko huko, wanasema hali kama hii mashimo kama haya mvua iliyokuja basi hata kifusi Mhe. Mwenyekiti. Kwahiyo, naomba Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango kupitia kwako Mhe. Mwenyekiti naomba niko chini ya miguu yake naomba anisaidie hii barabara angalau tuizibe mafusi utoe upendeleo kuanzia Kwahanzari huku Mwanyanya Jeshini unashuka mpaka huku Sharifumsa kwa Kisasi hapa. Kwakweli, ile njia mbaya Mhe. Mwenyekiti kuna wagonjwa, na mambo mbalimbali daladala sasa hivi kwenda haziendi kule ndani.

Kwahivyo, inakuwa shida kwa wananchi wetu wanakuwa hawafiki vizuri. Kwahiyo, naomba sana fedha hizo bilioni 20 tuangalie basi barabara hizi japo tutie kifusi kidogo Mheshimiwa nakuomba kwa serikali yetu sikivu naomba sana.

Pia tuangalie suala la maji Mhe. Mwenyekiti juzi nimesema Sharifumsa, Kibweni, Mwanyanya yenyewe kwenye chemchem Mtoni huku hakuna maji shida. Kwahivyo, naiomba sana serikali iangalie na huku miradi chungu nzima tumefanya, lakini maji kule hayaendi kwenye jimbo langu Mtoni pale Kibweni Sharifumusa hayaendi maji. Sasa hivi ukienda jimboni wananchi wanalalamika, keshokutwa uchaguzi bado miaka miwili tu hapa watatuhukumu hawa watu. Watatuambiya nyinyi mulisema mtaleta maji lakini matokeo yake hakuna, mpaka kwenye Ilani ya Chama cha Mapinduzi barabara ile imo. Kwahiyo, naomba sana Mhe. Waziri anisaidie kupitia kwako Mhe. Mwenyekiti japo uwekaji huu wa kifusi.

Mhe. Mwenyekiti, nije kwenye huu uwekaji wa hii *CCTV camera*. Nakupongeza sana mradi huu ni mzuri sana na mimi nilisema juzi kwenye Baraza, mimi nilikuwa ni mjumbe mmoja katika Baraza

hili na Mwenyezi Mungu kanijaalia pale nipo nilikwenda China kwenye mradi huu wa *CCTV camera*. Huu mradi Mhe. Mwenyekiti, dunia nzima wamefunga, lakini nchi zilizofunga zina fedha nyingi, kwa sababu mradi huu ni mkubwa sana. Nilipokwenda China kule kwa ajili ya kutizama miradi yote kule. Nilikwenda mimi na Waziri wa Fedha na Mipango wa zamani mstaafu, Mhe. Spika mstaafu, Katibu wa Baraza, Mhe. Abubakar Bakar Waziri wa Katiba na Sheria wakati ule tulikwenda, na mimi nilipata bahati ya kwenda kwenye mradi huu.

Kwahivyo, Mhe. Mwenyekiti, mradi huu tukiweza kuufanikisha basi hata watalii wataweza kuongezeka katika nchi yetu. Mradi huu hata uwe Marekani basi ukitaka kuona Zanzibar hali iko vipi basi utaijua kwa hizi *camera* zipo za teknolojia ya hali ya juu. Kwahivyo, namuomba Mhe. Waziri kwenye kitabu chake ameandika uendelee na mradi huu umalize, ili tupate kupata faida katika nchi yetu kwa kupitia *camera* hizi katika mambo ya ulinzi. Hapa umeandika karibu bilioni 14. Kwakweli, namuomba kazi nzuri na fedha hizi sio tatizo, hawa jamaa wakandarasi wazuri katika mradi huu watatusaidia katika kufanikisha *camera* hizi. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, nimalizie kwa wafanyabiashara mizigo inayokwenda Dar-es-Salaam wafanyabiashara wadogo wadogo. Mhe. Mwenyekiti, tuangalie hapa kuna changamoto. Mara nyingi nakuwa nakwenda Dar-es-Salaam nakwenda narudi napata kuangalia pale bandarini. Mtu anakuja na mzigo wake kutoka Zanzibar, sio mfanyabiashara lakini mtu ana mzigo wake kama TV au friji au ana kabati lake au ana nguo zake, za mtoto wake au za mkewe anaambiwa alipe kodi pale.

Mhe. Mwenyekiti, *TRA* anafungua mzigo anachakura anamwaga chini, anapiga mahesabu anamwambia shilingi 30,000 au shilingi

40,000. Mhe. Mwenyekiti, kodi ya nini kama tunatoka nchi moja, hapa Zanzibar na Tanzania Bara ni nchi moja. Unatoka hapa Zanzibar unakwenda kule Bara unaambiwa ulipe kodi, hili haliko sawa kidogo. Huu Muungano wetu mzuri, Muungano wa kihistoria katika nchi yetu, na ni Muungano wa kidugu na wa kidamu mimi nasema. Lakini tuangalie hii changamoto ndogo Wazanzibar na Watanzania Bara ni watu wamoja na ukitizama kwenye Katiba ya Jamhuri ya Muungano, ambayo inasema Mtanzania ana haki ya kwenda kuishi popote. Leo mimi nikiamua kwenda kuishi Arusha au Tanga ama Dodoma mtu hawezi kunizuwiya.

Mhe. Mwenyekiti, sasa mimi nakwenda kuishi Arusha natoka na vitu vyangu naambiwa nilipe kodi pale. Kwahivyo, suala hili tuliangalie kiundani Mhe. Mwenyekiti, kuna mambo tuyarekebishe, ili kuuboresha huu Muungano wetu, huu Muungano ni mzuri watu wanauchafua kwa kupitia hapa tu Muungano huu. Sasa naomba tuondowe suala hili kuhusu hii mizigo midogo midogo.

Mhe. Mwenyekiti, ukiangalia Dubai, nimeangalia kwenye mitandao Dubai mwaka 2018, wanasema watalipisha kodi asilimia 5 ya bidhaa, lakini bidhaa yenyewe ipindukie zaidi dola laki moja, diriam 370,000. Lakini ikiwa bidhaa ya dola 20,000 au 30,000 hulipi kodi, lakini kuanzia bidhaa ya laki moja basi utalipa asilimia 5 tu. Sasa hawa wafanyabiashara ndogo ndogo wetu maskini wanatafuta riziki. Mhe. Mwenyekiti, waachie wanatafuta maisha waende Dar-es-Salaam wakauze hiki na hiki huu ni Muungano wetu sote na Muungano huu lazima mmoja ataumia, tuurekebishe huu, ili wafaidike hawa mizigo midogo midogo waweze kupita nao.

Mhe. Mwenyekiti, nitowe mfano mwengine juzi kulikuwa na gari moja, nilisikia hiyo *story*, sijui wewe unaweza ukawa unaijua, lakini mimi niseme kama kweli au kama haliko utaniweka sawa. Kuna gari ya *SUZA Zanzibar University* siku moja ilikwenda Dar-es-Salaam kwa matengenezo tu, wakati wa kusafirisha kwenda kule ...

**Mhe. Mwenyekiti:** Mhe. Mjumbe, una dakika mbili.

**Mhe. Hussein Ibrahim:** Ahsante Mhe. Mwenyekiti, namalizia. Wakati wa kusafirisha kwenda kule Dar-es-Salaam, basi wakaambiwa haiwezi gari hii kwenda kule, ilitakiwa itowe *deposit* shilingi milioni 10 na ilitaka kwenda *garage* tu kutengenezwa, ilishindikana ikabidi itowe milioni 10 hiyo gari ya *SUZA* ilikwenda kwa ajili ya hiyo *deposit*.

Mhe. Mwenyekiti, kuna mtu mmoja gari yake ilikuwa *Rage rover* alikuwa anataka kupeleka Dar-es-Salaam *CMC* kutengenezwa ile gari ni ya kitaalamu kidogo. Akaambiwa gari ile ukitaka kuipeleka Dar-es-Salaam upeleke *deposit* shilingi milioni kama 20 uweke *deposit*. Sasa akawaambia mimi nakwenda Dar-es-Salaam kupeleka kwa fundi siku tatu narudi hapa, imeshindikana. Yule jamaa akaipakia kwenye *container* gari yake hapa ikenda mpaka Dubai ikatengenezwa, ikarejeshwa hapa ile gari kalipa *flight* dola 800 kwenye *container* tu kwenda Dubai na kurudi dola 800 kama 3,000 tu gari yake imeshatengenezwa Dubai imepelekwa. Lakini sisi kutoa gari hapa kwenda Dar-es-Salaam unaambiwa ulipe kodi uweke *deposit*. Sasa mtu kama hana milioni 10 au milioni 20 itabidi gari hiyo hawezi kuipeleka. Kwahivyo, naomba kama mtu anataka kwenda kutengeneza gari yake basi apewe kibali maalum. *(Makofi)*

Jambo jengine Mhe. Mwenyekiti, naomba nimuulize Mhe. Waziri, kama mtu ukimwacha Mhe. Mwakilishi, au Mhe. Mbunge, mtu wa kawaida mfanyabiashara ndogo ndogo ana gari yake anataka kwenda Ngorongoro Mikumi kutembea, ile gari anataka kwenda Dar es Salaam kuvuka nayo. Kuna meli ya Bakhresa hapa Sea Link inakwenda kwa shilingi 250, 000 tu unapakia gari yako. Lakini gari ikifika pale unaambiwa ulipe *differences*. Sasa kama mtu kama anataka kwenda kutembea wiki mbili na gari kaamua tu na familia yake. Hii iangalieni.

Mhe. Mwenyekiti, ukiacha mtu kwenda kuuza gari, kwenda kutembea. Ziwekwe *ID* na kila kitu zikamatwe baada ya wiki mbili lile gari ni lazima litoke Tanzania Bara irudi kwao. Hilo halina tatizo, sasa kuna mambo mengine Mhe. Mwenyekiti, turekebishe kwa ajili ya huu Muungano wetu mzuri na usiwe na changamoto ndogo ndogo kama hizi. Tuwakamate wafanyabiashara hatuna tatizo walipe kodi. Lakini hawa wafanyabiashara wadogo wadogo tuwaangalie tusiwabane. Mhe. Mwenyekiti, pale *TRA*...

**Mhe. Mwenyekiti:** Mhe. Mjumbe, muda wako umemaliza.

**Mhe. Hussein Ibrahim:** Haya. Ahsante Mhe. Mwenyekiti, naunga mkono asilimia mia kwa mia bajeti hii. Waheshimiwa Wajumbe nawaombeni sana, bajeti hii ni uti wa mgongo wa nchi yetu, kwahivyo tumwachie Mhe. Waziri afanye kazi tusimpigie mabuti, ili afanikiwe na azma yetu ifikie malengo. Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru sana ahsante sana. *(Makofi)*

**Mhe. Mwenyekiti:** Ahsante sana. Sasa namwite Mhe. Mohammed Said Mohammed na baadae Mhe. Panya Ali Abdalla ajitayarishe.

**Mhe. Mohamed Said Mohamed:** Mhe. Mwenyekiti, nikushukuru kwa imani yako kwangu. Kwanza na mimi nitowe pongezi za dhati sana kwa Mhe. Waziri kwa uwasilishaji wake bora. Lakini akifuatiwa na Katibu Mkuu na watendaji wote wa bajeti walioandaa bajeti hii, lakini na wote walioandaa kazi kubwa ambazo wamezifanya. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, nianze kwenye Tume ya Mipango. Mhe. Mwenyekiti, Mwenyezi Mungu ametujaalia Zanzibar tuna mipango mingi sana. Moja ya mipango hiyo tunayo *Vision* 2020, tuna *MKUZA I, II* na *III*, *Cluster I, II,* na *III*. Nilikuwa nataka kujua tu tunafanya labda tathmini yoyote katika mipango hii yote, na kama tunafanyia tathmini kuna viashiria gani ambavyo tunaweza kuvipata wanaita *indicators* za uchumi wetu. Maana yake kila Kaya tunaambiwa uchumi umekuwa. Lakini sisi tuliokuwa chini kwa wananchi tunaona bado mifuko iko mikavu sana na wananchi wanalia sana, labda tunataka kujua tu mipango hii inafanywa vipi. Lakini wale ambao wanafanya kazi kubwa na wazidi kutuelimisha ili basi tuweze kujua mipango yetu hii niliyoitaja mingi imefikia wapi.

Mhe. Mwenyekiti, nije tena kwenye kitabu chetu kikubwa hiki, nataka ufafanuzi kidogo kwenye fungu F01, ukurasa wa 19 kifungu kidogo cha SF010104 Usimamizi wa Fedha za Ndani. Mwaka jana zilitengewa milioni 720,881,000, lakini mwaka huu imetengewa bilioni 3,033,063,000, nilikuwa nataka kujua kazi gani kubwa ambayo imepangiwa bajeti hii ambayo imepita zaidi ya asilimia 100, tuweze tu kujua kidogo baadae naweza kutoa ufafanuzi tukenda kwenye mafungu.

Mhe. Mwenyekiti, kwenye kitabu hiki kwenye ukurasa wa 49 kuna gawiyo hapa la *BOT*. Gawiyo makadirio yake ni bilioni 4, lakini mwaka huo huo wa 2016 kwenye kifungu (c) hakuna kitu,

na kwenye *percent* pana *zero*. Sasa nilikuwa nipate tu ufafanuzi kidogo itakuwaje.

Lakini jengine kodi ya nyumba za serikali ukurasa huo huo 49. Kuna kodi ilikisiwa kupata milioni 900, lakini katika kukusanya ilikusanya milioni 86 asilimia 10 tu. Sasa nilikuwa nataka kujua watu hawa hawalipi au wanakaa bure au vipi.

Jengine niende kwenye ukurasa wa 50. Mhe .Mwenyekiti, ukurasa huu kuna tathmini ya ufuatiliaji wa mipango ya maendeleo, ambayo nayo imefikia asilimia 9. Nilikuwa najiuliza kwa akili ya kawaida tu, hivi asilimia 9 tutafuatilia mipango gani, sina uhakika Mhe. Waziri atakapokuja hapa labda aje aniambie tathmini hii imefanyika vipi.

Mhe. Mwenyekiti, jengine uratibu wa rasilimali za nje, tumepata asilimia 12. Vilevile, nilikuwa nina wasi wasi nayo sana. Jengine ni usimamizi wa uchumi mkuu, sasa nayo hii tumepata asilimia 11 tunasimamia vipi ikiwa tumepata asilimia 11, labda nilikuwa nimepitikiwa kidogo, hivyo Mhe. Mwenyekiti namuomba Mhe. Waziri hapa atakapokuja aniambie ni jinsi gani maana yake tunaweza kukusanya na asilimia hizi tulizozipata, kama wananchi hawa na nyumba hizi zilizotajwa za serikali zinalipa au la.

Mhe. Mwenyekiti, nije tena katika Mamlaka ya Uwekezaji Vitege Uchumi, niwapongeze sana kwa kazi kubwa wanazozifanya, lakini bado tunahitaji kupata *One Stop Centre*. Mhe. Waziri tunahitaji sana tupate *One Stop Centre* iwe imejumuisha kila kitu pale, ili basi wawekezaji wetu wanapokwenda waweze kuhudumiwa kwa muda mfupi lakini kwa uhakika.

Mhe. Mwenyekiti, kuiga sio vibaya tuwaige wenzetu wa Rwanda, tuwaige wenzetu wa Mauritius, tuwaige wenzetu wa nchi mbali

mbali ambazo zimeendelea kiutalii, ili tuone basi uwekezaji wao au Mamlaka hii ya Uwekezaji wanafanyakazi nyingi, na tusiogope kupoteza pesa kwa kuweza kutangaza na kuweza kufanikisha mamlaka hii, mamlaka hii ni nguzo yetu kubwa sana.

Mhe. Mwenyekiti, niende *PBZ*, niwashukuru na niwapongeze sana kwa kazi kubwa ambazo wanaweza kuzifanya. Tujitahidi sana na huduma zetu lakini waone nao tunawapongeza kwa kazi kubwa wanazozifanya.

Mhe. Mwenyekiti, nimeangalia katika ukurasa wa 28 wa kitabu hiki, unasema kazi za *ZUSP* lakini sikuona mtaro ule wa mpendae, nimeiona mitaro miwili tu ambayo inamaliza Julai. Mitaro yenyewe ni Mtopepo na Karakana, lakini bado Mpendae Kwabintiamrani sikuuona. Kwahivyo, nilikuwa nataka Mhe. Waziri aniambie mtaro huo umo au nao umewekwa *pending* mpaka mwakani inapokuja. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, niende kwenye *ZRB*. Nimpongeze Kamishna na naibu wake kwa kazi kubwa ambazo wanazifanya na tumeona ni jinsi gani wameweza kujitolea na kuvuka lengo la ukusanyaji.

Mhe. Mwenyekiti, sasa *ZRB* wanakusanya sana. Lakini nilikuwa nasema waweke miundombinu imara kwa walipa kodi wa hapa ndani, kwa sababu kodi ambazo wanazikusanya ni nzuri tu hasa za watalii. Lakini wananyanyasika wafanyabiashara wadogo wadogo, wafanyabiashara wenzangu wa Kwahajitumbo wa Mpendae, wa Magomeni kodi zimekuwa nyingi. Kwasababu hiyo basi tukiwa tunaziweka kodi hizi bila ya kuvuja za kwenye utalii na sehemu nyengine, basi wafanyabiashara hawa wadogo tunaweza tukawapa *holiday*. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, niseme tu kuna makontena yameshuka sasa hivi, lakini hatujui hata pamoja, ndio maana nakuwa nasema sisi Serikali ya Zanzibar hatujui lipi tunalolitaka, kama tunataka utalii, tunataka kukusanya kodi maana yake tumo tumekuwa tunajamba kwenye maji tu.

Moja kuna *Zanzibar Bureau of Standard (ZBS)*. Sasa hivi ukileta kontena kutoka Dubai, hata la *food staff,* linachajiwa pesa nyingi kama hukulipa kule, likitizamwa kule unalipa *penalty* na risiti ninazo hapa.

Lakini jengine tuna Mamlaka ya Kumlinda Mlaji katika Wizara ya Afya, kwa nini sasa isifanye kazi hii basi hata *food stuff.* Tuseme magari ilikuwa mbali, kuna makampuni ya watu binafsi yako kule, maana yake tutasema makampuni ya watu binafsi yanafanyakazi kule. Lakini kwa nini pesa hizi zisiingie kwenye serikari yetu moja kwa moja, kwa nini tusikusanye hapa, kwa nini tusifanye utaratibu mzuri. Tutakapofanya utaratibu mzuri kwa mlipa kodi, tutakapofanya utaratibu rafiki kwa mlipa kodi basi kodi zitalipika tu. Sasa tunapofanya huu ukiritimba na utitiri wa makodi lazima watatukimbia. Kwahivyo, niiombe sana serikali kuweza kuliangalia suala hili, hizi *interest* za watu ziachiwe mbali, tulipe kodi hapa kwa mujibu wa taratibu zetu na sheria za kodi zinavyotuelekeza.

Mhe. Mwenyekiti, nataka kuwapongeza sana *ZSSF* kwa kazi kubwa ambazo wanazifanya, lakini kwa uwekezaji mkubwa ambao wanaufanya na tuwashukuru tu. Lakini nilikuwa nataka kujua kitu kimoja kuhusu hizi pencheni za wazee wetu wanaostaafu, kuna wazee wengi sana wanastaafu, lakini pencheni bado mshahara unapanda pencheni bado haipandi. Mimi niseme tu kama sikupata jibu la uhakika Mhe. Mwenyekiti, nitakuja na

hoja binafsi sasa ya kuishurutisha serikali iweze kupandisha pencheni.

Kwanza kwa sababu kuna wazee, kama nimewaona wazee wangu wamefikia hatua yakuwa mameneja kwenye benki, lakini ukiangalia pesa zao ni ndogo sana. Ninao hapa lakini sitaki kuwataja tu, kwa sababu wao hawahusiki humu ndani. Wanapata pesa kidogo sana, lakini mtu wa kawaida tutizame vilevile na Askari Magereza. Tulikuwa tuna kesi miaka ya nyumba ya Askari Magereza, uliwekwa mfumo wa kuweza kupata pencheni zikawa ndogo. Lakini walipokwenda mahakamani wakapewa pencheni yao iliyokuwa kubwa, lakini sasa hata mtu mwenye nyota moja anapostaafu hawezi kumfikia *Staff Sergeant* yule wa zamani. Hebu tuweke utaratibu na tuone Mhe. Waziri atakapokuja hapa anijibu ni utaratibu gani unaoelekeza huu hata huyu mtu ana nyota moja anapitwa na stafsajenti ni utaratibu gani au *scheme* gani imepangwa hapa, labda tuweze kujua.

Mhe. Mwenyekiti, nije kwenye Mfuko wa Barabara niwapongeze sana na niwaambie tunayo haki ya kujisifu na Mfuko wa Barabara. Nitatoa mfano. Mfano wa kwanza kabisa tuone barabara ya Fuoni, barabara hii watu wengi watu wanadhani ile wameijenga wafadhili au fedha tumekopa, zile ni fedha za Mfuko wa Barabara ni lazima tujisifu, ile ni kodi yetu wenyewe ni kodi ya wananchi wavuja jasho, lazima tujisifu tumefika pahala Mfuko wa Barabara sasa unafanyakazi kubwa. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, mbali na hayo lakini niseme tu na kuna barabara nyingi sana chakavu katika miji yetu. Tuhangaike, lakini kila tunapoweza tunapopata muda basi tuweze kuzitengeneza. Barabara yetu kutoka Mchina Mwisho sokoni kupitia Mpendae mpaka Jang'ombe, bado ina ahadi ya Mhe. Rais. Kwahivyo, tungewaomba sana waweze kuishughulikia na waweze kuifanya

ili inaweza ikapunguza hata *queue* ya kupitia huku Kwamchina Mwanzo, inaweza ikapunguza hasa *queue* kubwa ambayo inaweza kutokea.

Vilevile, kuna barabara nyengine ya Wambaa Kwaazani, hiyo nayo haiwezi kujengwa kwa Mfuko huu wa Jimbo. Kwahiyo, tunaomba wajitahidi sana katika kufanya kazi na sisi tunawapongeza kwa kazi kubwa ambazo wanaweza kuzifanya.

Mhe. Mwenyekiti, nilikuwa leo nataka kuchangia mambo madogo sana haya. Lakini kubwa nimwambie Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Mwenyekiti, wafanyabiashara wadogo wapunguziwe utitiri wa kodi sio kodi zinakuwa nyingi kila unapokwenda unalipa kodi, watu wengi wanafunga biashara zao sasa kwa kodi zimekuwa nyingi. Kwahivyo, tungewaomba sana waangalie utaratibu wa kulipa kodi na uwepo mfumo mmoja hasa wa kulipa kodi. Nikushukuru sana Mhe. Mwenyekiti. *(Makofi)*

**Mhe. Mwenyekiti:** Mhe. Mohamed Said Mohamed ahsante sana. Sasa anayefuata ni Mhe. Panya Ali Abdalla na Mhe. Suleiman Sarahan Said ajitayarishe na Mhe. Abdalla Maulid Diwani naye pia ajiandae.

**Mhe. Panya Ali Abdalla:** Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, nichukuwe fursa hii kukushukuru kwa kunipatia nafasi ili niweze kusema machache katika wizara hii.

Mhe. Mwenyekiti, kabla ya mchango wangu napenda nichukuwe fursa hii kumpongeza sana Mhe. Waziri na watendaji wake wote kwa kazi kubwa na nzuri ambayo inaleta faraja kwa Wazanzibari wote. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, nianze mchango wangu katika Bodi ya Mapato ya Zanzibar. Mhe. Mwenyekiti, sina budi kuchukua fursa hii kuipongeza kwa dhati serikali na kumpongeza sana mwenyewe Mhe. Waziri kwa juhudi zake ambazo tunazishuhudia siku hadi siku katika ukusanyaji wa mapato.

Mhe. Mwenyekiti, mapato yetu yameongezeka kwa asilimia 31 kama alivyotueleza Mhe. Waziri ni jambo la faraja na ni jambo la kutia moyo. Sisi wenyewe tumekuwa ni mashahidi kuona bajeti yetu mara hii kila wizara kuna ongezeko la bajeti hii inatudhihirishia tutakapojitahidi kukusanya mapato na kudhibiti mianya ya mapato maana yake tunaweza kufikia katika hali ya kujitegemea sisi wenyewe, kujiendesha bila ya kuwa na bajeti tegemezi.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nimuombe tu Mhe. Waziri azidi kuongeza juhudi zake tuko nyuma yake tunam-*support* sana kwa kuona hili analolifanya tuko pamoja nae kwa sababu ana lengo zuri kabisa la kuweza kuifikisha nchi yetu mahala pazuri, kwa sababu nchi yoyote inatakiwa kuwa na uchumi mzuri kwa hivyo ukiweza kuisimamia vizuri huo uchumi wa nchi maana yake tayari tutaweza kujiendesha.

Mhe. Mwenyekiti, mchango wangu mwengine nilitaka niende katika vipaumbele vya wizara ambapo katika vipaumbele hivi vya wizara kuna kifungu cha 60 ambacho katika *bullet* ya 7 kinaeleza kukamilisha uanzishaji wa sheria mpya ya ushajihishaji wa kulinda uwekezaji. Mhe. Mwenyekiti, nimuombe Mhe. Waziri kwa kuwa tayari wanayo hii sheria wanataka kuikamilisha basi nikuharakisha kukamilika kwa sheria hiyo, ili tuweze kulinda uwekezaji, kwa kweli hvi sasa kuna matukio ambayo yanajitokeza yanavunja moyo wawekezaji. Kwahivyo, tutakapokuwa na sheria hii tukaweza kuulinda uwekezaji wetu, ili wakawa katika hali

salama kwa hivyo tunaweza kukuza pato la uchumi wetu. Mhe. Mwenyekiti, nimuombe Mhe. Waziri kuendelea na juhudi zake hizo ili hatimae tuweze kufika pahala pazuri.

Nikiendeela na mchango wangu pia nilitaka atakapokuja Mhe. Waziri hapa aweze kutufafanulia, kwasababu serikali imetuhimiza sana wananchi katika kujiajiri wenyewe na kweli wananchi wetu wamo katika harakati hizo za kujiajiri lakini kumekuwa kunaonekana kuna usumbufu unajitokeza. Sasa namuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Mwenyekiti atakapokuja hapa basi hebu atufafanulie ili tuweze kujua.

Katika hamasa hii wananchi wetu wameweza kununua vigari vile vya *carry* ambavyo wanafanyia wenyewe shughuli zao ndogo ndogo, lakini utakuta wengine wanafanya katika shughuli za kilimo na mifugo yao. Sasa akikutikana kigari kile kimebeba mbolea labda kinapeleka shambani katika kujiimarisha na kilimo basi utakuta *TRA* wanawazuria na kuwakamata na kuwapatisha tabu. Mhe. Mwenyekiti, namuomba Mhe. Waziri atakapokuja atufafanulie vipi wakulima wetu hawa waweze kutumia vile vigari vyao ili na wao waonekane kama wako katika juhudi za kujikwamua kiuchumi.

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea na mchango wangu niende kwenye Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali. Kwakweli, katika malengo ambayo mmejipangia moja katika *bullet* ya pili hii mnasema ni kukamilisha kazi za kufanya mapitio ya kuimarisha takwimu za pato la taifa. Mhe. Mwenyekiti nawapongeza kwa hilo, lakini pia niombe sana kwa sababu katika suala zima hili la takwimu kumekuwa na usumbufu mkuu wa kupata Takwimu ambazo ziko sahihi.

Hili nimuombe tu Mhe. Waziri lazima tujikite katika kupata takwimu zilizo sahihi kwasababu kuwa na takwimu sahihi ndio kuweza kuwa na pato la taifa ambalo tutaweza kulitumia vizuri, kwa sababu pato hili la taifa lazima liendane na takwimu ya idadi ya watu. Leo ikiwa idadi ya watu haiko vizuri basi hata hili pato ambalo tutaweza kukusanya litaweza kuwa haliendi kiukamilifu kwa sababu niseme tu mfano kipindi kilichopita nyuma tuliona wenzetu wakati wa zowezi la Sensa basi watu wengi hawakujitokeza katika zowezi lile, ili wakaweza kuorodheshwa na Serikali ikaweza kuwa na mipango yake katika usahihi.

Kwahivyo, naomba katika eneo hili basi tujikite ili tuone tutoe elimu ya kutosha kwa jamii, ili basi zowezi lile la Sensa linapofika basi watu waweze kujitokeza, ili pato ambalo tunalipata basi liweze kuendana na idadi ya watu.

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea na mchango wangu nilitaka pia katika *bullet* ya 7 kuna neno hapa lilijitokeza na mimi nilitaka nijuie kabla ya neno hili tulikuwa tukitumia neno gani katika *bullet* ya 7 aya ya 35 ambayo kuna neno limeandika kuandaa vipindi mubashara 12 vya Televisheni. Kwahiyo, nataka kujua hili neno mubarashara kwasababu nimekuwa nikiona katika vitabu vyetu yanajitokeza maneno kwakweli wengine yanakuwa yanatushinda kuyafafanua na kwakuwa sisi tunataka tuwe na Kiswahili fasaha ambacho utakapokieleza basi mwenzako anayekusikliza aweze kukijua.

Hivyo, namuomba Mhe. Waziri atakapokuja neno mubashara anitafsirie na labda linapatikana katika kamusi gani katika hapa kwetu, kwasababu lengo la serikali ni kuwa na Kiswahili kizuri, fasaha ambacho tunajivunia sisi Zanzibar Kiswahili chetu ni kizuri na walimu wazuri katika kuwafunza wenzetu. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, pia nikienda katika mradi wa kuimarisha utawala bora, hapa mumeeleza kama mtawajengea uwezo wafanyakazi wa taasisi za serikali katika maeneo ya ukaguzi wa tathmini ya fedha. Kwakweli, eneo hili ni muhimu sana na hapa ndipo mapato ya serikali yaapovuja kwa wingi kwasababu *value for money* inakosekana sana, kwasababu wenzetu jambo dogo mtu anaweza akalijenga kwa pesa nyingi au akatumia fedha nyingi katika fedha za serikali au fedha za umma bila ya kuangalia kwamba hizi fedha za wananchi walipa kodi wa nchi hii.

Kwahivyo, naomba sana katika eneo hili Mhe. Waziri atakapojikita sana katika kuangalia hii ukaguzi wake utakapojikita katika hii tathmini ya fedha, kwakweli ataweza kuzigundua fedha nyingi za serikali zinapotea katika maeneo haya. Kwahiyo, nimuombe tu Mhe. Waziri aendeleza juhudi zake ambazo amezikita katika kuiona nchi yetu hii inakuja juu kimapato siku hadi siku, tunaweza kuwa na bajeti ya kuweza kwa kuzingatia kuyahifadhi mapato yetu na pia kuyatumia vyema katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, nilikuwa sina mengi lakini kwa juhudi yetu huyu Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango Dkt. Khalid Salum Mohamed anavyoweza kujikita katika kukusanya mapato na kuyasimamia vizuri, ni lazima nikasema niinuke niunge mkono hotuba yake kwa asilimia mia moja. Mhe. Mwenyekiti ahsante (*Makofi*)

**Mhe. Mwenyekiti:** Ahsante Mhe. Panya Ali Abdalla kwa mchangio wako. Sasa naomba imwite Mhe. Suleiman Sarhan Said akifuatiwa na Mhe. Abdalla Maulid Diwani na Mhe. Miraji Khamis Mussa ajitayarishe.

**Mhe. Suleiman Sarahan Said:** Nashukuru Mhe. Mwenyekiti kwa kunipa fursa nikaweza kusaidia machache au kumpa maelekezo au ushauri wangu Mhe. Waziri, ili tuendeleze gurudumu letu.

Kwanza nianze na Shirika la Bima. Mhe. Mwenyekiti, Shirika la Bima limejikita kwenye vyombo vya moto tokea asili Shirika la Bima mapato yake ni vyombo vya moto ndio limejikita kwenye hilo hawana pesa watakaa barabarani wasimamishe magari basi, lakini halikujijengea uwezo kubiashara. Shirika la Bima kwa ufahamu wangu nimeona kama ni chombo ambacho kinachoweza kusaidia serikali katika kuepukana na matatizo ambayo serikali ingekuwa ni ya kulipa fidia au kusaidia katika mitaala mbali mbali ambayo wananchi wake wanaweza wakapata matatizo.

Lakini Shirika la Bima inawezekana wana taaluma ya maandishi kwamba wanatoa Bima za Afya, wanatoa Bima za Ajali, wanatoa bima za kila kitu lakini ufuatiliaji wake na utendaji wake unakuwa haujafikia kiwango, kwasababu hauoneshi dhana nzima ya kulazimisha, ili kuweza kuhakikisha kwamba wananchi wanakata Bima ya Afya, wanakata Bima ya Ajali, wanakatishwa bima ya kila kitu kwa mfumo wowote ilimradi kuipunguzia serikali mzigo na wananchi kwa ujumla. Kwahivyo, ningeomba sana Shirika la Bima likajipanua zaidi katika wigo wa kutafuta mapato, lakini wigo wa kuisaidia serikali katika mambo kama haya hilo kidogo ilikuwa nisaidia ingawa katika kitabu namba 47 wamejielezea humu lakini lazima niweze kutoa ufafanuzi zaidi na kusaidia.

Jambo jengine nataka katika majukumu ya wizara katika ukurasa wa tatu, ninachosema Mhe. Mwenyekiti majukumu mengi ya taasisi ambayo yamejiwekea ni kwamba kukusanya mapato ya serikali kutokana na vyanzo vya ndani, kuratibu upatikanaji wa rasilimali kutoka nje ya nchi na kusimamia matumizi yake,

kusimamia rasilimali za serikali, kusimamia mwenendo wa deni la taifa, kutoa huduma za uhasibu serikalini, kusimamia maendeleo ya sekta za fedha kuanda, ni mambo mengi kupunguza umasikini wa mfumo huu.

Mhe. Mwenyekiti, nilikuwa nizungumze kwamba wizara ilitakiwa ijikite sana maneno yake na utendaji wake yaweze kufikia malengo, si hivyo tutabakisha kwenye vitabu kwasababu tunapeleka neno kupunguza umasikini, kufuatilia mambo haya lakini bado tukitizama ufuatiliaji kidogo unakuwa na matatizo.

Mhe. Mwenyekiti, tukichukulia unaweza ukaona kuna wizara imefanya makosa katika suala la mtendaji, lakini haraka haraka serikali inamuondoa mtendaji yule inampeleka pahali pengine bila ya fedha zake zilizopotea kurejeshwa mtu yule anapangiwa sehemu yengine na ushahidi unapotea. Lengo la serikali sio mtu yule kufanya chochote zaidi ya kwanza zirudishwe pesa zilizopotea halafu mengine yatafuata baadae. Lakini sio kumuondoa mtu yule kabla fedha ile haijapotea. Mhe. Mwenyekiti, naomba kuishauri sana serikali ikalitizama kama mtu kaharibu basi awe *pending* pale pale mpaka fedha ya serikali irudi ndio tena maamuzi mengine ya serikali yafanyike.

Mhe. Mwenyekiti, jambo jengine ambalo nataka kulizungumzia ni kwamba kusimamia ujenzi wa jengo jipya la Afisi Pemba. Kwakweli, nimeona upeo mzuri wa kusimamia maofisi kitu kilichonifurahisha ni mwelekeo ambao nilikuwa naupigia kelele kila siku, serikali inasema kwamba ardhi ni mali ya serikali, lakini siku zote serikali inakodi nyumba za watu, hili sijui ilikuwa sababu inakuwa wapi, lakini nimefurahishwa humu sasa hivi katika hatua zao Mhe. Waziri, karibu wizara tatu Pemba sasa hivi zinajenga majengo mapya, hivyo napongeza pamoja na kutoa shukurani. Mhe. Mwenyekiti, na hii ninashauri mpaka ikifika

mwaka 2020 panapo majaaliwa iwe hakuna tena wizara zinazokodi lakini pia na hadhi yake itimie kutokana ile hadhi ya lile jengo. Mhe. Mwenyekiti, ilikuwa pia nishauri kwa Mhe. Waziri, likiwezekana kutokana na uwezo liwezekane hilo.

Vilevile, nimpongeze Mhe. Waziri kwa hatua aliyofikia katika kipindi labda niseme mwaka mmoja tokea kuteuliwa kwake, ameibua miradi mingi ambayo baadae kwa kipindi cha miaka mitatu mpaka minne panapo majaaliwa mpaka 2020. Mhe. Mwenyekiti, nina uhakika kodi zitaendeleza au zitakuja kodi nyingi kutokana na uibuaji wa miradi, itakapokamilika miradi hii basi nina hakika hatuna haja ya kuongeza kodi isipokuwa zaidi ni kukusanya kodi. Mhe. Mwenyekiti, nimpongeze sana Mhe. Waziri anajitahidi kwa kuibua miradi ambayo itasaidia kuongeza kodi.

Mhe. Mwenyekiti, nataka nije kwenye *ZSSF* Mhe. Waziri bado malalamiko ya wafanyakazi wanaomaliza muda wao yanakuwa yana matatizo. *ZSSF* sasa hivi imejikita sana kwenye majengo kwenye maeneo ya biashara ni vizuri sana inaongeza mitaji. Lakini basi tufike pahala unajua mtu anapofanya kazi katika umri wake wengine wana mashaka mengi na binaadamu na Mwenyezi Mungu hawana ahadi ya umri, siku nyengine anamaliza kazi na mauti yamemfika almradi ni mashaka makubwa sana yanayomfika binaadam baada ya kuacha kazi.

Lakini ningeishauri serikali kwasababu ina uhakika na ina takwimu za kutosha kwamba mfanyakazi fulani anamaliza muda wake, hivyo, nashauri kabla ya miezi mitatu ya kumaliza kwake kazi basi mafao yake ama yakawa tayari au yakawa ameshalipwa kabisa akiondoka pale tukaachana kabisa kabisa. Mhe. Mwenyekiti, nashauri hili suala Mhe. Waziri akalitizama kwamba unajua kuna vitu vyengine inakuwa kama vinatushtaki kwa

Mwenyezi Mungu unapomuona *ZSSF* anajenga jengo la bilioni pesa yangu milioni 10 hanipi Mwenyezi Mungu atanilipia inaumiza kidogo na inaleta sitofahamu sio nzuri.

Ningeomba kitengo ambacho Mhe. Mwenyekiti kina watu ambao wanastaafu kimpe taarifa Mhe. Waziri mapema watu hawa wanastaafu mwezi fulani aweze kujipanga na kuwawekea fungu lao, ili tusipate matatizo katika masuala kama haya.

Lakini pia nikupongeze nimeona kwenye kitabu katika ukurasa wa 14 aya ya 27 nimeona umejiamulia sasa hivi kutujengea barabara yetu ya Chake-Chake/Wete nimeiona katika humu na kupongeza sana hichi ni kilio cha muda mrefu, lakini pia watu na ile hamu yao itawafikia katika masuala husika.

Mhe. Mwenyekiti, nataka kidogo kwenye ukurasa wa 49 Mhe. Waziri atakapoku katika ukurasa wa 49 nimeona ukusanyaji au mapato yaliyokusanywa na Wizara ya Fedha katika kipindi cha Julai mpaka Machi, 2016/2017. Hivyo, namuomba Mhe. Waziri atakapokuja naomba anipe ufafanuzi kidogo katika vyanzo vyote. Katika chanzo ambacho nimekiona kimevuka lengo ni mapato kutoka Idara ya Uhamiaji hii imepata asilimia 118, lakini wizara nyengine nimeona asilimia kumi uuzaji kama huu wa vifaa chakavu, kodi za nyumba asilimia 10 kodi za bohari asilimia 15 ukija hebu nipe ufafanuzi kidogo kwa nini haa kodi zao zikochini sana, mapato yao yamekuwa yako chini. Lakini hili la vifaa chakavu kama litakuwa linaingia hapo ningeomba labda sijui kama ni sheria au utaratibu atakapokuja anieleze hizi gari za serikali zinatumika katika serikali mpaka muda gani, ili iweze kuuzwa au kuondoka katika serikali isiwape mzigo kwa sababu imeshachakaa.

Vilevile nataka ufanywe uhakiki gari za serikali inalala kwa kipira cha breki prado au gari gani, lakini gari ile wakati wa kuja kuuzwa haina tairi, haina *engine*, haina hata defu limebakishwa bodi. Sasa sijui utaratibu wa chombo hicho wakati inalala inaandikwa vipi na wakati inauzwa inauzwa vipi. Mhe. Mwenyekiti, namuomba Mhe. Waziri atakapokuja aje anipe utaratibu wa uuzaj wa gari za serikali kwa nini yasiuzike wakati ambao bado zina uhai na zinaweza kusaidia tukapata gari nyengine nzuri na bei ambayo ina muafaka. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, nataka nizungumze tena na Mhe. Waziri sijui ushauri wangu atauchukua au vipi na kuna kitu kimoja kwamba Mhe. Waziri anakusanya mapato mengi lakini matumizi makubwa ya serikali. Naomba kutoa ushauri Mhe. Mwenyekiti, kwa nini katika mambo ambayo ni ya lazima tunayoyaona yana maslahi kwa wananchi, kwa nini tusitumie zaidi makampuni, mashirika au watu wegine katika kufanya ubia na pesa zetu ambazo tunazo *cash* katika serikali tusiweze kuzitumia kama kufanya *risk*, maana yake ni *risk* tunatumia tumenunua meli yetu ya Mapinduzi mabilioni lakini lengo na madhumuni ni kuwasaidia wananchi wa Pemba kuondokana na tatizo la usafiri.

Lakini nashauri kama hapa tungeweza kutafuta mtu mbiya tukaingia naye mkataba ile pesa yetu tulioundia meli tukaweza kufanya mambo mengine. Kwahivyo, ningeona kwamba kungekuwa tunafanya mambo ambayo tukiona kama kuna shida fulani tukatafuta mtu haraka akatusaidia katika mambo ya kufanya ubia.

Serikali ikakushanya kodi lakini pia ikawa ina mpangilio wa kibiashara lakini pesa yetu ya ndani tukaweza kuidhibiti kwanza tusiitumie haraka haraka, mpaka tukaona tumeshindwa kupata mtu ambaye tunaweza tukawasiliana naye katika mambo haya

ndotukaweza kuitumia, ni pesa nyingi tunazozitumia katika miradi mingi tu lakini mengine inakuwa kama ni miradi ya muda mfupi, mengine inakuwa miradi ya muda mrefu. Lakini kama tunapata uwekezaji tukaweza kutumia fedha zetu tunaweza kuzikusanya na tukawa tuna mtaji, ili kupunguza makali ambayo tunaweza tukasema tunanua chombo lakini hakilipi, tunanunua chombo lakini baadaye kinakuwa hakipati faida zaidi ya hasara ya serikali. Lakini kama tutapata mbiya wa kututekelezea lile tatizo letu basi tungeondokana na hilo tatizo na bado fedha zetu tunazo.

Mhe. Mwenyekiti nataka nimwambie Mhe. Waziri kwamba upotevu wa fedha tunautizama sana *ZRB* tunautizama sana katika mazingira mengine, lakini upotevu wa fedha za serikali ziko kila sekta. Mhe. Mwenyekiti, namuomba kwamba anawasimamia wahasibu katika kitabu chake katika wapi, lakini Mhe. Mwenyekiti fedha bado sio ya muhasibu ambayo anayoipeleka yeye kuitumia lakini hata makusanyo katika mawizara zinapoteza fedha nyingi. Kwakweli, Mhe. Mwenyekiti, bado mpangilio wa kusema tunatumia risiti za vitabu bado tunapoteza kodi, tunashapisha sisi na kitabu kinatoka nembo ile ile, na kitabu chako na changu kiko sawa sawa lakini bado fedha zinapotea. Kutokana na hali hiyo, bado namshauri Mhe. Waziri ajitahidi atafute pahala pa kuweza kwenda kwenye *eletronic*, ili kupunguza mianya hii ya kuvuja.

Tunatizama pande kidogo za kuvuja tunawang'ang'ania watu wa *ZRB* na watu wengine, ni kweli kuna uvujaji kuna kila kitu, lakini na mashirika mengine yanavujisha hivyo hivyo, lakini tu kwasababu yule ni mkusanyaji kodi anakuwa yeye huwa mbuzi wa kafara. Kwahiyo, nimeona lazima tuangalie kitu hicho ambacho kitakuwa katika muelekeo huo.

Mhe. Mwenyekiti, nirudi tena kwenye mfumo huo huo, wa ulipaji kodi, nina matumaini ya mfumo mpya wa ulipaji kodi na kuondoa mfumo wa makisio utaratibu huu, kodi huu ni mzuri kwa kuthibiti wahalifu na wakopa kodi. Mhe. Mwenyekiti, dhana pamoja na fikira zangu inaweza ikatusaidia sana kwenye makisio mtu akeshafikisha anavua koti analitundika, kilichobakiya lete huku inakuwa kama mfumo ambao kidogo unampa *limit*, nafikiri huu mfumo mpya unaweza ukatusaidia sana.

Lakini pia bado *ZRB* nairudia sana katika sekta nyengine ujiimarishe kwa makini au kwa umakini na uadilifu tudhibiti mfumo wa kodi na mianya inayopotea kirahisi rahisi. Mhe. Mwenyekiti, mifumo hii ya *ZRB* sisi ndio tegemeo letu *ZRB* kila kitu tumeikamata *ZRB* kuisaidia serikali na ndio kwasababu yeye ndio mkusanyaji kodi. Kwahiyo, Mhe. Mwenyekiti lazima mfumo ubadilike wa *ZRB* masaa yaongezeke kukusanya kodi, upanuzi wa kukusanya kodi uendelee lakini pia na miundo mbinu ya kukusanya kodi iendelee kwasababu ukusanyaji wa kodi mu kutoa pesa, na baadae akaenda pale akakaa foleni akasema leo sipati nafasi, anaweza akakaa tena siku kumi, kumi na tano labda akachukuliwe kwa polisi ndio aje alipe tena. Kwahivyo, naomba sana miundombinu ya *ZRB* ikaboreshwa zaidi ili kuangalia hali halisi.

Mhe. Mwenyekiti, nataka nikwambie kwamba bado mfumo wa kodi za mahoteli kwakweli tunaibiwa, tena nikikwambia tunaibiwa hesabu ni kwamba muangalie Mhe. Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo atakupa takwimu gani wageni walioingia, lakini tizama pesa ulizopata kodi katika habari hii, humu ukipiga mahesabu sitaki nikupigie mahesabu. Lakini Mhe. Mwenyekiti bado mfumo, ninachokwambia pengine kodi tunayopata asilimia 30 tu, na iliyobakiya kodi asilimia 70 watu wanacheza nayo kwa kila mbinu, pengine pia na hawa

wafanyakazi wake wa *ZRB* pia wanacheza michezo hiyo hiyo. Kutokana na hali hiyo, huyu lazima acheze na yule ndio pafanyike.

Mhe. Mwenyekiti, hii naomba lifuatiliwe kwa kina. Zanzibar ina watalii wengi lakini bado kodi, kodi haijatufikia. Kwahivyo, naomba tena ushahidi unaonekana watu wapo, mambo yapo lakini bado sana kwasababu nimesikia juzi hapa, hakuna mpango wa kuongeza kodi lakini atasimamia kodi sasa tuzisimamie hizi kodi, asionawe mtu, mtu haki yake apewe. Mhe. Mwenyekiti, nataka nikwambie na kitu kimoja, katika kufuatilia kodi watu wa *ZRB* nao wana matatizo baadhi ya *time*, wanaweza akamng'ang'ania mtu kumlipisha kodi na sio halali yake...

**Mhe. Mwenyekiti:** Mhe. Suleiman Sarahan Said unazo dakika mbili.

**Mhe. Suleiman Sarahan Said:** Naam!

**Mhe. Mwenyekiti:** Mhe. Suleiman Sarahan Said unazo dakika tatu.

**Mhe. Suleiman Sarahan Said:** Mhe. Mwenyekiti, dakika tano.

**Mhe. Mwenyekiti:** Unazo dakika tatu.

**Mhe. Suleiman Sarahan Said:** Naomba dakika tano Mhe. Mwenyekiti kwa hisani yako. Mhe. Mwenyekiti, basi ni hilo ni kwamba ajaribu kukaa nao na kuwaeleza asione mtu, usimuone mtu tajiri kwasababu sio haki yake kumtoza kodi kubwa usimtoze mpe haki yake, wala msimuone mdogo ana haki ya kulipa ukasema huyu mdogo namlipisha kidogo, kama ni haki yake ya kulipa alipe, hatumuoni mtu katika serikali na imewekwa kiwango

ambacho kila mmoja anaweza akakilipa. Mhe. Mwenyekiti, naomba hilo alifuatilie sana.

Jambo jengine ambalo nataka nimuombe Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Mwenyekiti, ni kwamba ameshaona matatizo mbalimbali yanayotupata. Mhe. Mwenyekiti, sasa hivi unapotoa pesa ya kupeleka kwenye mradi baada ya takwimu zitakazokuja kutoka wizara, basi namuomba Mhe. Waziri afanye tathmini ya kutoa pesa mradi ule unaanza na kumalizika utumike kwa wakati na lile lengo lililokusudiwa limalizike kama ni kupata kodi, kama ni matumizi yote tunaachane na lile suala hata kama ni vitu vitatu vinne kwa mwaka lakini tunamaliza na baadaye tunaanza na vyengine.

Kwa kweli sio mradi sijui tunakwenda na hatua ya kwanza tunalala baada ya miaka mitano, tunakwenda katika hatua ya haraka katika maendeleo namuomba sana Mhe. Waziri hili atusaidie sana hili. Vilevile, Mhe. Mwenyekiti bado elimu ya kodi, pamoja na mambo yote haitoki bado kuna kodi zinafichwa ndani mtu anakuja ah! Kwa wewe toa kiasi fulani, kwa wewe toa kiasi fulani, kwani kodi halisi ni kiasi gani? Mhe. Mwenyekiti, naomba atangaze, atowe vipeperushi, kodi hii shilingi fulani, kodi hii shilingi fulani, kwasababu utasikia mtu mpaka huko bandarini gari anashindwa kutoa, gari hii kwa siku Wizara ya Fedha na Mipango sijui mapato imepanda bei, bei zimepanda vipi ukiulizwa hapa unajibu bei hazijapanda lakini huko watu wanafanya mambo yao kwa *interest* zao. Nakuomba Mhe. Mwenyekiti, ingawa wakati sina lakini nakimbilia.

**Mhe. Mwenyekiti:** Mheshimiwa muda wako umemaliza.

**Mhe. Suleiman Sarahan Said:** Mhe. Mwenyekiti, nimekuomba dakika tano, sasa unanambia mara moja.

**Mhe. Mwenyekiti :** Mhe. Mjumbe, nakupa dakika mbili uweke sawa na umalizie.

**Mhe. Suleiman Sarahan Said:** Ahsante Mhe. Mwenyekiti.

Jambo jengine ambalo nataka kuzungumza suala la ajira. Kwakweli, nina wasiwasi kwamba ajira baina ya Wizara ya Fedha na Mipango na wizara hizi zinazohusika na ajira pamoja na wizara husika hazina *reaction* nzuri ya mahesabu kamili, kwasababu sasa hivi tunapiga kelele kuhusu ajira na serikali tayari ilikuwa imeshaajiri watu, lakini watu wale kwa hatua moja ama jengine wengine wamestaafu wengine wamekwenda, lakini ninachofahamu na ninachofikiria kuna watu katika wizara anajua kama mtu wangu hayupo hapeleki ripoti kwamba mimi nihitajia mtu, vyeo vyote viwili anavikalia yeye kwa manufaa yake. Mhe. Mwenyekiti, namuomba sana Mhe. Waziri tunaangalia kwasababu kwa nini ambapo tunaweza tukafanya mambo ambayo mtu mmoja tunamtwika kazi mbili tatu wakati nafasi tunayo pamoja na waajiriwa wapo lakini hatuwajiri.

Kwahiyo, namuomba Mhe. Waziri akalipitia hili suala la ajira katika kila wizara akatizama wapi kuna kasoro ambazo hazina watendaji akazifuatilia naomba sana, kwa sababu sina muda Mhe. Mwenyekiti wa kuweza kuelezea zaidi.

Lakini jengine, Mhe. Mwenyekiti kuhusu ukusanyaji wa kodi habari ya wafanyabiashara Mhe. Mwenyekiti...

**Mhe. Mwenyekiti:** Mhe. Suleiman Sarahan Said muda wako umemaliza.

**Mhe. Suleiman Sarahan Said:** Namalizia hili basi Mhe. Mwenyekiti, habari ya wafanyabiashara. Mhe. Mwenyekiti, naomba kwa sababu *PBZ* anayo mikononi mwake naomba akafanya semina baina ya wafanyabiashara pamoja na *PBZ* akaweza kuwasaidia wakapata mikopo wengine hawana utaalam wa mikopo wanalala huko. Pamoja na kwamba hee! Basi Mhe. Mwenyekiti naunga mkono hoja asilimia 100. *(Makofi)*

**Mhe. Mwenyekiti:** Ahsante sasa nitamwita Mhe. Abdalla Maulidi Diwani na Mhe. Miraji Khamis Mussa ajitayarishe.

**Mhe. Abdalla Maulid Diwani:** Ahsante sana Mwenyekiti, kunipa nafasi na mimi kuchangia Hotuba ya Wizara ya Fedha na Mipango.

Awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu kunijaalia adhuhuri hii kusimama hapa kuwa mmoja wa wachangiyaji. Lakini kabla ya kuchangia kidogo naomba nitowe pongezi zangu za dhati kwa Waziri wa Fedha na Mipango wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar Dkt. Khalid Salum Mohammed, kwa ujasiri wake na ukakamavu wake kuisimamia Wizara ya Fedha sasa hivi tumekuja na bajeti hapa inayobadilika tarakimu baada ya bilioni tunakwenda *trillion* nimpongeze sana. *(Makofi)*

Kwakweli, hayo yote yamekuja kutokana na umakini wake pamoja na watendaji wake, Makatibu Wakuu, Manaibu Makatibu Wakuu na Wakurugenzi ikiwa yeye ndio msimamizi namsifu sana. Ilikuwa kilio hapa kwa Serikali ya Mapinduzi kwa *OC* kutotimia lakini sasa hivi *OC* kwa mawizara yote yanakwenda *hundred percent* Mhe. Waziri nakupongeza sana. *(Makofi)*

Baada ya pongezi hizo nende moja kwa moja kwenye hoja bila ya kupotoza muda. Nianzie kwenye ukusanyaji wa mapato kuna

taasisi mbili za ukushanyaji wa mapato Zanzibar kuna *TRA* na *ZRB* nizipongeze kwasababu kitabu kimeandikwa vizuri tu, mpaka sasa hivi robo ya tatu ya mwaka tayari wamo katika asilimia nzuri ya ukushanyaji wa mapato miezi mitatu iliyobakia hii watavuka malengo. Mhe. Mwenyekiti, nampongeza sana Mhe. Waziri kwa kusimamia kuona kwamba wanavuka malengo. Lakini katika hicho Mhe. Mwenyekiti japo nyuma tulizungumza wenzetu wa *ZRB* wanapokushanya mapato yao kuna *ten percent* ya mapato wanapata aidha kama kichocheo *bonus* namna gani sawa naipongeza sana katika hilo.

Wenzetu upande wa pili japo katika Serikali ya Muungano, lakini mapato yale wanayokusanya ni kwa ajili ya Zanzibar, pamoja kwamba katika Mfuko Mkuu pengine *TRA* huko Tanganyika inatoka lakini kuthamini ule mchango wao kwa ajili ya mapato ya Zanzibar, ambao unatumika hapa Zanzibar, basi angalau asilimia mia mbili ya makushanyo basi ili na wao wameze kurekebishe ile changamoto zao. Vereje leo hii inaharibika *AC* mpaka wapate pesa kutoka kutoka Tanzania Bara, wanataka mafuta yanakwisha hawezi kununua mpaka pale Tanzania Bara. Mhe. Mwenyekiti, naomba katika hilo tuangalie taratibu zinasemaje katika hichi, basi japo asilimia mia mbili ya kile wanachokikusanya kama *policy* ziko vizuri na mambo mengine, basi wapewe na wao *TRA* ili watie chachu zaidi katika kukusanya mapato yao mazuri na kuona kwamba tunapiga mbele.

Mhe. Mwenyekiti, najua mambo mengi wanafanya wenzetu hawa lakini wanafanya kwa udhati kabisa wa nafasi, kupitia kamishna mpya pale, mchapa kazi hodari anaisaidia sana nchi hii katika suala la fedha, basi tumpe nguvu na yeye ajisikie kwamba mchango wake katika serikali hii inathaminika zaidi kupatiwa japo hiyo asilimia mia mbili. *(Makofi)*

Nikiendelea mbele na mchango wangu, nazungumzia *PBZ* pamoja ufanisi mzuri ya *PBZ* lakini bado kuna changamoto ya kuzidiwa kwa wateja kipindi hichi, kwasababu huna siku hata moja utokwenda katika benki zetu hizi zote tatu kwa hapa mjini, ukianza Mwanakwerekwe, Mazizini na hata Darajani kwamba usiingie benki saa moja utatoka saa nne. Kwakweli, ni changamoto najua kuna jengo karibu mtaanza kulijenga pale la Malindi *Motorsell* lifanywe haraka, ili kupunguza hizi changamoto zilizokuwepo pamoja na *ATM* zilizoongezeka pamoja na benki nyingi zilizokuwepo, imeonesha wazi kwamba watu wa Zanzibar wamesajihika kwa nguvu kabisa kutumia Benki ya Watu wa Zanzibar, kwasababu ni benki yao basi hata zile kazi ambazo zinafanyika pale benki, zende kwa haraka zaidi tuondokane kwa kupoteza muda mwingi sana katika Benki yetu ya *PBZ*.

Mhe. Mwenyekiti, najua Serikali yote Zanzibar wafanyakazi wake wanapokelea pesa na ndio maana wamekuwa watu wengi sana katika benki zile, lakini njia mbadala zipo najua kuna *ATM* sasa hivi za kuweka na kutoa, basi *PBZ* tuelekee huko sasa hivi, tumeze kutumia *ATM* zile kwa kuweka pesa na kutoa pesa kama zilivyo baadhi ya *ATM* za benki yengine zitasaidia kupunguza usumbufu wa kwenda benki na mafoleni makubwa.

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea mbele napenda kuchangia kuhusu suala zima la *ZUSP*. Naipongeze serikali kwa awamu ya kwanza imekwenda vizuri watu wengi hapa mashahidi wamesema katika sehemu ambazo zilikuwa zinakero ya kujaa maji, mara kila masika ahame nyumba au ahame mtaa kwa safari hii *alhamdulillahi* hatujapata ile niwapongeze sana. Pamoja na muwendeleze wa mradi ule mimi kwenye jimbo langu umenikusa *ZUSP* kwamba mafuriko safari hii hayakuwepo hata pahali pamoja, lakini kuna changamoto hii baadhi ya nyumba za jimbo

la Jang'ombe zimepigwa "X" kipindi kirefu hawajui nini mustakbali wao lini.

Kwakweli, kama binaadamu angalau na yeye ananze kujitayarisha lini ule mradi wa *ZUSP* utaendelea kwa wale ambao watu wa Jang'ombe barabarani unaendelea mpaka Jang'ombe skuli baadhi yao tayari, lakini wengineo bado lini kutafanyika *compensation*, ili waweze kuangalia taratibu nyengine katika kutafuta maeneo mengine wakati nyie tayari baadae mshawalipa, lini mtawalipa wale watu ili tuone wanaachia yale maeneo kuwa nafuu zaidi kuweza kuhangaikia maeneo mengine.

Sasa hivi wako wanatapa tapa nafsi tu kwa sababu "X" zipo lakini jana nimekutana nao lakini hawajajulikana siku gani aidha mwezi gani au mwaka gani. Mhe. Mwenyekiti, namuomba Mhe. Waziri atwambie basi *atleast* wananisikiliza sasa hivi kuwa nimelizungumza hili suala na serikali imetowa kauli hii, kwamba pengine mwakani Januari au Februari au mwaka huu watapata *compensation* yao, ili waanze taratibu na waondoke pale huku wakiwa wanafurahi, japo kuondoka pale ulipopazoea ni shida, lakini anapokuwa amelipwa ataondoka pale bado ana furahi ningekuomba sana Mhe. Waziri katika hilo.

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea mbele katika mchango wangu nende katika suala zima la upande wa bidhaa ambazo zinasafirishwa kutoka Zanzibar kwenda Tanzania Bara. Mhe. Mwenyekiti, nathubutu kutamka katika Baraza lako hili tukufu, jana tu wakati wa usiku saa tano au sita zimelia risasi baharini, Mnazimmoja jahazi au boti imepakia mzigo bandarini Zanzibar kuelekeza Tanzania Bara, katika ukuta wa bandari ana kila kitu pana ulinzi wote kuna polisi, kuna KMKM, kuna Idara Maalum na Vikosi vyote vilivyohitajika bandarini pale vipo na bahati nzuri mfanyabiashara yule katimiza kila kitu kinachohitajika

mpaka boti ile inaondoka. Kwa bahati nzuri kufika mbele tu hapo Mnazimmoja wamekutana na askari wa Kikosi chetu Maalum cha Kuzuia Magendo. Ikatokea sitohafahamu kwamba ni lazima watu wageuze chombo wende nacho Kibweni.

Bahati nzuri namsifu sana nahodha aliyekuwa jasiri akasema mimi Kibweni siwezi kwenda, kwa sababu siko nilipotoka na mzigo nitakwenda nilipopakia mzigo bandarini twende bandarini. Sasa ikatokea sitofahamu kujibizana pale namna gani zogo lakini mpaka mwisho wa time pale wakabuburusha wakapiga risasi juu wakakubaliana mzigo uje bandarini Malindi umefika. Kwahiyo, mtu tayari ana *manifesto* tayari mtu keshajaza vitu vyake vyote, tayari mtu anayo SD tayari mtu ana *invoice* au *tax invoice*, ambavyo *ZRB* amethibitisha ule mzigo halali kuna tatizo gani kupata *harassment* baharini. Mhe. Mwenyekiti, hiyo ni changamoto kwa wafanyabiashara wetu wa Zanzibar ambao sasa hivi, baada ya changamoto kutoka Tanzania Bara sasa hivi changamoto zinatoka ndani ya Zanzibar wenyewe kwa wenyewe.

Mhe. Mwenyekiti, ukweli usiofichika kwamba kuna zaidi ya madumu 1,600 ya mafuta *ZRB*, yalikamatwa juzi yakapelekwa Kibweni bahati nzuri sasa hivi yako pale *ZRB* na mtu tayari anayo *tax invoice* yake taratibu zote za usafirishaji bidhaa zile amekamilisha njiani tu wanabuburushana twende huku. Mhe. Mwenyekiti, namuomba Mhe. Waziri wa Fedha anaesimamia uchumi wa nchi hii watu wapo wengi sana kutusaidia katika uchumi huu yaani, wafanyabiashara tusiwasumbue hawa watu milango ya Zanzibar mizuri, kwasababu bado amani na utulivu upo, kwahiyo mambo yote wende kwenye *compromise* watu wazungumze yasifike kuvutana katika kitu kama hicho.

Mhe. Mwenyekiti, namuomba Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango kwasababu tunataka kukuza uchumi wetu haya mambo madogo

madogo yanazungumzika awambie au atowe kauli katika kadhia kama hiyo. Kwa upande wa biashara na upande wa fedha kwasababu huwezi kuwa na biashara bila ya kuwa na fedha. Mhe. Mwenyekiti, namuomba sana Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango, nilitaka niseme hilo dogo.

Mhe. Mwenyekiti, nije Wizara ya Fedha. Nakwenda katika Kanuni ya 112 ya Katiba ambayo inamtambua Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali, kama inavyofahamika kwamba atakuwa na utaratibu wa kukagua kila kitu katika Ibara ya 112(1)(c) ya Katiba angalau mara moja kwa mwaka anafanya ukaguzi katika taasisi zetu zote. Ni kweli amefanya ukaguzi kuanzia mwaka 2013, 2014, 2015 hakuna tatizo. Mara ya baada ya pale ilitokea kadhia ya baadhi ya wafanyakazi wa Kada ya Uhasibu Wizara ya Fedha wale waliopata matatizo.

Mhe. Mwenyekiti, kuna malalamiko ya kutotendewa kwa yale waliyostahiki kutendewa. Kama nilivyokuuliza nyuma hapa ukanijibu kwamba umetumia Kanuni ya Utumishi wa Umma Nam. 81 ukaongezea 84(4) lakini watu wale bado kuna manung'uniko kwamba yale masuala yaliyofanyika tukiangali vizuri katika vifungu vyetu hivi vya sheria ya fedha tunakuta vifungu 2005 kifungu 22 kinachomtambua Katibu Mkuu ambaye ni Afisa Mahsusi wa mambo ya fedha mwenye majukumu ya kulipa kila kitu ambaye ana *vote* yake. Hawa walitakiwa baada ya kadhia hiyo wajieleze kwake yeye kama kumpa taarifa.

Mhe. Mwenyekiti, namuomba Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango atakapokuja anambie Makatibu wake wangapi waliopa ile kadhia ambao waliojieleza namna gani ilivyotokea ile kadhia. Pamoja na *CAG* kukagua pengine hajayakuta makosa yale lakini baadaye yakaja makosa yale. Makatibu Wakuu wote ambao wenye *vote*

wanatakiwa waeleze ile kadhia kwake yeye kwa sababu yeye ndiye *responsible* wa ile taasisi.

Vilevile, tukienda mbele wale watu bado wanayo kesi, sasa hivi wanakaribia mwaka, ukimaliza mwezi huu ni mwaka mmoja mzima. Wanahangaika, wana-*hang* hawajui mustakbali wao, jinai si jinai. Lakini ni vizuri kwamba sheria yetu ipo vizuri katika Katiba yetu ya Zanzibar Ibara ya 11(1) tayari wale watu imeshakuwa ni muda mkubwa sana na ibara inasema kwamba kesi za jinai zisikilizwe kutolewa hukumu haraka, ili wale watu waweze kujitambua imeshakuwa siku nyingi, wana familia zinawategemea, wana mambo chungumzima sasa hivi, basi lile jambo lipelekwe kwa haraka ili ijulikane.

Mhe. Mwenyekiti, hakuna hata ubaya kwa mfano kama Baraza la Wawakilishi ikataka pengine ripoti ya ukaguzi wa mwanzo. Hakuna kosa katika hicho kama kweli umeshakamilika uchunguzi, tukajua na sisi ni tatizo gani. Sisi kazi yetu ni kusimamia serikali, basi Mhe. Mwenyekiti namuomba Mhe. Waziri kama kuna uwezekano basi tukaipata ile ripoti ikaja Barazani tukaipitia na tukajua ni nani na matatizo yako wapi kama kunazima au kuna haja ya hivyo. Kwahiyo, namuomba Mhe. Waziri ili kutowabaguwa hawa watendaji wengine wakawa bora wengine si bora.

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea mbele katika hayo hayo, tunajua sheria ziko nzuri sana za fedha, kuna vifungu mbali mbali kama kifungu cha 2005(8)(1) ya kumpa majukumu katibu. Vereje suala kama lile muhasibu analipa Katibu asitambuwe au asiwe na taarifa. Sasa wanapata matumaini au sijui ndiyo ile kauli ya kutishiwa kwamba wewe ukimwaga mchuzi mwenzio atamwaga mboga, Mhe. Waziri inakupa kidogo gati gati katika kulisimamia hili suala likenda haraka ili watu wale wakapata haki yao. Mhe.

Mwenyekiti, namuomba Mhe. Waziri juu ya hicho kwa mapenzi kabisa, najua anaweza, anajiamini na anafahamu suala kama hilo ili alisimamie awaone wale wachache waliofikwa na hii kadhia wanaondokana na changamoto hiyo. Najua Mhe. Waziri ushupavu wake katika hilo.

Mhe. Mwenyekiti, nikisogea mbele niende kwenye mambo ya ukusanyaji wa kodi. Kuna hawa washirika, imekuwa wana kero kubwa sana, unajua kukatwa makato ya *payee* na *ZRB* ukiangalia watu wenyewe mashine sana ni wao wenyewe miili yao na mikono yao. Mhe. Mwenyekiti, namuomba sana Mhe. Waziri katika hilo, tuwaonee huruma wale watu namna gani tuwaangalie kama kuna pahali ambapo tunaweza kupenya tukawasamehe yale makato, kwa sababu wale watu wanafanya kazi hawana *security* yoyote wanatumia nguvu zao. Wanaamka asubuhi wanabeba mizigo, wanachokipata wanagawana lakini hicho hicho kinakatwa pesa na pesa siyo kidogo.

Kwakweli, namuomba Mhe. Waziri tuwaone kwa jicho la huruma kwasababu wana nia njema, baada ya kukaa nje kufanya mambo yasiyokuwa na maana, wamejikusanya kama vikundi kuona kwamba wanafanya kazi ya halali kutumia miili yao, kwa sababu wanabeba mizogo sana bandarini na kufanya shughuli nyengine. Mwisho wa siku wale baada ya miaka kumi, kumi na tano wote wale wagonjwa, kazi ya ubebaji mizigo unaijua ni ngumu. Mwenzangu pale Bamkwe Tumbatu najua ndio fani yao, wanakiuka maiti kwa kubeba mizigo.

Mhe. Mwenyekiti, namuomba Mhe. Waziri katika hili awaonee huruma sana kama kunauwezekano wa kusamehewa wale watu wasamehewe *atleast* kile wanachokipata, jasho lao wafaidike sana.

Sitaki niseme mengi ni hayo machache tu. Nakushukuru sana Mwenyekiti, naunga mkono hoja kwa asilimia 99.9 hii point moja nitamsubiri Mhe. Waziri atakapokuja kunifanyia majumisho nitaimaliza. *(Makofi)*

Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti. *(Makofi)*

**Mhe. Mwenyekiti:** Sasa namwita Mhe. Miraji Khamis Mussa na baadaye anafuatiwa na Mhe. Maryam Thani Juma kwa dakika tano.

**Mhe. Miraji Khamis Mussa:** Mhe. Mwenyekiti, kwanza nikushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Fedha na Mipango kwa mwaka wa fedha 2017/18.

Kwanza naomba nimpongeze sana kaka angu Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango Dkt. Khalid Salum Mohammed na Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu, Katibu Mtendaji Tume ya Mipango pamoja na Makamishna wa Wizara hii, kwa kazi yao kubwa ya kutayarisha bajet lakini pia na uendeshaji mzuri wa Wizara hii. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, naomba nichangie machache sana kwasababu mambo mengi yakwenda vizuri katika Wizara hii na mengi nitakuwa nashauri lakini nakuuliza moja moja tu.

Mhe. Mwenyekiti, niende katika programu ya Usimamizi na Uwekaji wa Mali za Serikali ibara ya 20. Katika eneo hili kuna maelezo mazuri sana ya uendelezaji wa programu hii ambayo inajukumu la ununuzi, utunzaji na uondoshaji wa mali za serikali. Lipo tatizo kidogo ukifuatilia Mashirika na Mali za Serikali hawana mfumo mzuri wa kuweka kumbukumbu na usimamizi wa

mali za serikali. Tunaona ripoti zinapotolewa katika ule mwaka wa fedha unakaguliwa kupitia *CAG* kuna vyombo mle na mali za serikali zinaainishwa ili kutengeneza ile *statement* ya fedha lakini ukenda katika uhalisia ukifuata ule muongozo uliotolewa na Wizara ya Fedha kunako *asset register* zile hukuti zikaenda vizuri na uhifadhi wa mali za serikali.

Juzi tumepitisha sheria najua haya mambo yatakwenda vizuri lakini tunakumbushana katika ustaarabu mzima wa kuonekana kwamba tukilinda vizuri mali zetu basi tutafika mahali pazuri. Kwa sababu sasa hivi hata ule uondoshaji wa mali za serikali haupo vizuri. Taasisi tumezipa mamlaka tumezipa bodi, miongozo tumetoa zinafanya kazi yake, lakini yapo hata magari nayo yanauzwa mazima.

Ndiyo maana nikasema kwamba tunahitaji utaratibu mzuri wa kusimamia lakini na kuweka *record* vizuri kuonekana ule muda wa kuishi ile gari kunako masuala ya *depreciation* yanawekwa vizuri hata mtu akenda kuangalia anajua hili lilikuwepo hapa katika *asset register depreciation* hii lakini tumelifanyia matengenezo hapa lika *add value* wakati mwengine likapungua ile thamani, lakini ikifika pahala tujua hili sasa kwa muongozo ulivyo tunaweza tukaliondosha kama tukaliuza au tukafanya utaratibu mwengine kama ambavyo sheria inasema.

Taasisi nyingi kwa kamati yetu tulipokuwa tunapita nyengine hatukuzikagua kwasababu hazikuwemo katika ripoti lakini nyengine tulibahatika kuzikagua. Mhe. Mwenyekiti, niwapongeze sana *ZIPA* pamoja na Shirika la Umeme, wanaweka kumbukumbu vizuri na kufika tu tukakagua basi tukaona utaratibu mzuri wanaouweka. Lakini naomba sana Mhe. Waziri na maeneo mengine ambayo sheria na miongozo yote tunayoitunga wanapaswa kuifuata basi eneo hili tuweke mambo sawa. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, naomba sasa niende katika aya ya 25 Programu ya Usimamizi wa Huduma ya Mfuko Mkuu wa Serikali. Nimepongeza kule kuna maeneo haya tumekwenda vizuri. Kwakweli, hapa huduma hii ili iyende vizuri maana yake Mfuko Mkuu unatakiwa uingize na utoe, lakini tumeona sijui utaratibu ukoje, hapa sheria kidogo sina kichwani. Sasa mfuko huu hatujaona hata siku moja kuonekana unakaguliwa katika kipimo kile cha utekelezaji wa ile *performance* ya utekelezaji tu ionekane. Namuomba Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango atakapokuja hapa, maana hata juzi tuliuliza humu swali Barazani na aliyeuliza kama sikukosei ni Mhe. Hamida Abdalla Issa, nikawa nasikiliza kwa makini sana.

Mhe. Mwenyekiti, kipindi kilichotokezea kadhia fulani muhusika kwa wakati ule alikuwa nani kunako huwo huwo kuuendesha Mfuko wa Serikali majibu hayakutoka vizuri. Kwahiyo, tufike pahali katika kupima *performance* ya utekelezaji kwenye mapato na matumizi yake katika uendeshaji wa mfuko huu basi nao pia ukaguliwe kama zipo kasoro basi yule ambaye anakagua, anaelekeza, anashauri serikali inaenda. Mhe. Mwenyekiti, naomba tu katika eneo hili sina tatizo sana. Lakini leo mchango wangu zaidi kushauri, ili kuona haya mambo yaende vizuri.

Mhe. Mwenyekiti, naomba niondoke hapo niende kwenye eneo la *ZRB*. Kwanza nimpongeze sana Kamishna na watendaji wa *ZRB*, wamefanya kazi kubwa tumeiyona lakini naomba niongee masuala machache katika eneo hili. Kuna kodi zile tunazopaswa kuzikusanya za *VAT*, kuna maeneo yanafanyika kazi vizuri lakini kuna maeneo Mhe. Waziri naomba niyaongelee kwa kushauriana lakini kwa kuongeza kasi ya utekelezaji, basi tuone sote kwa pamoja tunaisaidia nchi katika kusukuma mbele gurudumu letu hili la serikali yetu.

Mhe. Mwenyekiti, mimi ni mdau wa *NMB* lakini wengine ni wadau wa benki nyengine, unapotumia *mobile bank* ukiuliza tu lile salio unakatwa *VAT* kwanza na mimi mteja niko Zanzibar. *VAT* yangu ninatakiwa nichangie serikali yangu. Katika huduma hii tunaona hii *VAT* kweli inabaki na inakusanywa vipie. Sasa utaratibu huo na kodi hizi za kuonekana kwamba mimi mdau nachangia serikali yangu nimeshakubali kukatwa lakini *VAT* ile nina mashaka nayo. Kwahiyo, kama inakusanywa na wenzetu wale tunaipata vipi na kama hatuipati, ni utaratibu gani ambao tunauwandaa, ili kuona tunafanikiwa.

Lakini juzi nilikuwa nikisikiliza kwa makini lilipozinduliwa suala lile la kukusanya kodi kupitia mitandao ya simu. Nashukuru sana viongozi wetu waliohudhuria na utaratibu mzima na muongozo ulitoka na ndiyo maana hili katika ile mitandao ya simu zile huduma za *VAT* sichangii sana kwasababu nimeshajua muelekeo wake na majibu nimeshayapata.

Mhe. Mwenyekiti, niende katika huduma za vipeperushi vya posta, napo pia tunaotumia *EMS* au *DHL* kutuma mizigo tunatozwa kodi na hapa pia pana *VAT*. Mhe. Mwenyekit, namuomba Mhe. Waziri wakati atakapokuja pia atwambie kunako eneo hili, kwasababu najua zile ni taasisi za kimuungano *VAT* zake zinaingia katika mfuko wa Serikali ya SMT, tunazipataje. Naelewa kuna utaratibu wa mchango wa bajeti tunaupata kupitia SMZ ile 4.5 ya kuja kusaidia ile *budget support* tunayoipata kule, lakini ina *accommodate* na hii, lakini kama haimo sisi tunaipata vipi. Mhe. Mwenyekiti, namuomba Mhe. Waziri atakapokuja kwa kuondoa hofu tu kunako kodi kama hizi tunazipata vipi.

Mhe. Mwenyekiti, pia nije katika kodi ya *incometax* nako kodi hii Mhe. Waziri pia hasa hapa nazungumzia wale wafanyakazi wa

Wizara za Jamhuri ya Muungano wanaofanya kazi Zanzibar, wanastahiki kulipwa *incometax* najua fedha inakuja. Lakini katika kusimamia suala hili kunaushirikishwaji wowote au tunapokea tu fedha tuliyoipata mara hii ni hii, lakini kuna utaratibu gani wakuwatambua wale wachangiaji wa kodi hii kupitia serikali yetu. Mhe. Mwenyekiti, namuomba Mhe. Waziri atakapokuja na hapa kidogo anipe darasa kidogo.

Mhe. Mwenyekiti, nije katika mapato ya serikali katika kusaidia zile mbinu na utekelezaji wake. Nije katika eneo lile la gawiyo la benki. Kuna benki tunafanyakazi nazo na zinatoa huduma kama *NMB, CRDB, EXIM, BARCLAYS* na nyenginezo. Kuna gawiyo la faida wanapata lakini ile *business* yao wanafanya kwetu, utaratibu huu ukoje nilikuwa naona huku kwenye kitabu kikubwa kuna fungu ambalo linatokana na Benki Kuu.

Lakini huduma ipi ambayo inakwenda kule, basi naomba Mhe. Waziri aje atueleze tu ili kuweka sawa yale mazingira ambayo hatunayo sasa. Kwakweli, najua mimi na wenzangu hatujafika pahali pazuri, nimeona humu, lakini nasema kunako eneo hili lile gawiyo lao la faida sisi tunapata nini. Hivyo, isijekuwa hii pesa inakwenda moja kwa moja haiwezi kuja kukusanywa huku ambako wanafanya biashara zenyewe.
Mhe. Mwenyekiti, namuomba Mhe. Waziri anifahamishe juu ya hili na nilieleza katika utaratibu wa kawaida, najua kuna *GBS* (*General Budget Support*) lakini nasema ile kama sikosi iliamuliwa tokea mwaka 1992 na makubalianao ambayo yalisimamiwa na *IMF*. Mimi sina tatizo na hii, lakini migao hii fungu lake linakwenda wapi. Mhe. Mwenyekiti, namuomba Mhe. Waziri atakapokuja anaeleze.

Mhe. Mwenyekiti, nije katika eneo moja tu katika kitabu kikubwa nilikuwa nakipitia hichi ambacho tulikuwa tunakuja kupitisha

mafungu, kuna fungu ambalo liko katika Idara ya Mipango Sera na Utafiti kuhusu mapato ya Uhamiaji. Nyuma huko Uhamiaji walikuwa wanakadhia ya ujenzi na wamejenga wamemaliza kuna makubaliano ndani yake inasemekana maana ni lazima niseme hivyo, sija-*prove* na sijawahi kuingia katika hicho kikao. Lakini niseme tu kunako eneo hili kuna makubaliano ya kuzidisha *percent* katika Idara ya Utawala yaani, kubakiwa na lile gawiyo mpaka huduma yao ya ujenzi imalize. Sasa hivi muda mrefu wamemaliza bado tunakwenda na utaratibu ule ule au tunapata asilimia ile ya mwanzo kama makubaliano ambayo tulikuwa tumekubaliana.

Nikiendelea na mchango wangu Mhe. Mwenyekiti, naomba niende kwenye kitengo cha mapato ambacho kinasimamiwa sana na *ZRB*. Kuna uhaulishaji wa mahoteli niliuliza katika bejeti iliyopita. Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira akanijibu ule uhaulishaji wa kuondoa jina la mtu mmoja kuweka jina la mtu mwengine. Lakini uhaulishaji niliokuwa nauliza mimi na sikupiga buti kwasababu nilifika pahala nikasema kile lichokichangia labda hajakielewa na ikiwa hajaelewa maana yake atanijibu vile ambavyo kaelewa yeye.

Sasa leo nalifafanua vizuri zaidi. Mhe. Mwenyekiti, nilichokikusudia katika suala la kuuza hoteli yaani, tuna *sale asset*, lakini na suala la kukodisha uongozi (*management transfer*). Katika maeneo haya mawili utakakokwenda maana yake kuna *liabilities* unazihamishia kwa mtu mmoja kwenda kwa mtu mwengine, kuna kodi ndani yake. Najua kuna uzito mkubwa sana wa kupata taarifa, lakini serikali lazima ifike pahala tujipange katika eneo hili, kwasababu mahoteli mengi aidha yamebadilisha uwongozi au yameuza kabisa.

Sasa sijui utaratibu gani ambao Mhe. Waziri, ambao wizara yake imejipangia kupitia taasisi husika kwenda kukusanya vizuri eneo hili. Lakini kama wanatupiga chenga huku basi tuone tuna mikakati gani ya kibalozi, kwasababu hawa wengine wanakuja kuuziana kwetu, lakini wengine wanauziana nje mali zao. Sasa wale wanaouziana nje sisi tuna mabalozi tunafanya kazi nao, lakini lazima tufike pahala tufanya kazi nao kwa ukaribu, ili tuone wale wote wana *asset* kwetu sisi kuna taasisi karibu nne taarifa zao zipo kwa Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora kuna Kitengo cha Usajili, ukenda kule taarifa zipo, lakini ukenda *ZRB* zipo, *ZIPA* zipo, sasa ukaja *ZRB* kwenyewe wao ndio wanaosimamia *ORIC*.

Kwahiyo, maeneo haya mawili ushirikishwaji wa kupata taarifa ukoje, miye sina tatizo na eneo hili, lakini nachangia ili kuweza kusaidia zile fikra endelevu tunatumia utaratibu gani, ambao nahisi sana hawa wanapouziana wanakutana nje kama wanabadilisha uongozi huko nje huku wanakuja kukamilisha, zile ofisi zetu za kibalozi tunazitumiaje katika kuweza kusaidia kadhia hii, ili hizi pesa zetu tuzipate kwasababu tunapoteza pesa nyingi sana. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, namuomba Mhe. Waziri atakapokuja anambie katika utaratibu mzima wakionekana aa! Basi tunapofika pahala katika kuuza tunafanikiwa labda katika utaratibu huo nilioushauri mimi, lazima ile *Diplomatic Relation* hapa ipatikane na kama haipatikani maana yake tutarudia kule, maana narudia tena kusema si wingi wanaouziana ndani ya nchi yetu wanauziana nje. Kwahivyo, miradi yetu tukawapa mabalozi watatusaidia mbinu ya kuongea na serikali zile, ili kuona hawa wanapouziana katika mabenki wakifanya *transfer* huu mradi au hii *asset* ilikuwepo wapi, basi alau na sisi tupate chetu shida tu tuengeze fedha zetu mimi sina tatizo sana.

Lakini mwisho Mhe. Waziri naomba niendelee kupongeza kupitia mradi wa *ZUSP* ibara ya 50 mradi huu unaendelea vizuri kule Jimbo la Chumbuni mambo yamekwenda vizuri kulikuwa na nyumba zinajaa maji lakini sasa hivi kila kitu kinaenda sawa. Mhe. Mwenyekiti, niwapongeze sana walobuni mradi lakini walotekeza mradi huu akiwemo na yeye Mhe. Waziri. Lakini pia naomba niulizie tu kidogo, kwasababu wakati kunatengenezwa Chumbuni nilikuwa nikipita hii njia ya Kwamchina kuna mtaro pale hasa watu wa Magomeni, sasa tuwone katika utekelezaji wa mara hii umalizaji wake uko vipi.

Mhe. Mwenyekiti, namuomba Mhe. Waziri atakapokuja anambie lakini ile programu nzima ya uendelezaji katika ambao mradi huu haujaanza katika bonde la Mwanantenga, bonde la Sogea na Nyerere, haya yako katika programu ipi kwenye fedha hizi ambazo tumeziona katika kitabu kikubwa au labda au kuna progamu ya mwaka ujao wa fedha. Sasa namuomba Mhe. Waziri atakapokuja kunako eneo hili atushibishe kidogo maelezo, ili tuone wananchi wetu wa Magomeni mara nyengine tukija tukawaomba wanatupigia kura vizuri.

Mhe. Mwenyekiti, naomba sana kuunga mkono hoja kwa asilimia mia moja ahsante sana. *(Makofi)*

**Mhe. Mwenyekiti:** Ahsante sasa ninamwita Mhe. Maryam Thani Juma atachangia kwa dakika tano kama alivyoomba na Mhe. Suleiman Makame Ali ajitayarishe kwa dakika tano kama alivyoomba ahsante sana.

**Mhe. Maryam Thani Juma:** Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa fursa hii ya kuzungumza machache juu ya bajeti hii ya Wizara ya Fedha na Mipango.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza kabisa niende moja kwa moja kwenye ukurasa wa 28 kifungu cha 50 Mradi wa Kuimarisha Huduma za Jamii Mjini *ZUSP*.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza kabisa napenda kuipongeza Wizara hii ya Fedha wakishirikiana na Mradi huu wa *ZUSP*, na vilevile napenda kuipongeza sana Baraza la Mji la Wetu ama Manispaa ya Wetu kwa ujenzi mkubwa wa Soko la Kisasa la Biashara la Wete. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, soko hili limejengwa kwa muda mrefu kupitia kwa maradi huu wa *ZUSP* na soko hii tayari Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Ali Mohamed Shein tayari kishalifungua. Lakini hadi sasa Mhe. Mwenyekiti hatujaona matumizi ya soko hili na wananchi wa Wilaya ya Wete wana matumaini makubwa sana na soko lao la Wete ili kuweza kutumika kwa kufanyia biashara zao.

Lakini Mhe. Waziri katika hotuba yake amesema mradi huu utandelea na maelezo yake yamo katika kitabu cha bajeti kikubwa. Mhe. Mwenyekiti, naomba nimueleze Mhe. Waziri, soko lile la Wete ujenzi wake haujakamilika na ukiangalia soko hili mvua hizi zilizopita ilikuwa likivuja sana. Hivyo, naomba nimuulize Mhe. Waziri kwamba soko hili litamalizika lini na liko chini yake na linaendelezwa na Mradi huu wa *ZUSP*. Je, Mhe. Waziri katika bajeti hii mradi ule umezingatiwa. Mhe. Mwenyekiti, namuomba Mhe. Waziri atakapokuja anieleze haya ambayo nimeyazungumza kuhusiana na Soko la Wete.

Vilevile nielekea katika ukurasa wa 31 kifungu cha 53 tumeambiwa kwamba mradi umepangiwa kutumia jumla ya shilingi 5.57 bilioni kwa ajili ya utekelezaji wa programu

mbalimbali ya ujenzi na ukarabati wa majengo. Mhe. Mwenyekiti, tumeona kwamba jengo la Hoteli ya Wete ambalo ni jengo la serikali lakini Mhe. Mwenyekiti jengo lile liko kwa muda mrefu na halitumiki, jengo lile ambalo lilikuwa zuri sana na kwa kweli lilikuwa likivutia katika mji wetu wa Wete. Lakini hadi sasa jengo lile lipo na liko vilevile halitumiki na kwenye kitabu hiki ameeleza kwamba ujenzi na ukarabati wa majengo ya serikali, lakini sikuona kwamba jengo hili litafanyiwa ukarabati wowote ama litatumika ama vipi. Kwahiyo, namuomba Mhe. Waziri atakapokuja anieleza kwamba wizara ina mpango gani ya kuliendeleza jengo lile likatumika kwa ajili ya shughuli za serikali ama shughuli zozote, bali lisikae vilevile na likazidi kuchakaa.

Mhe. Mwenyekiti, katika jengo ambalo liko Wete pia ni jengo la sinema. Mhe. Mwenyekiti, jengo lile la sinema tunataka tujuwe kwamba liko serikalini ama analo mtu binafsi anatumia, kwasababu nalo jengo hili ni la serikali lakini kwa sasa hatujui mmiliki ni serikali ama ni nani. Kwahivyo, tunaomba kujuwa kama ni serikali fedha zinazopatikana zinaingia sehemu gani. Mhe. Mwenyekiti, namuomba Mhe. Waziri atakapokuja atuelezee kuhusiana na jengo la sinema ya Wete pamoja na Hoteli ya Serikali ambayo iko Wete bila ya kutumika. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, nilikuwa na hayo machache tu. Hivyo, namuomba kwa heshima Mhe. Waziri atakapokuja anieleze, ili wananchi wa Wilaya ya Wete waweze kujuwa juu ya majengo yale ya Serikali ambayo yapo katika Wilaya yetu ya Wete. Ahsante Mhe. Mwenyekiti. *(Makofi)*

**Mhe. Mwenyekiti:** Ahsante Mhe. Mjumbe, kwa kutumia muda wako vizuri. Sasa ninamwita Mhe. Suleiman Makame Ali naye ana dakika tano na baadaye nitamwita Mhe. Said Soud Said

(Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum) kuchangia muda utakakuwepo kabla ya kuakhirisha. Ahsante.

**Mhe. Suleiman Makame Ali:** Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuweza kuchangia hotuba hii ya Waziri wa Fedha na Mipango.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza kabla ya kuchangia ingekuwa kama Kanuni yetu hairuhusu ya kutowa shukrani. Lakini nakuomba uniruhusu niweze kuwapa pole wananchi wa Pemba hususan wale jana waliopata msiba baada ya gari kuanguka pale maeneo ya Kiuyu Minungwini na wananchi wangu ambaye ni mpiga kura wangu kutoka kule katika kijiji cha Michugwani kufariki dunia, Mwenyezi Mungu amuweke mahala pema peponi na siye tuko nyuma yake.

Mhe. Mwenyekiti, badala ya hapo pia niwape pole wafiwa wa marehemu Mzee wetu Mwenyekiti mstaafu wa Chama cha Mapinduzi Mzee Khamis Mkadara pale Wawi, nao pia nawaombea kwa Mwenyezi Mungu awape subra, kwasababu hiyo ni mipango ya Mungu na sisi tuko nyuma yake tunafatana safari yetu sote.

Mhe. Mwenyekiti, badala ya hapo niende katika mchangio wangu kwenye kitabu hiki ukurasa wa 21 Mfuko wa Barabara.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza nampongeza sana Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango, jembe, mtenda kazi, mahiri, makini na mbunifu. Mhe. Mwenyekiti nimuombe Mhe. Waziri azidi kufanya kazi tuzidi kumuamni kwasababu yeye ndiye mwenye fedha, mipango, pamoja na kila kitu. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, nimuombe Mhe. Waziri kwamba asivunjike moyo na pengine *inshaallah* kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu badala ya hapo alipo akamuweka pakubwa zaidi. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, niende kwenye Mfuko wa Barabara moja kwa moja. Mhe. Mwenyekiti, tunaziona barabara zinavyotengezwa kama alivyosema Mhe. Mohamed Said Mohamed wananchi wengi labda walikuwa hawajui kwamba barabara ya Fuoni imetengezwa kupitia katika Mfuko wa Barabara, lakini pia si ya Fuoni tu kuna na barabara ya Kiwani imetengenezwa kupitia Mfuko wa Barabara.

Lakini Mhe. Mwenyekiti, kitabu kilichopita ukurasa wa 49 imeonesha barabara ambazo kwamba zimetengenezwa kwa kiwango cha lami kwa mwaka 2015/2016. Kwahiyo, namuomba Mhe. Waziri katika mwaka huu katika Mfuko wa Barabara aiangalie kwa jicho la huruma ile barabara ya Ndagoni, ambayo kila siku naipigia kelele humu kwenye Baraza.

Mhe. Mwenyekiti, nikitoka hapo naenda katika Ujenzi wa Ofisi za Serikali. Mhe. Mwenyekiti, kwanza nipongeze serikali kwa kuona umuhimu wa kujenga majengo ya serikali na kuachana kukodi. Mhe. Mwenyekiti, hususan kule Pemba pesa nyingi sana zinakwenda kwenye kukodi majengo ya serikali, lakini leo hii kunajengwa majengo ambapo kwamba jengo lile moja litachukuwa si chini ya wizara tatu. Kwahiyo, naipongeza sana serikali kwa kuliona hili, kwasababu ni pesa za wananchi zile ambazo zimetarajiwa kukodi zitafanyiwa mengine ya kimaendeleo. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, nikitoka hapo niende kwenye Mfuko wa Hifadhi ya Jamii (*ZSSF*). Mhe. Mwenyekiti Ilani yetu ya Chama cha Mapinduzi inasema kwamba Serikali ya Mapinduzi ya

Zanzibar chini na Uongozi wa CCM imefanya juhudi kubwa ya kuendeleza ujenzi wa nyumba bora kwa ajili ya makaazi ya wananchi. Mhe. Mwenyekiti, napenda kunyanyuka na Ilani ya CCM, kwasababu ndiyo tunayoitekeleza, inayotekelezeka na inayokubalika katika nchi hii ya Tanzania. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, makaazi ni muhimu sana kwa wananchi lakini leo *ZSSF* wanajenga nyumba zile, nawapongeza sana, lakini sasa zile nyumba zinakuwa ni bei kubwa sana mwananchi wa kawaida hawezi kuimiliki nyumba ile. Kwahiyo, Mhe. Mwenyekiti niwaombe *ZSSF* waangalie na wananchi wa kawaida wenye kipato cha chini kama mimi hivi na wenzangu wengine. Mhe. Mwenyekiti, naiomba sana *ZSSF* wawangalie wananchi ambao kwamba hawawezi kumiliki nyumba zile, waweze kuwajengea angalau nyumba au kuwapunguzia bei ikawa bei ya nafuu. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, nikitoka hapo niende Mamlaka ya Uwekezaji na Vitega Uchumi. Mhe. Mwenyekiti, Waheshimiwa Wajumbe wengi wamesema hapa kwamba Mamlaka ya Uwekezaji na Vitega Uchumi kuna maeneo mengi sana ya Wawekezaji hapa Zanzibar na ukiangalia Zanzibar yetu ni ndogo lakini leo kuna maeneo yamewekewa *beckon* tangu sijui ilipoundwa dunia niseme hivyo, maeneo yale hayaendelezwi, hayajengwi na Mhe. Omar Seif Abeid alitoa mfano, lakini Mhe. Mwenyekiti na mimi katika Jimbo langu Ndagoni kule Mkumbuu nadhani Mhe. Waziri wa Fedha anakujua kabla ya kufika kwenye umeme.

Kwakweli, kuna maeneo pale ya kujenga mahoteli yamekaa tuu mpaka leo hii hata wale wakulima waliokuwa wakulima viazi kwenye eneo lile pia hawalimi tena, sasa faida itakuwa haionekani. Kwahiyo, namuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Mwenyekiti, aliangalie na alichukwe hili alifanayie kazi

kwamba waliokusudiwa kuwekeza basi wawekeze hawakusudia kuwekeza watoe yake maeneo wapewe wawekezaji na wazalendo wanaoweze kufanya hivyo.

Mhe. Mwenyekiti, mimi sina mengi sana isipokuwa ni hayo namuomba sana Mhe. Waziri aendelee kuwatumikia wananchi kama alivyoaminiwa na Mhe. Rais na huwenda *inshallah* kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu akampa nafasi ya juu zaidi na sisi tuko nyuma yake tunamuombea dua *inshalllah* Mhe. Mwenyekiti naunga mkono asimilia mia kwa mia. *(Makofi)*

**Mhe. Mwenyekiti:** Ahsante Mhe. Suleiman Makame Ali. Sasa ninamwita Mhe. Said Soud Said *Member* wa Baraza la Mapinduzi aweza kuchangia machache. Mhe. Mhe. Said Soud Said (Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum) karibu sana.

**Mhe. Said Soud Said (Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum):** Nashukuru Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipatia nafasi hii ili niweze kutowa mchango wangu katika wizara hii. Wizara ambayo ni mama na Wazanzibari wote tunategemea wizara hii, kwa maana ya kwamba tayari inaoneka kwamba inafanya kazi yake vizuri mno na maslahi ya nchi hii yanaonekana. *(Makofi)*

Lakini pamoja na yote nachukuwa nafasi ya kumpongeza Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi pamoja na kumpongeza Mhe. Makamu wa Pili wa Rais kwa kushirikiana vyema katika kuendeleza wizara hii ifanye majukumu yake vile inavyotakiwa. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, wizara hii tayari inaonekana kwamba ina uwezo mkubwa ambayo imeweze kuwafanikisha Wazanzibari kufikia malengo yao kwa asilimia 99.5. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, wizara imeweza kufanikiwa kutengeneza mambo makubwa sana katika nchi yetu ambayo wenzetu waliopita walibeza na wakaona kwamba hakuna sababu ya kufanyika mambo kama hayo. Lakini kiukweli ni kwamba kutokana na kuwepo kwa Ilani ya Chama cha Mapinduzi ambayo ndiyo inayoielekeza Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kutekeleza majukumu yake yananyotakiwa na yale yote yanayofanyika, yanafanyika kutokana na kwamba watu wanatekeleza ilani waliyoahidi wananchi.

Mhe. Mwenyekiti, wizara hii imeweza kufanikiwa kukusanya mapato ambayo yamemuwezesha Mhe. Rais wa Zanzibar kuweza kuwasaidia wazee wa nchi hii elfu ishirini, kila mwezi bila ya jasho haya ni mafanikio makubwa sana ya wizara hii, na kama wizara hii isingekuwa na watu mahiri au watendaji wake wasingekuwa mahiri basi haya yasingeweza kufanikiwa. *(Makofi)*

Vilevile, wizara hii imeweze kufanikiwa kukusanya mapato ambayo yamemuwezesha Rais wa Zanzibar kutangaza kuongezeka kwa mishahara katika visiwa vyetu hasa wale watu wa kima cha chini, wameweza kufanikiwa sana na ongezeko kubwa la mshahara kwa hiyo Wizara ya Fedha mimi naweza kusema kuanzia waziri mpaka watendaji wote wanapa pongezi sana. *(Makofi)*

Katika hali ambayo si ya kawaida wizara hii imeweza kufanikiwa kwa haraka haraka kutengeneza mambo makubwa ikiwemo barabara ya Fuoni, barabara ya Kiwani Pemba, barabara ya Mgelema na barabara ya Ngomeni kwasababu fedha zimetumika ndiyo mafanikio yale yakapatikana, bila ya kukusanywa kwa fedha basi mafanikio haya yasingeweza kupatikana. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, mbali na hayo tumeweza kuona kwamba wizara hii imeweza kufanikiwa kuweza kuwasaidia Wazanzibari, kujikwamuwa katika hali ambayo si ya kawaida kwa kuweza kufanikiwa, kupata yale ambayo yamewawezesha kufikia pahala pazuri katika kutengeneza mambo yao ya kawaida.

Mhe. Mwenyekiti, ni vyema sasa tunasema kwamba ka jitihada zetu sisi kama mawaziri, pamoja na wawakilishi tuna ulazima wa kusaidia kuona yake yote tunayoyapigia kelele tunayasimamia. Hivyo, haiwezekani kuona kwamba vyanzo vya mapato vinapotea halafu sisi tukasubiri bajeti kuja kuleta malalamika kwenye bajeti, hapana, kiilivyo ni kwamba kila mwakilishi ana haki ya kuisimamia mapato ya serikali hii yasipotee na milango iko wazi.

Sasa yule ambaye anaona hana uwezo wa kufika kwa waziri sisi mawaziri ambao hatuna wizara maalum tuko tayari kusikiliza, na mukituletea hoja zenu kuhusiana na vyenzo vya mapato vinavuja sisi tutafika kwa Makamu wa Pili wa Rais kumueleza, ili serikali ifanikiwe kukusanya mapato ya nchi hii yasipotee. Kutokana na hali hiyo, naamini kwamba kwa mashirikiano yetu ya pamoja Mhe. Mwenyekiti, bajeti hii hata haihitaji mabuti maana kila mtu kafurahi. *(Makofi)*

Nyongeza za mishahara zipo, wananchi wanafaidika, mahospitali wanapata madawa, Abdalla Mzee imejengwa, sioni sababu mimi ya kupiga mabuti kwa wizara hii yaani, hii wizara tayari imeshajiosha na sisi sasa hivi tuipe kila aina ya *big up*, ili iweze kupita bajeti yake na tufikie pahala pa kusema kwamba mwaka ujao tuone maendeleo yameongezeka zaidi.

Mhe. Mwenyekiti ahsante sana. *(Makofi)*

**Mhe. Mwenyekiti:** Ahsante Mhe. Waziri. Sasa nitamwita Mhe. Juma Ali Khatib (Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum).

**Mhe. Juma Ali Khatib (Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum):** Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi hii nakushukuru sana.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza nachukua nafasi hii kumpongeza Waziri wa Fedha na Mipango kwa kusimamia kazi yake vizuri na kuwajibika vizuri. Mhe. Mwenyekiti, lakini unapompongeza Waziri wa Fedha basi lazima utampongeza Katibu Mkuu ndugu yetu Khamis Mussa pamoja na Katibu Mipango somo yangu Juma Reli na Manaibu wao na Wakurugenzi wao kwa kweli wanashirikiana pamoja katika kufanya kazi nzuri ya kutekeleza Ilani ya CCM. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, leo Serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar inatembea kifua mbele kutokana na wizara hii, na ukiipongeza wizara hii lazima tumpongeze Kamishna wa *ZRB*. Pia nachukua nafasi hii kumpongeza Naibu Kamishna wa *ZRB* na wasaidizi wao wote. Kwakweli, Mhe. Mwenyekiti serikali bila ya pesa inakuwa haiwezi kutekeleza wajibu wake. Lakini wizara hii na Makamishna hawa wanakusanya kodi vizuri na wanafanya zile ahadi za Mhe. Rais wa Zanzibar Dkt. Ali Mohammed Shein za kuongeza mishahara, kutoa pensheni kwa wazee zitekelezwe kwa wakati. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, sote tunakumbuka katika awamu za nyuma zilizopita za nchi yetu kulikuwa na wakati mishahara inachelewa inafika miezi miwili bado mshahara haujapatikana. Lakini ni jambo la kufurahisha katika awamu hii Serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar haijapata mshahara kuchelewa, kama alivyosema mwenzangu hapa ahadi ya Mhe. Rais ya kuongeza

mishahara imekuja kwa wakati. Lakini yote haya ni kutokana na kwamba wafanyakazi wetu na viongozi wetu wa *ZRB* na Wizara ya Fedha wanafanya kazi nzuri na kwa uadilifu mkubwa. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, sisi viongozi wa serikali hutembea kifua mbele kutokana na kwamba uchumi wetu unakua, kutokana na hawa wasimamizi wazuri. Mhe. Mwenyekiti, kama mapato yanavuja basi ni sawa sawa na kuchukua maji kuyatia kwenye tenga la samaki. Lakini tunawapongeza nataka niwaombe sasa wasimamie wale wasaidizi wao kwa sababu kama tunavyoambiwa na Mhe. Rais wa Zanzibar Dkt. Ali Mohamed Shein tusifanye kazi kwa mazoea. Mhe. Mwenyekiti, bado kuna baadhi ya watu wachache wanapewa madaraka ya kusimamia nafasi zao, bado wanafanya kazi kwa mazoea. Sasa nawaomba tufanye kazi kwa kasi aliyonayo waziri, na kasi aliyonayo Katibu, na kasi aliyonayo Katibu wa Mipango kuonesha uzalendo kwa nchi yetu na taifa letu. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, pia mimi nataka kuipongeza Benki yetu ya Watu wa Zanzibar (*PBZ*). Kwa kweli ilifika wakati benki yetu ilikuwa katika hali mbaya, lakini sasa hivi *PBZ* mimi nawapongeza sana wanafanya kazi nzuri pamoja na changamoto ndogo ndogo lakini lazima tukisifu chetu. Mhe. Mwenyekiti, *PBZ* wanafanya kazi nzuri sana, imekuwa sasa hivi ni kimbilio la wanyonge. Wamesema Waheshimiwa Wawakilishi wenzangu hapa na mimi naunga mkono kwamba waendelee kufungua matawi, waendelee kufungua mashine za *ATM* kuwarahisishia wananchi wetu wa Zanzibar, wakulima, wavuvi na wafanyabiashara, lengo letu sote tuone kwamba hii benki yetu inakwenda mbele zaidi. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, wizara hii si wizara ya kuipigia debe sana kwa kweli, kwasababu hawa wawakilishi wote kila mmoja anajua

umuhimu wake, tunajua faida zetu. Kwahiyo, niwaombe kwamba itakapofika wakati wa kupitisha mafungu hakuna sababu ya kupiga buti kutokana na hii hotuba iliyokuwemo humu na uhalisia wenyewe. Mhe. Mwenyekiti, sasa niwaombe Waheshimiwa Wawakilishi wenzangu tupitishe hii bajeti kwa asilimia mia juu ya mia.

Vilevile, naamini Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango atakapofika hapa zile hoja zote za Waheshimiwa Wawakilishi atazijibu vizuri na kwa ufasaha, lakini mwisho wa siku tushirikiane sote kwa pamoja tupitishe bajeti hii iliyomo katika kitabu hiki, kwasababu inaridhisha, na inatia moyo na inafurahisha.

Ahsante Mhe. Mwenyekiti, nashukuru naunga mkono hoja mia kwa mia. (*Makofi*)

**Mhe. Mwenyekiti:** Ahsante Mhe. Waziri. Sasa namwita Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira.

**Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira:** Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako na mimi naomba nichangie bajeti hii ya hotuba ya Wizara ya Fedha na Mipango. Kwanza kabisa naomba nimshukuru sana waziri na watendaji wake kwa kazi kubwa ambayo wanaifanya kuhakikisha kwamba nchi yetu hii tunakwenda nayo katika maendeleo ya hali ya kiuchumi. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, mimi naomba sasa nielezee mchango wangu ndani ya hotuba hii. Naomba niendelee kwa kuishukuru sana *ZIPA* pia kwa mashirikiano yao makubwa wanayotupa katika kuhakikisha kwamba nchi hii inaendelea katika suala zima la uwekezaji. Naomba nikiri kwamba *ZIPA* wanafanya kazi kubwa, wanafanya kazi hiyo kwa pamoja wakishirikiana na watu wangu, na mimi ninachoamini katika kulinda maslahi ya nchi hii amani na

utulivu ni muhimu zaidi. Wawekezaji tunawapenda sana tunataka waje, tunawakaribisha lakini waje kwa nia njema na waje kwa misingi inayoeleweka, na pia tuangalie mazingira yetu.

Mhe. Mwenyekiti, tumepiga kelele sana hapa kuhusu suala zima la mazingira, mazingira yetu tunayaona, hali yetu tunaijua, kisiwa chetu tunakifahamu, bahati mbaya sana kisiwa hiki kimezungukwa na bahari, lakini *resources* tulizonazo kwa maana ya malighafi na vitu vyengine tulivyonavyo katika mazingira ya uwekezaji, viwanda na biashara nyengine pia inabidi yote tuyatizame na tuyaangalie.

Mhe. Mwenyekiti, kama hiyo haitoshi wakati tunaawapokea wawekezaji kuna vigezo ambavyo pia vipo na utaratibu ambao umewekwa kwa mujibu wa sheria na kwa mujibu wa vigezo ambavyo tunavyo. Mhe. Mwenyekiti, mwekezaji yeyote anapokuja nchini kitu cha kwanza lazima tumtizame uhalisia ile *due diligence* lazima tuifanye ili tujue, lakini tuangalie *capacity* ya uwezo wake katika kufanya kazi kwa sababu kuna watu wengine wababaishaji pia tunawaona ndani ya maeneo, mtu analichukua ardhi kubwa, anachukua ardhi yetu na anaendelea kuiuza.

Kwahiyo, vitu hivi vyote Wizara hii ya Fedha imekuwa makini katika kuviangalia na tukiongozana kushirikiana katika kuelekeza ndani ya wizara yangu. Hivyo, naomba sana kuwapongeza watu wa Wizara ya Fedha waendelee kuwa makini, tuendelee kufanya kazi kwa mashirikiano na tuweze kuendeleza hali ya Zanzibar katika suala zima la uwekezaji.

Mhe. Mwenyekiti, jambo la mwisho ambalo nataka kulizungumza katika sekta hii ya fedha na uchumi nilikuwa naona kabisa sasa hivi Wizara ya Fedha na Mipango inafanya kazi kubwa ya ziada hasa kwenye Tume ya Mipango, katika kuwakaribisha wageni.

Mhe. Mwenyekiti, kuna maeneo ambayo Tume ya Mipango inafanya moja kwa moja katika ile programu ya *PPP*, kwa kweli wanafanya kazi kubwa na tutatoa wito kwa wawekezaji wenye nia njema kwa Zanzibar basi waende Tume ya Mipango, na wale watu wote wenye watu ambao wanahitaji kuekeza ndani ya nchi hii basi wawapeleke Tume ya Mipango, kuna programu nyingi ambazo tunazihitaji nchi hii ni nchi inayohitaji maendeleo lakini ni nchi salama na ni nchi ya amani. Kwa hiyo, wale wote wanaotaka kuekeza basi pia tunawakaribisha katika maeneo lakini katika hali ya usalama wa wananchi wetu.

Mhe. Mwenyekiti, naomba niseme tunahitaji maendeleo, tunahitaji fedha lakini pia tunataka kuwalinda na kuwahifadhi wananchi wetu wa Zanzibar, hatuwezi kuwa na fedha nyingi tukawa na wawekezaji lakini nchi ikawa haiko katika hali ya amani, hili litakuwa sio suala jema wala sio suala sahihi. Kwa umoja wetu sote tutoe wito kuwa na wawekezaji ambao ni bora na wenye nia thabit.

Katika suala hili naomba nimalizie kwa kusema kwamba kuna mambo mengine ambayo pia tunaangalia mambo ya mazingira. Mambo ya mazingira haya kama tunaona yanaathari kubwa kwasababu ya nchi yetu, basi pia tunayaangalia na pale tutapoona kwamba mazingira haya hayastahiki basi tunayaacha.

Mhe. Mwenyekiti, niwaombe sana Waheshimiwa Wajumbe nimalizie kwa kusema naunga mkono hoja na niwaombe Wajumbe wa Baraza lako tukufu hili waendelee kuunga mkono hoja hii mia juu ya mia, na tuweze kuipitisha bajeti hii ya Wizara ya Fedha na Mipango kwa utulivu na kwa usalama zaidi. Naomba kuunga mkono hoja ahsante sana. (*Makofi*)

**Mhe. Mwenyekiti:** Ahsanteni Waheshimiwa Wajumbe, kwa utulivu wenu na michangio yenu kwa Wizara ya Fedha na Mipango, hii ni wizara mama inayotuwezesha kuweza kukaa tukajadili kwa utulivu. Niwapongeze sana kwa muda huo mlipokuwa mkifanya hivyo.

Waheshimiwa Wajumbe, mbele yangu pana matangazo mawili. Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira anawatangazia Waheshimiwa Wajumbe wote wanaotaka viwanja Pemba wakaorodheshe majina yao kwa Katibu wa Baraza viwanja vipo Tumbe na Mfikiwa Pemba. *(Makofi)*

Tangazo jengine linatoka kwa Mhe. Hamza Hassan Juma Mwenyekiti wa Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi, anawaomba Wajumbe wa Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi wakutane mara moja baada ya kuakhirisha kikao hiki hapa hapa ndani, kuna ujumbe fulani wanataka kupewa.

Baada ya hayo naomba nichukue fursa hii tena kuwashukuru na kuweza kuliakhirisha Baraza hili hadi kesho saa 3:00 asubuhi. Ahsanteni sana.

*(Saa 8:46 mchana Baraza liliakhirishwa hadi tarehe 09/06/2017 saa 3:00 asubuhi)*